

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TISA

Kikao cha Tatu – Tarehe 9 Novemba, 2017

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Tukae, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mkutano wetu wa Tisa, leo ni Kikao cha Tatu. Katibu. *(Makofi)*

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Kama ilivyo ada swali la kwanza litaulizwa na Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbowe, namuona yupo leo.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Waziri Mkuu swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu nina imani utakubali kwamba usalama wa nchi na mahusiano mema miongoni mwa raia ni tunda la mahusiano mazuri kati ya vyama vya siasa, Serikali na vyombo vyote vya dola.

Mheshimiwa Spika, siku za karibuni kumekuwa kuna mwendelezo wa matukio mengi yanayovunja usalama huo,

yanayovunja amani na yanayojenga chuki miongoni mwa vyama vya siasa na kuharibu utengamano wetu wa kitaifa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tukio la kushambuliwa kwa risasi kwa nia ya kuu kwa Mheshimiwa Tundu Anthipas Lissu, Mbunge na Mnadhimu wa Kambi ya Upinzani Bungeni limezua hofu kubwa sio tu kwa Taifa ila katika Bara zima la Afrika na Jumuiya ya Kimataifa. Nina hakika taharuki hiyo imeharibu sana sura ya Taifa, heshima tuliyoukuwa nayo kama Taifa na hatujaona kama Serikali inachukua hatua zozote kujaribu kufanya jambo hili lisiendeleo kuharibu *image* yetu kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mheshimiwa Waziri Mkuu atakumbuka kwamba hapo nyuma vimetokea vifo vya kisiasa. Alifariki Mwenyekiti wetu wa Mkoa wa Geita, Bunge na Serikali tulilizungumza hapa na Serikali ikasema inafanya uchunguzi, hadi leo hakuna hatua iliyochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, akapotea msaidizi wangu Ben Saanane, nikakuomba Waziri Mkuu na Serikali yako iruhusu uchunguzi wa kimataifa ili kutatua tatizo hili, ukasema vyombo vyetu vya ndani vina uwezo hadi leo hakuna lililopatikana. Tumeomba vilevile kushambuliwa kwa Mheshimiwa Tundu Lissu kuchunguzwe na vyombo vya uchunguzi vya kimataifa vilivyo huru, visivyofungamana na upande wowote, bado Serikali inaonekana ina kigugumizi katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, unatupa kauli gani sisi kama chama, Wabunge na Taifa? (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nieleze kwamba amani yetu na utulivu ndani ya nchi ni jambo ambalo Watanzania wote lazima tushikamane na tushirikiane katika kulidumisha. Ndilo ambalo linaendelea kutupa heshima duniani kwa sababu Watanzania wote tunashirikiana katika hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yapo matukio yanajitokeza, Mheshimiwa Mbowe umezungumzia upande wa siasa lakini pia matukio haya yapo kwa ujumla wake nchini kwenye maeneo kadhaa kwa ngazi ya familia, lakini pia na maeneo mbalimbali ya mikusanyiko, na watu wengine pia. Wapo wenzetu ambao hawana nia njema nchini wanajitokeza katika kutenda matendo hayo.

Mheshimiwa Spika, na hata hili analisema la Mheshimiwa Tundu Lissu si Mheshimiwa Tundu Lissu pekee ingawa hatupendi mambo kama hayo yatokee, lakini pia tumepoteza Watanzania wengi. Hata mnakumbuka Wilaya za Mkuranga, Kibiti na Rufiji tumepoteza watu wengi. Hata hivyo pia hata siku za karibuni Kamanda wetu wa Jeshi la Ulinzi nchini (JWTZ) naye alipigwa risasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuyazungumze haya kwa ujumla wake na tunapoyazungumza haya kwa ujumla wake, na kwa utamaduni ambao tumeujenga wa nchi hii katika kujilinda wenyewe na kuhakikisha kwamba nchi inaendelea kuwa salama, nataka nikuhakikishie kwamba vyombo vyetu vya dola vinaendelea kufanya uchunguzi wa haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na uchunguzi huu hauwezi kuwa wa leo leo ukapata ufumbuzi kwa sababu wanaotenda matendo haya wanatumia mbinu nyingi za kujificha. Kwa hiyo, na sisi lazima tutumie mbinu zetu za kutambua hao waliotenda matendo hayo katika kila eneo ili pia baadaye tuweze kutoa taarifa ya jumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niendeleo kukuhakikishia pia kwamba vyombo vya dola haviko kimya, vinaendelea. Nataka nikuhakikishie vilevile kwamba vyombo vyetu vya dola vinao uwezo wa kusimamia usalama ndani ya nchi, ni suala la muda ni wakati gani wanakamilisha taratibu na hatua gani zichukuliwe. Sasa hilo linategemea na waliotenda matukio na namna ambavyo wamejificha na namna ambavyo na sisi tunatumia njia mbalimbali za kuweza

kuyapata haya na kuweza kujua na kutoa taarifa kwa Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nikusihi na familia zote ambazo zimepata athari na zimeripoti polisi na wameripoti kwa vyombo vya dola na vinaendelea kufanya kazi kwamba, pale ambapo tutakamilisha uchunguzi tutatoa taarifa kwa ngazi ya familia ambazo pia zimepata athari au ndugu au jamaa kupata athari hiyo na kuwaambia hata hatua ambayo sisi tunaichukua pia. Kwa hiyo, nataka niwasihi kwamba jambo hili tuendelee kujenga imani kwa vyombo vyetu vya dola vitakapokamilisha kazi zake vitatoa taarifa. (Makofi)

SPIKA: Kiongozi wa Upinzani Bungeni, swali la nyongeza.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakubaliana na wewe kwamba maisha ya kila Mtanzania yana thamani kubwa, lakini swali langu lilikuwa *specific*, sikuzungumza suala la Watanzania wote wanaoathirika kwa matukio mbalimbali. Swali langu lilikuwa *very specific* ya jambo linaloitwa *political persecution*, na ningeomba nieleweke hapo.

Mheshimiwa Spika, matukio ya kushambuliwa Mheshimiwa Lissu, lile tukio si la kawaida na naomba tusjaribu kuli-*dilute* kwa kuchanganya na matukio mengine mengi. Nimeuliza swali *specific* ambalo ninaomba *specific answers*. Na uonevu dhidi ya viongozi na wanachama wa vyama vya upinzani nchini umekuwa ni utamaduni wa kawaida. Vyombo vya dola vinafanya, vinatesa watu na vinaumiza watu.

Mheshimiwa Spika, leo ninavyozungumza hivi ni siku ya tatu tangu Mbunge wangu wa Ndanda, Mheshimiwa Cecil Mwambe akamatwe na polisi Mtwara na yuko chini ya *custody* sasa hivi ni zaidi ya saa 48, kisa alikuwa anafanya mkutano wa kampeni ya uchaguzi katika kata mojawapo pale Mtwara Mjini, polisi wakamshika. Huyu ni Mbunge na

Mwenyekiti wa Kanda ya Kusini yenye Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma, yuko ndani siku ya tatu sasa. Sasa matendo haya ya uonevu yanaendelea na hivi tunavyokwenda kwenye uchaguzi wa marudio katika hizi kata chache, viongozi wetu kadhaa wanakamatwa, wanawekwa ndani, wanapigwa na wanateswa.

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu ninachouliza, mimi nilikuomba *specific* utuambie Serikali inaona shida gani? Kwa sababu si mara ya kwanza kwa Serikali hii kuomba msaada wa vyombo vya uchunguzi kutoka nchi za nje. Wakati Benki Kuu ilipoungua *Scotland Yard* walikuja hapa kufanya uchunguzi kuhusu jambo hili, ni mambo ya kawaida katika jamii ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, na kwa sababu vyombo vya dola tumevi-*suspect* kwamba *either* havikuchukua tahadhari ya kulinda viongozi au havikuchukua hatua ya mapema kuzuia uharifu ule aidha kwa kutaka ama kwa kushiriki. Lakini ambacho napenda nikuambie Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi nina imani kabisa vyombo vyetu vya ndani vina uwezo wala sidharau, ila hakuna dhamira ya kuchunguza jambo hili, hapo ndio kwenye tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na kwa sababu hakuna dhamira na kwa sababu wanaoonekana wanaumia ni wa upande mmoja tunaitaka Serikali itoe hiyo *clearance*. Waje watu wafanye *investigation* kama ni ku-*clear* kila mtu anaehusika awe *cleared* ili jambo hili likomeshwe kwa sababu linaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni kwa nini sasa usikubali kwa niaba ya Serikali turuhusu vyombo vya uchunguzi vya kimataifa vije vikamilishe jambo hili ili tukate huu mshipa wa fitina? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo la nyongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbowe, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbowe unaposema jambo hili nilijibu umeliuliza *specific*, naweza kusema kwamba unapotaka *specific* basi inabidi sasa vyombo vya usalama vikamilishe kazi yao ndio vije viseme hasa kwa tukio ambao umetaka lizungumzwe. Hakuna mtu yeyote aliyefurahishwa na tendo alilofanyiwa Mbunge mwenzetu. Hakuna mtu yeyote anayefurahishwa na matukio yanayojitokeza huko iwe ya mauaji au ya mashambulio au migongano inayoendelea kwenye jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vyombo vya dola tumevipa jukumu la kusimamia na kuhakikisha kwamba tunalinda usalama wa raia na mali zao kwa kiwango kinachotakiwa. Na pale ambapo kunatokea tatizo, vyombo vya dola vina majukumu ya kuhakikisha kwamba vinafanya uchunguzi na kuwakamata wale wote ambao wamehusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimeeleza hapa kwamba wakati wote watenda makosa ni watu ambao wanafanya matendo yale wakiwa wameshajiandaa pia kuweza uovu wao na kujificha dhidi ya vyombo vya dola. Wanapojificha sio kwamba vyombo vyetu vya dola havina uwezo wa kufanya kazi yake ya uchunguzi. Mimi nimekwambia haya matukio yote, wanayo matukio megii yamejitokeza katika kipindi kifupi, tumeanza hayo kama nilivyoeleza na huwa ninapozungumza Kibiti, Rufiji na Mkuranga sina maana ya kuficha au kulifanya jambo hili lisitambulike, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunachukua mwenendo wa matukio, tunachukua uwezo wa vyombo vyetu na namna vinavyofanya kazi ili kuhakikisha kwamba tunabaini matukio haya na ndiyo sababu wakati wote Watanzania tumeendelea kuwaambia na kuwahamasisha kwamba ni lazima tushirikiane katika kuilinda nchi yetu na kila mmoja ashiriki katika kutoa taarifa. Sisi tunakaribisha mtu yeyote anayejua kama kuna mwelekeo wa jambo hili atusaidie ili

vyombo vya dola viweze kufanya kazi yake kwa urahisi zaidi.
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, najua unazungumzia kwa upande wako kama Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na yeye Mbunge mwenzetu ambaye ni Mheshimiwa Tundu Lissu anatoka kwenye upande wako, lakini utambue kwamba na sisi pia ni Mbunge mwenzetu na jambo hili ni letu pia, lazima tushirikiane kuhakikisha kwamba jambo hili linapata mwelekeo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nikuhakikishie vyombo vyetu uwezo upo, lakini pale ambapo wataona kama kuna umuhimu huo, vyombo vyenyewe vitafikia hatua vinaweza vikalieleza, lakini mimi siwezi kuhakikishia Taifa kwamba tumekosa uwezo kwa sababu tunaamini vyombo vyetu vinao uwezo wa kufanya uchunguzi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Kiongozi mwenzangu wa Kambi ya Upinzani naomba uamini kabisa kwamba Serikali yetu inayo nia njema, familia za wale wote walioathirika akiwemo Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Tundu Lissu waamini kwamba Serikali yetu inayo nia njema ya kukamata, lakini pia ya kulinda amani ya nchi hii ili kila mmoja, hata sisi pia tuwe na uhakika wa shughuli tunazozifanya za kila siku. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutaendelea kufanya hilo na tutaendelea kuwasiliana nawe kama kiongozi mwenzetu ili uweze kuona haya na namna ambavyo tunaweza tukatatua matatizo haya ya ndani, juu ya matatizo ambayo yanajitokeza kwenye maeneo yetu, ahsante sana.
(Makofi)

SPIKA: Ahsante, tumetumia dakika 14 mpaka sasa, kwa hiyo, kwa mnaofuata ni moja kwa moja swali ili muweze kupata majibu kwa kifupi.

Mheshimiwa Munde Tambwe, karibu, kwa kifupi sana.

MHE. MUNDE A. TAMBWE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuuliza swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu umekuwa mfuatiliaji mzuri wa mazao ya wakulima huko mikoani ili waweze kupata tija. Umekuja Tabora mara kadhaa, umetoa maelekezo kadhaa kuhusu suala zima na kero za tumbaku, lakini agizo kubwa lililolitoa la kuhakikisha tumbaku iliyopo ndani ya wakulima na kwenye magodauni ya msimu uliopita inunuliwe, ambayo mpaka leo hii ninavyoongea tumbaku hiyo bado haijanunuliwa. Hii imesababisha adha kubwa kwa wakulima wa tumbaku wa Mkoa wa Tabora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ni msimu wa kulima tumbaku nyingine lakini tumbaku iliyopo ni ya mwaka wa jana na haijanunuliwa; na tumbaku hii ikikaa kwa muda mrefu inashuka *grade* ambapo ubora wa tumbaku unapungua na inateremka uzito. Mpaka sasa ma-*godown* mengi yanavuja na tumbaku hiyo kuvujiwa na kusababisha hasara kubwa na tahaluki kubwa kwa wakulima wa tumbaku Mkoa wa Tabora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Tabora wana imani kubwa na Serikali ya Awamu ya Tano na leo wanakuomba sana, wanakusihhi wapo chini ya miguu yako wameniagiza; wanaomba utoe tamko.

Je, Serikali inatoa tamko gani leo kuhusu kununua tumbaku ya msimu uliopita ambayo bado haijanunuliwa, iliyopo kwenye magodauni ya wakulima wa Mkoa wa Tabora? (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, maswali yawe mafupi. Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Munde, Mbunge wa Tabora kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la zao la tumbaku ni jambo ambalo Serikali tumelifanyia kazi kweli kweli, na zao la

tumbaku ni miongoni mwa mazao ambayo tunataka sasa yapate mabadiliko ya kilimo chake, lakini pia na masoko yake. Moja kati ya tatizo ambalo lipo sasa ni lile aliloeleza mheshimiwa Mbunge la masoko ya tumbaku na Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote wanaotoka kwenye maeneo ya tumbaku wanajua jitihada za Serikali zilizofanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la tumbaku upo utamaduni wa kila mwaka wa wakulima wetu na makampuni yanayonunua kufunga mikataba ya kiwango cha tumbaku kitakachonunuliwa na makampuni na ndicho kiwango ambacho wakulima wanapaswa kulima.

Mheshimiwa Spika, jambo lililojitokeza mwaka huu ni kwamba wakulima wamelima zaidi ya kiwango kilichowekewa mikataba ya kununuliwa kwenye msimu. Kwa hiyo, tumbaku ambayo imebaki sasa ni ile ya ziada ya msimu ya bajeti ambayo makampuni yanayonunua yalitaka yanunue tumbaku. Ile tumbaku yote ambayo ilikuwa kwenye bajeti ilishanunuliwa, hii ni ile ya ziada.

Mheshimiwa Spika, Serikali ziada hii hatujaiacha kama ambavyo tunaona sasa, ni kwamba makampuni yenyewe tumekaa nayo, tumeyasahi yaweze kununua tumbaku. Wameeleza kwamba walikuwa nje ya bajeti na walikuwa wanaendelea kuzungumza na vyanzo vyao vya fedha ili waje kununua tumbaku yote iliyobaki. Mjadala huo umeendelea na sasa upo mjadala wa bei kwa kuwa sasa imekuwa ni ziada ya mahitaji yao wao wanalazimisha na wanataka wanunue kwa kiwango cha chini, lakini Serikali tunataka wanunue angalau kwa bei dira ya zao lile.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo bado tumeendelea na jitihada za kutafuta nchi mbalimbali zinazoweza kununua tumbaku. Tumeenda Indonesia, China, Misri na Iran na nchi zote hizi zimeonyesha nia ya kuinunua tumbaku iliyopo sasa kwenye maghala yetu. Nchi ya Indonesia imefikia hatua nzuri, wanajadili kiwango cha tumbaku watakachochukua na sasa wanajadili kwenye eneo la bei. Watakapokamilisha mjadala wa kujua kiwango gani watanunua, Serikali sasa itaridhia.

Interest yetu Serikali ni kuona kwamba mwananchi ananufaika kwa kuuza tumbaku yake kwa bei nzuri ili sasa kila mkulima aweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawasihi sasa Waheshimiwa Wabunge wenzangu, lakini pia wakulima wote wa zao la tumbaku, jana nimeona pia kwenye *TBC* tumbaku ipo pale Kaliua, nimemwona Mwenyekiti wa Halmashauri akieleza madhara yanayojitokeza kama ambavyo umeeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka tu nieleze kwamba jitihada za kilimo zitakapokamilika tutawapa taarifa ya hatua nzuri tuliyoifikia na hatua nzuri kwetu ni kutaka kununua tu hiyo tumbaku iliyobaki. Kwa hiyo, tunaendelea na bei tutawapa taarifa. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mwikwabe Mwita Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba nimuulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni sera ya Serikali kulinda raia na mali zao. Lakini mnamo tarehe 24 na tarehe 25, askari wa *FFU* katika Kambi ya Ukonga, Mombasa, walifunga barabara wakapiga akina mama, vijana na wazee na wakawatesa sana abiria na kuleta madhara makubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba nipate tu, na wananchi wangu wasikilize, Serikali inatoa kauli gani juu ya matukio kama haya ambayo yanafanywa na viongozi na vijana ambao kimsingi tunatakiwa tuishi kama ndugu na kushirikiana kwa ajili ya kulinda raia na mali zetu? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa waziri Mkuu majibu ya swali hilo.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Waitara, Mbunge wa Ukonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunazo taarifa kwamba pale Ukonga kulikuwa na mgongano mkubwa kati ya Jeshi letu la Polisi na raia, na mgongano huu umesababisha pia kuuawa kwa askari mmoja na watu wengi kupigwa, lakini hatua nzuri zimechukuliwa. Mkuu wetu wa Wilaya ya Ilala, Mheshimiwa Mjema, aliingilia kati na kuchukua hatua ya kuunda tume ambayo inafanya ufuatiliaji kuona chanzo na madhara yaliyojitokeza na wahusika katika jambo hili. Baada ya tume kumaliza kazi yake, ikibainika nani ametenda kosa hatua kali zitachukuliwa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu wewe ni Mbunge wa eneo lile lazima utashirikishwa pia katika kupata taarifa za matokeo ya tume iliyoundwa na Mkuu wetu wa Wilaya ya Ilala, Mama Sophia Mjema.

SPIKA: Ahsante sana, sasa tunaendelea na maswali, sasa ni upande wa Chama cha CUF, la Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nimuulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika Serikali ya Awamu ya Nne nchi hii ilitumia mabilioni ya fedha kuzunguka nchi nzima kwa ajili ya kukusanya maoni ili kuandaa Katiba Mpya na hii ilikuja baada ya kugundua kwamba Taifa hili linahitaji Katiba Mpya ili kutibu changamoto nyingi ambazo zinaikabili katika maeneo mbalimbali ikiwemo kulinda rasilimali, uwajibikaji, haki za binadamu, tunu za Taifa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa kuanzisha mchakato ule, pamoja na changamoto ambazo zilijitokeza baadaye.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali ya Awamu ya Tano toka imeingia madarakani, leo miaka miwili tayari imepita haijafanya jambo lolote la kuendeleza mchakato ule ili zile ndoto za Watanzania za kupata Katiba Mpya ziweze kutimia. Zaidi tumekuwa tukisikiliza kauli mbalimbali za kwenu viongozi na za viongozi wa Chama chenu cha Mapinduzi ambazo hazioneshi nia ya kukamilisha mchakato huo wa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba awaambie Watanzania leo, nini mpango wa Serikali ya Awamu ya Tano katika kutimiza ndoto za Watanzania kupata Katiba Mpya? *(Makofi)*

SPIKA: Mbona mnapiga makofi, kuna nini? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mtolea, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali ya Awamu ya Nne ilianza mchakato wa Katiba Mpya na kupitia hatua zote za kuunda Tume, ikapita kukusanya maoni na sisi kama Waheshimiwa Wabunge tulikuwa miongoni mwa Wajumbe ambao tulishiriki katika kuweka misingi ya Katiba hiyo. Suala la Katiba Mpya linahitaji gharama kubwa ya fedha na zinatokana na mapato yanayokusanywa ndani ya nchi lakini kila mwaka wa fedha una vipaumbele vyake na sisi tumejikita katika kutoa huduma za jamii kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukishuhudia Watanzania wanahitaji maji kwenye vijiji, kumekuwa na mahitaji ya huduma za afya, tunahitaji kuimarisha elimu, miundombinu, ili kuwawezesha Watanzania kuendelea na maisha yao. Katiba ni mwongozo ambao unaelekeza mambo kadhaa. Sasa hivi tunayo Katiba ambayo pia ina miongozo ile ile ingawa tumekusudia kuibadilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunayo Katiba inaendelea na miongozo ipo, na haya ni mapendekezo ya kufanya marekebisho ya maeneo kadhaa; lakini mchakato wake kwa sababu unahitaji gharama kubwa na kipaumbele cha Serikali ni kutoa huduma ya jamii kwa Watanzania; kwanza tumeanza kuimarisha makusanyo ya ndani ili tuweze kumudu kutoa huduma za wananchi, Watanzania. Pale ambapo tutafikia hatua nzuri ya mapato huku tukiendelea kutoa huduma hiyo na matatizo haya yakipungua kwa kiasi kikubwa, tutakuja kuendesha mchakato huo pale ambapo inaonekana tunaweza tukaufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niendeleo kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua hayo yote lakini pia tumeona muhimu zaidi tuanze na huduma za jamii ili Watanzania waendeleo kufanya kazi zao za kuboresha uchumi wao ili wapate nafasi ya utulivu waje waangalie jambo lingine, kwa sasa tutatumia Katiba iliyopo. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Tunaendelea na Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa na mimi niweze kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingikakwamba Serikali hii ya Awamu ya Tano imefanya mambo mengi sana; tumeona imepunguza matumizi mengi, uchumi unakwenda vizuri, Sekta ya Madini inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, watumishi wa Serikali au watumishi wa Umma wana malalamiko muda mrefu sana, na malalamiko yao makubwa ni juu ya mishahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu ninapenda nikusikie uwaambie Watanzania ni lini Serikali itapandisha mishahara ya watumishi? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu kwa swali hilo muhimu sana tafadhali. *(Makofi)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kigua, Mbunge wa Kilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, na mimi nakiri kwamba wafanyakazi wanahitaji kuboreshewa maslahi yao, eneo hili la mishahara likiwa ni moja kati ya maeneo muhimu. Kama ambavyo tumekuwa tukitoa majibu kwenye maswali ya msingi kupitia vipindi vyetu kwa Mawaziri husika, lakini pia nyakati kadhaa kueleza nia ya Serikali ya kuboresha maslahi ya watumishi. Maslahi ya watumishi ni pamoja na kuweka stahili zao za kila siku, madeni yao, kupanda kwa madaraja na malimbikizo yao pamoja na nyongeza ya mishahara ni miongoni mwa mambo ambayo Serikali imedhamiria kuyafanya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya kuboresha maslahi ya watumishi wakati wa sherehe ya Mei Mosi na aliwaambia wafanyakazi wote. Sasa Serikali kuanzia mwezi wa sita tunaendelea kuhakikisha kwamba tunakamilisha taratibu za kimsingi ambazo zitaiwezesha sasa Serikali kuanza kutoa malipo kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, lakini eneo la kwanza ni lile la madeni, eneo la pili kwa muda mrefu tulisitisha madaraja ambalo sasa tumeanza kuwapandisha madaraja watumishi ambao hawakupanda madaraja kwa muda mrefu tunawafikisha mahali pao, na tunapobadilisha madaraja haya inabidi tulipe malimbikizo yake. Pia kuna ambao walishapanda, walikuwa hawajalipwa malimbikizo, sasa tunaanza uratibu. Na hapa juzi tumetenga shilingi bilioni 147 kwa ajili ya kulipa na Mheshimiwa Rais alishaeleza nia ya kulipa maslahi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukishakamilisha haya, ni pamoja na yale mambo ambayo tulianza nayo, uhakiki wa watumishi, vyeti *fake*, ili kuondoa watumishi tusije tukawalipa

watu ambao sasa hawastahili. Eneo hilo tumelimaliza, madeni tumeendelea kuhakiki, na kwa sababu madeni yanaendelea kila siku nayo tunaendelea kuyahakiki lakini yale ya muda mrefu tayari, na tumeanza kulipa. Na madeni haya yanalipwa kupitia mishahara yao. Tusingependa tuwe tunatangaza leo tumelipa, hii inaweza ikaleta athari kwenye eneo la mabadiliko ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali inalipa ingawa inalipa kwa awamu, lakini tutahakikisha kwamba madeni yote ya watumishi tunamaliza, waliokosa kupanda madaraja kwa muda mrefu tunawapandisha na kulipa stahili yao mpya halafu sasa tuje tuongeze mishahara. Tutakuwa tayari Serikali tunajua tuna watumishi wangapi, tutahitaji fedha kiasi gani za kulipa nyongeza ya mishahara, na wakati huo itakapokuwa imekamilika, nataka niwahakikishie watumishi tutaendelea na uboreshaji likiwemo na eneo la uongezaji wa mishahara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nawasahi sana wafanyakazi wenzetu kote wawe na imani na Serikali yao na huku tukiendelea kuratibu vizuri. Tunachotaka sisi tusije tukapoteza fedha tukawalipa watu ambao hawastahili, lakini pia lazima tujiridhishe ni kiwango gani cha fedha kinahitajika kulipa kwenye eneo hili ili kila mtumishi apate stahili yake na kila mtumishi tunapoboresha mishahara apate kima ambacho angalau kinaweza kukidhi mwenendo wa maisha ya kila siku na huo ndiyo utaratibu ambao Serikali imejiwekea. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Swali la mwisho kwa siku ya leo, Mheshimiwa Pauline Philip Gekul.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali imekuwa ikitoa kauli na matamko mbalimbali kwa wakulima wa mbaazi kote nchini kwamba Serikali inafanya

mazungumzo na Serikali ya India ili wakulima hawa wapatiwe soko. Hata hivyo hadi sasa mazungumzo hayo hayajakamilika na wakulima wamebaki na mazao yao.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nifahamu, kwa nini Serikali isione ni busara kuwatangazia wakulima wa mbaazi kote nchini kwamba wameshindwa kuwapatia soko na wasiende kulima katika msimu huu wa kilimo ambao unakwenda kuanza sasa? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gekul, Mbunge wa Babati Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hata juzi wakati tunapeana maelekezo ya msingi jambo hili la matatizo ya masoko ya mazao yetu lilijitokeza, mbaazi ikiwemo. Ninachoweza kusema hatuwezi kuwaambia wakulima msimu huu wasijiandae kulima kwa sababu suala la masoko, awali zao la mbaazi tulikuwa na soko la uhakika la nchi ya India na ndio wanunuzi wakuu wa zao hili. Huku kwetu sisi mikoa yote inayolima imeendelea kulima kila mwaka na tumeendelea kufanya biashara na nchi ya India bila tatizo lolote lile.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hata hivi karibuni Waziri Mkuu wa India alipokuja nchini, aliweza kusesitiza pia tulime mbaazi nyingi na wao pia wanalima na sisi tumelima. Sasa tulipofikia hatua ya kuuza kwa bahati mbaya au nzuri kwao nchi ya India imeweza kuzalisha mbaazi kwa asilimia 30 zaidi na kwa maana hiyo wana mbaazi ziada na kwa hiyo, walisitisha utaratibu wa kununua mbaazi kutoka nchi za nje kuingiza kwao mpaka hapo akiba yao watakapoifikiria vinginevyo. Kwa kufanya hilo wametuatiri kwa sababu soko pekee la mbaazi kwetu sisi ilikuwa ni nchi ya India.

Mheshimiwa Spika, sasa nini jukumu la Serikali kwa sasa; tunaendelea kutafuta masoko na ndiyo sababu

tumewasihi wakulima wa mbaazi nchini kote, na ni mikoa mingi inayolima sana mbaazi, tumeendelea kuwasihii kwamba waendeleo kutusubiri kwa sababu Bodi ya Mazao Mchanganyiko ambayo inashughulikia mbaazi pia sasa inaendelea kutafuta masoko, likiwemo na lile zao la tumbaku ambalo nimelieleza muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jitihada hizi zitakapofikia hatua nzuri, tutauza. Kwa sasa hatuwezi kuwaambia kwamba tutauza kwa sababu bado *negotiations* zinaendelea na mataifa ambayo yatataka kununua zao hili la mbaazi ikiwemo na India yenyewe kwa sababu ya ile *commitment* ambayo ilikuwa imeshatolewa kati yetu na wao; na ndiyo utaratibu wa kawaida kwa nchi ambazo tunafanya nao biashara za mazao. Pale ambapo kunatokea tatizo lazima na sisi tupate taarifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hii ni taarifa kwa wakulima wote wa mbaazi kwamba kwa sasa wawe watulivu, tunaendelea na utaratibu huu wakati wowote tutawapa taarifa. Ni kweli tunajua wanaathirika sana lakini ni muhimu pia taarifa hii kuwa nayo na uvumilivu ni muhimu pia kuwa nao.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Huo ndiyo mwisho wa kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Tunakushukuru sana kwa kuwajibu Waheshimiwa Wabunge kwa ufasaha mkubwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana. Mtaona katika nusu saa hii CUF wamepata swali moja, CCM wamepata maswali mawili na Chadema wamepata maswali matatu. Kwa hiyo *in average* Upinzani wamepata manne, CCM mawili. Kesho kutwa kwenye magazeti, aah, uongozi wa Bunge. *(Kicheko/Makofi)*

Tunaendelea na maswali yetu. Ofisi ya Rais, TAMISEMI, swali tutakaloanza nalo leo ni la Mheshimiwa Ruth Hiyob Mollel. Mheshimiwa Ruth Mollel, tafadhali.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 30

Kuimarisha Serikali za Mitaa

MHE. RUTH H. MOLLEL aliuliza:-

Maboresho ya utendaji wa Serikali za Mitaa yalilenga kuimarisha na kujenga uwezo wa Serikali za Mitaa kujiendesha kwa kuwapatia rasilimali watu na fedha za kutosha kutekeleza Sera ya Ugatuuji wa Madaraka.

Je, Serikali ina lengo gani kuimarisha Serikali za Mitaa ziweze kujiendesha?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Hiyob Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara za 145 na 146 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mamlaka za Serikali za Mitaa ni mamlaka shirikishi za kisheria na kidemokrasia zilizoanzishwa kwa kwa lengo la kuwashirikisha wananchi katika shughuli zote za maendeleo, huduma za jamii, utawala bora, utekelezaji wa sheria, ulinzi na usalama kwa kuzingatia kanuni za uwazi na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 1999 Serikali imetekeleza programu mbalimbali za kuboresha utendaji katika ngazi ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Miongoni mwa programu hizo ni Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa iliyolenga kuimarisha miundo na mifumo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ili zijiendeshe na kuwahudumia wananchi kwa ufanisi. Aidha, Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha imeimarisha na kuinua uwezo wa Halmashauri katika kukusanya mapato na kudhibiti matumizi.

Mheshimiwa Spika, katika kuziimarisha zaidi Mamlaka za Serikali za Mitaa, bajeti ya ruzuku ya maendeleo kwa Halmashauri imeongezeka kutoka shilingi bilioni 49 mwaka 2008 hadi shilingi bilioni 249 mwaka 2017. Aidha, kuanzia mwaka 2015, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeruhusiwa kwa mujibu wa sheria kuajiri watumishi wake wa kada 22 za ngazi za chini ikiwemo Watendaji wa Vijiji baada ya kupata kibali cha kuajiri. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Ruth Mollel swali la nyongeza.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, ili hawa watumishi wa Serikali za Mitaa waweze kutoa huduma kwa ufanisi wanahitaji kupata mafunzo ya mara kwa mara ili kuboresha utendaji wao. Kwa kuwa kwa muda mrefu mafunzo yamesimamishwa, tunategemeaje hawa watumishi waweze kutoa huduma ipasavyo? Hilo swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, viongozi ambao wako karibu sana wananchi ni Watendaji wa Kata na Mitaa pamoja na Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Kata, ndio wapo karibu sana na wananchi na ndio ambao wanatoa huduma karibu kabisa na wananchi. Watendaji wanapata mshahara lakini Wenyeviti hawapati chochote. Je, Serikali ina mpango gani kwa ajili ya kuwamotisha Wenyeviti ili waweze kutoa huduma vizuri kwa wananchi? *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Joseph George Kakunda, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Spika, katika maeneo ambayo yamejengewa uwezo kwa hali ya juu kabisa ni hili eneo la Serikali za Mitaa. Kuna programu nyingi sana za kisekta zimeendelea kutoa mafunzo

mbalimbali kwa nyakatii mbalimbali. Kuna Programu kwa mfano ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo, Programu ya Kuendeleza Sekta ya Maji, zote hizi zimekuwa na mafunzo mbalimbali kwa watendaji wa Serikali za mitaa kwa ajili ya kuimarisha uwezo wao, hasa hasa zile kada za fedha, ununuzi na wahandisi. Serikali inatoa *commitment* ya kuendelea kutoa mafunzo mara fedha zinapopatikana.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu posho za Wenyevitwa wa Serikali za Vijiji na Vitongoji. Mwongozo uliopo ni kwamba kila Halmashauri inatakiwa iboreshe makusanyo yake ya ndani, iongeze makusanyo yake ya ndani na mwongozo uliopo ni kwamba asilimia 20 ya mapato yake ya ndani yanatakiwa yatumike kwa ajili ya posho na agizo ambalo limetolewa na kusisitizwa na Serikali ni kwamba wale ambao wanachelewesha kulipa posho za wenyevitwa wa vijiji na vitongoji sasa itabidi wachukuliwe hatua.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, swali fupi la nyongeza. Leo Mheshimiwa Lubeleje amepiga tai. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lengo la Serikali kuchukua vyanzo vingi vya Halmashauri za Wilaya ilikuwa ni kusaidia ruzuku ya kutosha kwenye Halmashauri hizi. Lakini kwa kuwa ruzuku inayotolewa haitoshelezi kabisa kwa Halmashauri hizi kujijendesha.

Sasa swali langu, naishauri Serikali kwamba je, Serikali inaweza kurudisha baadhi ya vyanzo vya mapato kwa Halmashauri ili nazo ziweze kujijendesha badala ya kusubiri ruzuku na ruzuku yenyewe inachelewa sana?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Saidi Jafo, tafadhali majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu wangu katika swali la msingi nilipenda kujibu swali la Mheshimiwa Lubeleje ambapo mimi ninamuita greda la zamani makali ya yale yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna vyanzo mbalimbali vilichuliwa na Serikali Kuu. Hata hivyo, kwa mamlaka tuliyopewa tutafanya namna ili kuhakikisha kwamba mapato, hata hayo ya vyanzo vilivyobaki yaweze kukusanywa vizuri.

Mheshimiwa Spika, ilikuwa kwamba hata miongoni mwa vyanzo tulivyokuwa navyo ukusanyaji ulikuwa na changamoto kubwa na ndiyo maana katika program zetu hivi sasa tunafanya namna ili tuweze kutumia mifomu ya *electronic* kwa ajili ya uongezaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishieni kwamba sasa hivi Wizara ya Fedha imefanya *commitment* kwamba fedha zote zilizokusanywa zipelekwe na ndiyo maana mpaka leo hii ninavyozungumza katika *quarter* ya kwanza zaidi ya shilingi trilioni moja imechukuliwa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika *OC* na miradi ya maendeleo.

Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba kutokana *commitment* ya Serikali katika ukusanyaji wa mapato jambo hili litakwenda vizuri; na hatimaye Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaweza kutimiza wajibu wake kama inavyokusudiwa.

SPIKA: Ahsante sana, tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano swali la Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau Mbunge wa Mafia.

Na. 31

Jengo la Abiria na Taa za Kuruka Ndege

MHE. MBARAKA K. DAU aliuliza:-

Serikali imekamilisha ujenzi wa barabara ya kuruka ndege katika Uwanja wa Ndege Mafia kwa awamu ya kwanza kwa ufadhili wa Mfuko wa *Millenium Challenge Account (MCA)*.

Je, ni lini Serikali itajenga jengo la abiria na kuweka taa za kurukia kwenye uwanja huo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mbunge wa Mafia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Mafia uliofadhiliwa na Shirika la Changamoto za Milenia la Serikali ya Marekani na kutekelezwa kupitia Mfuko wa Changamoto za Milenia Tanzania (*Millennium Challenge Account - Tanzania*) ulikamilika mwaka 2013. Mradi huo haukuhusisha ujenzi wa jengo jipya la abiria, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho mapya ya magari, maegesho mapya ya ndege (*apron*), barabara za viungio (*taxiways*) pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongeza ndege wakati wa kutua.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizosalia ambazo usanifu wa kina ulifanyika katika mradi wa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina uliohusisha viwanja saba kwa fedha za Benki ya Dunia na kukamilika mwaka 2009 hazijaanza kutekelezwa. Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali, zikiwemo fedha za ndani na washirika wa maendeleo, kwa ajili ya kukamilisha kazi zilizosalia.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inatambua umuhimu wa Kiwanja cha Ndege cha Mafia kwa Wilaya ya Mafia kwa kuwa kutokana na jioografia yake kisiwa hiki kinategemea zaidi kiwanja hiki katika kuchochea shughuli za uchumi zikiwemo utalii. Hivyo, Serikali itaendelea kutafuta fedha ili kuweza kukamilisha ujenzi wa kiwanja hiki.

SPIKA: Swali la nyongeza Mheshimiwa Mbunge wa Mafia.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri anakiri hapa kwamba kutokana na jioografia yake kisiwa cha Mafia, kiwanja cha ndege ni muhimu sana katika kukuza uchumi. Lakini mimi nataka nimuongeze, kuna ziada pia masuala ya jamii. Hivi ukiwa Mafia ikifika saa kumi na mbili na ukapata dharura ya ugonjwa huna namna ya kutoka kwenda katika Hospitali ya Rufaa kwa sababu kiwanja hakina taa.

Sasa kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri anakiri kwamba usanifu na upembuzi ulishafanyika toka mwaka 2009 na leo ni miaka minane kwa hesabu za haraka bado unakuja kutuambia kwamba pesa hazija patikana?

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini hizi pesa zitapatikana ili ujenzi wa kuweka taa katika uwanja wa Mafia na jengo la abiria ufanyike?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, barabara ya kurukia na kutua yani *runway* ya kiwanja cha Mafia ina mita kama 800 hivi, hivyo ndege kubwa haziwezi kutua na unasema kuna fursa za kitalii pale.

Je, ni lini sasa Serikali itaongeza urefu wa uwanja ule kwenda mpaka kilometa mbili ili kuruhusu ndege kubwa zitue

moja kwa moja kutoka Ulaya na kuleta watalii Mafia? Nakushukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo kwa kifupi Naibu Waziri, Mheshimiwa Kwandikwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, ninapenda nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dau mjukuu wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada anazozifanya ili kuhakikisha kwamba kisiwa cha Mafia kinachangia pia katika ukuaji wa uchumi Taifa, kwa maana ya kuleta maendeleo katika kisiwa cha Mafia.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba upembuzi yakinifu na kazi ya ukarabati wa uwanja baada ya usanifu ilishaanza, kwa sababu kazi iliyofanyika ya kupanua kiwanja na kukarabati ilikuwa ni awamu ya kwanza. Kwa hiyo, kuna awamu ya pili ambayo itafanyika kwa ajili ya kuhakikisha kwamba uwanja huu sasa unafanana na kwamba unatoa pia huduma. Kwa sababu Serikali tunapanua viwanja vikubwa kwa mfano Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam, Uwanja wa Ndege wa KIA, kwa maana hiyo na viwanja vingine vya Mikoani tunavyovifanyia upanuzi sasa vitakuwa na tija kwa kutoa huduma katika viwanja hivi vikubwa.

Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali kufanya upanuzi, na mimi nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Mafia kwamba kwenye awamu ya pili tutazingatia ushauri wake kwamba tuone namna ya kuvipanua vile viungio ili huduma ziweze kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi, mimi nitahakikisha kwamba kwenye bajeti zinazokuja awamu hii ya pili tutaiwekea fedha ili huu uwanja wa Mafia uweze kufanana na hali ilivyo na kwamba tuweze

kukuza utalii, lakini pia uweze pia kuweza ku-*feed* viwanja vikubwa ambavyo tunavipanua.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Dau mjukuu wangu usiwe na wasiwasi tutakuja Mafia na mimi nitahakikisha kwamba jambo linakwenda vizuri. Ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 32

Ndege za Serikali Aina ya Fokker 50 na Fokker 28

MHE. KAPT. ABBAS ALI MWINYI aliuliza:-

Ndege za Serikali aina ya Fokker 50 iliyoletwa nchini mwaka 1992 na Fokker 28 iliyoletwa nchini mwaka 1978 ni chakavu na teknolojia zake zimepitwa na wakati. Aidha, Kampuni iliyotengeneza aina hizo za ndege imeshafungwa hivyo upatikanaji wa vipuri vya ndege hizo kuwa mgumu na gharama kuwa kubwa.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzibadilisha ndege hizo na kuleta mpya?

(b) Je, ni lini Serikali itarekebisha hali ya *hanger* la kuegeshea ndege za Serikali?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimwa Kepteni Abbas Ali Mwinyi, Mbunge wa Fuoni lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli ndege aina ya Fokker 28 na Fokker 50 zina umri mkubwa. Hata hivyo kiutaalamu usalama wa ndege huwa haupimwi kwa miaka iliyonayo bali hupimwa kwa masaa iliyoruka. Hivyo, kwa hali ya kawaida muda wa masaa ya ndege kuwa chakavu (*beyond economic benefit*) ni masaa 90,000 na kati ya ndege hizi mbili

hakuna hata ndege moja yenye masaa zaidi ya 15,000. Aidha, ndege hizo zimekuwa zikifanyiwa matengenezo kwa kuzingatia ratiba.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa ndege ya Fokker 50 ipo kwenye ubora wa kutumika na inaendelea kuhudumia viongozi wetu. Ndege ambayo haitumiki ni Fokker 28 kwa sababu ina matatizo ya breki na *engine* ya kulla. Serikali imewasiliana na mtengenezaji ili kuweza kutatua matatizo hayo. Ndege hizi mbili bado zina teknolojia ya kisasa na zimekuwa zikipelekwa kwenye matengenezo ya lazima kwa mujibu wa matakwa ya Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO) na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA). Kimsingi vipuli vya ndege hizo bado vinapatikana.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya kutengeneza ndege hizi haijafungwa bali wamesimamisha utengenezaji wa ndege mpya na wanaendelea kutoa huduma ya matengenezo (*maintenance support*) kwa zile ndege ambazo zimekwishawahi kutengenezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, Serikali inatambua changamoto za karakana ya kutengeneza ndege za (TGFA) kutokana na uchakavu. Tayari nimeshawaagiza Wakala wa ndege za Serikali TGFA kufanya tathimini ya gharama halisi zitazotumika kwa ajili ya kukarabati Karakana hiyo. Gharama halisi zitakapopatikana, Serikali itafanyia kazi marekeboshu ya *hanger* hilo. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Abbas swali la nyongeza kama lipo.

MHE. KEPT. ABBAS ALI MWINYI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa makampuni yanayotengeneza aina hizo za ndege yamesitisha utengenezaji, sasa je, Serikali haioni itakumbwa na changamoto za upatikanaji wa vipuri? Hilo ni swali la kwanza.

Swali la pili, je, lini hasa uboreshaji wa karakana hiyo utanza? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Nditiye, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Abbas Ali Mwinyi kwa uzalendo wake mkubwa sana wa kuhakikisha kwamba viongozi wetu wa kitaifa wanasafiri katika hali ya usalama mkubwa. Vilevile nikusifu kwa kutumia utaalamu wako mzuri kama rubani mzoefu wa kuhakikisha kwamba ndege zetu zinakuwa salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Abbas kwa kuwa ni kweli kwamba Serikali inafahamu hilo; lakini nimhakikishie kwamba vipuri hivyo bado vinatengenezwa na kampuni hiyo hiyo ya Uholanzi ambayo ndiyo mtengenezaji mkubwa wa ndege za Fokker ambako vipuri hivyo vinapatikana kwenye *unit* yao iliyopo nchini Malyasia.

Mheshimiwa Spika, vilevile huko nchini Malyasia ambako ndiko vipuri vinapotengenezwa kuna *unit* yao ya mafunzo (*training center*) ambako wanafanya *re-validation* ya *licence* na kwa ndege hizo marubani wetu wote huwa wanakwenda kule kwa ajili ya ku-*review* leseni zao. Nimhakikishie Mheshimiwa Abbas kwamba vipuri vipo vinapatikana kwenye *unit* yao hiyo na tutaendelea kuvitumia na tunaendelea kuwasiliana kwa ajili ya matengenezo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili ni kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi. Mara *TGFA* watakapotuletea makadirio basi Serikali itatenga pesa kwa ajili ya matengenezo ya hanga hilo la ndege, ahsante sana.

SPIKA: Swali dogo la nyongeza, Mheshimiwa Mbunge wa Mbeya.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Bado niko kwenye *aircraft*, kwenye tiketi za *ATCL* kuna picha ya ndege aina ya Embraer ambayo inabeba abiria 105 ambayo kimsingi bado haipo nchini, lakini kwenye tiketi za *ATCL* wameweka picha ambayo inaonekana kama ndege ipo na ukinunua ile tiketi unaweza ukafikiri kwamba unaenda kupanda *aircraft* hiyo ya abiria 105 lakini ukienda kule unakuta na *bombardier* ya abiria 70.

Sasa kwa nini Serikali inafanya udanganyifu? Haihofii kwamba iko siku atatoka mtu mwenye upeo wake akaenda pale akakuta anapandishwa ndege ambayo haipo picha kwenye tiketi alafu aka-*sue* ndege ikakamatwa? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. *Engineer* Atashasta Nditiye.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwenye tiketi alizozitungumza hiyo picha bado ipo, lakini yale ni matoleo ya tu ya kawaida ambayo kikawaida kibiashara hayawezi kuathiri kabisa shughuli za utaratibu wa biashara ya usafishaji wa abiria kwa njia ya ndege. Hata hivyo, tutaliangalia na kuangalia namna ya kuweza kulirekebisha katika muda mfupi ujao. (*Makofi*)

Na. 33

Usalama wa Fedha za Wanachama- *NHIF*

MHE. RASHID ALI ABDALLAH aliuliza:-

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (*NHIF*) mara nyingi hutumika kwa kutoa mikopo kwa Serikali kwa ajili ya maendeleo ya jamii.

Je, ni utaratibu gani wa kisheria unaofanyika ili kuhakikisha fedha za wanachama zinalindwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K. n. y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ni mpango wa kisheria wa kuchangia huduma za matibabu ulioanzaishwa kutekeleza sera ya uchangiajia wa huduma za afya ya mwaka 1993 kupitia utaratibu wa wananchi kuchangia gharama za matibabu kabla ya kuugua.

Mheshimiwa Spika, ili kuufanya mfuko huu uwe endelevu, Mfuko huwekeza fedha za ziada katika vitenga uchumi mbalimbali vya muda mfupi na mrefu vyenye lengo la kuboresha utoaji wa huduma za afya kwa ujumla wake. Uwekezaji huu pia unajumuisha mikopo kwa Serikali kwa ajili ya maendeleo ya jamii. Uwekezaji unaofanywa na *NHIF* ni jukumu mojawapo la kisheria linalotekelezwa chini ya Sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya ya mwaka 1999 ambao pia unasimamiwa na Sera ya Mfuko wa Bima ya Afya ya Uwekezaji pamoja na miongozo ya uwekezaji kama ilivyotolewa na Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii ikishirikiana na Benki Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kazi mojawapo ya msingi ya mamlaka ya usimamizi wa sekta ya hifadhi ya jamii ikishirikiana na Benki Kuu ya Tanzania ni kutetea na kulinda maslahi ya wanachama kwa kuhakikisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inaelekeza uwekezaji wake katika vyanzo vya uwekezaji vilivyo salama na vyenye tija kwa wanachama na taifa kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa kupitia utaratibu huu nilioueleza, fedha za *NHIF* zipo salama. Aidha, kwa mujibu wa tathimini ya nne uhai wa Mfuko (*actuarial valuation*) iliyofanywa

mwaka 2013 imeonesha uwezo wa mfuko kifedha na uendelevu wake ni hadi kufikia mwaka 2040.

SPIKA: Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah swali la nyongeza

MHE. RASHID ALI ABDDALLAH: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Chuo Kikuu cha Dodoma kilijengwa kwa mkopo wa shilingi bilioni 44.29 kutoka katika Mfuko *NHIF* bila ya kuwa na mkataba na bila ya uthinbitisho wa udhamini kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, swali langu, je, Serikali haioni kwamba imeshindwa kutekeleza jukumu lake kisheria?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kama Serikali imeshindwa kutekeleza jukumu lake kisheria haioni kwamba inasababisha upotevu mkubwa wa fedha za wanachama kama angetokea mkopaji yule si mwaminifu?

SIPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa, ahsante Kituo chako kimejengwa Jimboni kwako, ulifanya mpango nini Mheshimiwa Mbunge! Majibu tafadhali Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA: Mheshimiwa Spika, nikianza na swali la kwanza, kama nilivyoeleza pale awali katika majibu yangu ya msingi katika taratibu zote hizi za uwekezaji zinasimamiwa kwa miongozo ambayo ipo chini ya *SSRA* na *BOT*. Kwa sababu sekta ya hifadhi ya jamii inasimamiwa na *SSRA*, na upo utaratibu amabo *SSRA* umekuwa ukiufanya kuhakikisha kwamba yale madeni yote ambayo mifuko inaidai Serikali utaratibu umewekwa wa namna ya kuweza kuyalipa ili mifuko hii iendelee kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana katika majibu yangu ya awali nimesema kwamba *actuarial evaluation* ambayo inajumuisha pamoja na madeni yote, inaonesha kwamba mfuko huu bado unauwezo kuwa endelevu mpaka kufikia mwaka 2040.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la upotevu wa fedha za wanachama maelezo yangu ni yaleyale kama nilivyosema pale awali; kwamba katika utaratibu wa miongozo ambayo imetolewa na *SSRA* na *BOT* imetoa namna gani mifuko ifanye uwekezaji na baada ya tathimini kufanyika imeonesha kabisa kwamba mifuko hii bado endelevu. Nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hakuna upotevu wa fedha za wanachama, mfuko huu bado ni utakuwa endelevu sana.

Mheshimiwa Spika, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba kilichofanyika pale juu Dodoma ni uwekezaji mkubwa ambao una tija kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania. Kwa hiyo, hakuna upotevu wowote na Serikali katika hakuna jambo lolote kuonyesha upotevu. *(Makofi)*

SPIKA: Tuaendelea na Wizara ya Kilimo kwa sababu ya muda Waheshimiwa, atauliza swali Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo.

Na. 34

Ujenzi Wa Chuo Cha Kilimo na Mifugo Kata ya Lufilyo

MHE. FREDY A. MWAKIBETE aliuliza:-

Tunatambua juhudi za Serikali za kujenga Chuo cha Kilimo na Mifugo katika Kata ya Lufilyo.

Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa bwalo la nyumba za walimu ili chuo hicho kianze kutoa huduma kwa wananchi, hasa ikizingatiwa kuwa majengo ya madarasa yalishakamilika?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mbunge wa Jimbo la Busokelo kama ifuatavyo:-

Wizara ya Kilimo ina jukumu la kusimamia na kuviendeleza vyuo vya kilimo hapa nchini. Hiki ni kituo kidogo cha kutoa mafunzo ya kilimo kwenye *scheme* za umwagiliaji kwa maana ya *World Agriculture Resource Center*. Kituo hiki kilijengwa kwa jitihada kwa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Rungwe Mashariki Profesa Mark Mwandosya ambapo mwisho alikabidhi kituo hicho kwa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ili wakamilishe sehemu iliyobaki.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua uwepo wa kituo hicho na inaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo ili kupata fedha za kukamilisha ujenzi wa majengo hayo kwa ajili ya kutumika kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, vyuo vya kilimo vinavyosimamiwa na Wizara ya kilimo vipo 14. Vyote hivi vimejengwa muda mrefu na hivi sasa vinakabiliwa na changamoto nyingi sana ikiwa ni pamoja na uchakavu wa miundombinu ikiwemo ofisi za walimu, madarasa, mabweni, maabara, nyumba za walimu, maktaba pamoja na karakana. Changamoto nyingine ni uhaba wa wakufunzi na watumishi wa kada nyingine pamoja na vifa vya kufundishia.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo Wizara imeweka kipaumbele cha kuboresha vyuo vilivyopo badala ya kufikiria kuongeza vyuo vingine. Vyuo hivyo vikikarabatiwa vitaweza kuchukua wanafunzi wengi hivyo kuwezesha Serikali kufikia lengo la kuwa na mtaalam mmoja wa kilimo katika kila kijiji na pia kuzalisha maafisa ugani wenye uwezo wa kutoa huduma bora kwa wakulima. Aidha, katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 Serikali imeshatenga shilingi 773,208,000 kwa kuanzia kwa ajili ya kufanya ukarabati katika Vyuo vya *MATI*.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Busokelo, swali la nyongeza nimekuona.

MHE. FREDY A. MWAKIBETE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa furda hii niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Mary Mwanjelwa Dada yangu niipongeze Serikali katika majibu haya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika jibu lake la msingi amekiri kwamba Serikali ina vituo ama vyyo 14 kwa ajili ya kilimo hapa nchini, lakini chuo/kituo hiki kilianza kujengwa tangu 2009 na kilikabidhiwa kwa halmashauri na halmashauri imeshindwa kukiendeleza. Je, hauoni kuna umuhimu sasa kupitia Wizara yako muweze kuchukua jukumu hili ili chuo hiki kiweze kukamilika maana ni zaidi ya miaka nane hadi sasa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, pamoja na kwamba kuna vyyo hivyo 14, tumekuwa tukitoa wataalam na watafiti mbalimbali na wanakuwa wanazalisha kwa tija; lakini changamoto kubwa iliyopo ni kwamba anapokwenda kufanya kazi ama kwenye *field* changamoto kubwa ni kwamba masoko ya mazao wanayozalisha yanakuwa hayapo. Wizara imejipangaje, ni *mechanism* gani itatumika kutafutia masoko kwa bidhaa mbalimbali zinazozalishwa nchini hasa hasa katika kilimo ukizingatia kwamba mahindi sasa hivi yameshuka bei, viazi mviringo vimeshuka bei, choroko zimeshuka bei na mazao mbalimbali? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Mary Mwanjelwa.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, katika swali lake la (a) amezungumzia kwamba kituo hiki kimechukua miaka nane; na mimi ni kweli ninakiri kwamba kituo hiki kimechukua miaka nane. Hata hivyo kwenye majibu

yangu ya msingi nilishaeleza kwamba kituo hiki kilikabidhiwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara; na kwa sababu masomo yanayofundishwa pale yanahusiana na kilimo; ningependa niwasiliane na Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kuangalia ni taratibu gani ambazo zinatakiwa kufuatwa, na ikiwezekana kwenye bajeti ya msimu wa fedha ujao basi tuweze kukiingiza. Vilevile niko radhi kwenda kutembelea kituo hiki ili niweze kujithibitishia kitu amcaho kiko mahali pale.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la (b) Mheshimiwa Mbunge amzungumzia kwamba kuna wataalam wengi ambao wanasoma katika vyo vyetu hivi vya mafunzo. Ni kweli na mimi naomba niendelee kusisitiza na kwamba sisi kama Wizara tunasisitiza sana kuwa na uzalishaji wa tija. Kwa hiyo nini kifanyike sasa? Ni kwamba tunaendelea kuwahamasisha wakulima wote kujunga katika vikundi vya SACCOS kwa sabbau wataendelea kupata mikopo ambayo itakuwa na riba nafuu na vile vile waweze kujijiri wenyewe binafsi. Ahsante

Na. 35

Kuanza kwa Mfumo wa *Commodity Exchange*

MHE. JEROME D. BWANAUSI aliuliza:-

Serikali iliahidi kuanzisha mfumo wa *commodity exchange* ili kuwasaidia wananchi wanaolima korosho kupata bei nzuri katika msimu husika

(a) Je, Serikali ina kauli gani huu ya kuanza kwa mfumo huo?

(b) Je, Serikali itatatua vipi suala la kodi nyingi kwa wakulima wa korosho inayosababisha kupata bei ndogo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya soko la bidhaa (*commodity exchange*) yalianza mwaka 2011 kwa lengo la kufanya biashara ya mazao kuwa ya wazi na yenye ushindani kulingana na nguvu ya soko. Aidha, mfumo huu umelenga kupunguza gharama za uendeshaji wa masoko yote ya mazao yote ya chakula na biashara ili kuwawezesha wakulima kupata bei nzuri na yenye tija.

Mheshimiwa Spika, hatua ambazo zimeshachukuliwa hadi sasa ni pamoja na kupitishwa kwa waraka wa soko hilo, kuundwa kwa bodi ya soko, kutungwa kwa sheria ya mwaka 2015 ya soko la bidhaa pamoja na kanuni zake, kufanya uzinduzi wa kuanzisha soko hili, kutoa mafunzo kwa madalali watakaoendesha soko hilo na kutoa mafunzo kwa baadhi ya viongozi wa Serikali na sekta binafsi ili kujenga uelewa wa pamoja. Vilevile ofisi na jukwaa la soko hilo vimefunguliwa kwenye jengo la *LAPF* lililo kijito nyama Jijini Dar es Salaam. Kazi za uwekaji wa vifaa katika ofisi na jukwaa zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, elimu ya soko la bidhaa inaendelea kutolewa kwa baadhi ya viongozi wa ngazi za Mkoa na Wilaya na maafisa kilimo, ushirika, biashara na maendeleo ya jamii katika Mikoa ya Lindi, Mtwara, Morogoro, Dodoma na Singida. Aidha, elimu hiyo imeshatolewa kwa viongozi wa vyama vikuu vya ushirika na viongozi wa vya msingi na vyama visivyokuwa vya kiserikali ili kujenga uelewa wa somo hili. Pia elimu itaendelea kutolewa kwa wakulima na wananchi wka ujumla ili wadau waufahamu mfumo huo wa soko.

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imeondoa ushuru na tozo an kubakiza makato ya usafirishajia korosho kulingana na umbali halisi. Mchango wa kuendeleza zao na ushirika na kuondoa shilingi 50 kwa kila kilo zilizokuwa

zinatozwa kwa ajili ya kufungashia korosho. Aidha, Serikali imepunguza ushuru wa Halmashauri za wilaya kutoka asilimia tano hadi tatu.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Bwanausi swali la nyongeza.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu kwa kujibu maswali kwa ufasaha sana na natambua kazi nzuri inayofanywa na Waziri wa Kilimo akimsaidia katika kuhakikisha kwamba tunaboresha soko la korosho, nataka niulize maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, msimu wa ununuzi wa korosho umeshaanza, na katika Wilaya ya Msasi kuna uhaba mkubwa sana wa magunia kiasi cha kupelekea wananchi wote kuchanganyikiwa kutokana na kutopata magunia ambayo yanawawezesha wao kwenda kuuza korosho zao katika maghala.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anawambia nini wananchi wa Wilaya ya Msasi ambao hivi sasa hawajui la kufanya baada ya Serikali kushindwa kuwapelekea magunia?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wakulima wa Wilaya ya Masasi katika msimu wa mwaka 2015/2016 hawajalipwa kiasi cha shilingi bilioni moja na milioni mia sita. Katika msimu wa 2016/2017 hawajalipwa kiasi cha shilingi bilioni moja, na katika msimu huu wa sasa tayari minada mitatu imefanyika lakini kumekuwana kusua kwa kuwalipa wakulima. Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya madeni makubwa haya yaliyopo kwa wakulima wa Wilaya ya Masasi?

Je, pia Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuandamana na mimi kwenda Masasi pamoja na Mbunge wa Msasi kwenda kushuhudia tatizo la magunia lakini pia kuangalia mnada?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kukiri kabisa kwamba nimkweli kumekuwa na uhaba wa magunia kwa wakulima wa korosho katika Mikoa ya Lindi na Mtwara hususani katika Wilaya ya Masasi.

Mheshimiwa Spika, lakini kuchelewa huko naomba niliambie Bunge lako Tukufu, ni kwamba kumetokana na mkandarasi aliyekuwepo kuchelewa kufikisha magunia haya kwa wakati. Nimemuagiza Mrajisi wa Vyama vya Ushirika ambaye ndiye muhusika kwamba mkandarasi huyu awe amepewa *seven days* awe ameshakabidhi magunia haya pamoja na kamba kwa wakulima hawa wa korosho, *failure to do that* basi zabuni yake ivunjwe mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba nitoe habari njema kwa wakulima wote wa korosho hususani katika Mikoa ya Lindi na Mtwara kwamba meli itawasili katika Bandari ya Mtwara kesho kutwa Jumapili tarehe 12/11/2017, magunia milioni moja pamoja na kamba yatafika mahali pale. Vilevile na mimi katika swali la Mheshimiwa Mbunge niko radhi kwenda huko Mtwara na nategemea kwenda wiki ijayo kuhakikisha na kujiridhisha kabisa kama magunia haya na yameshafika kule *site*.

Mheshimiwa Spika, vilevile ni kwamba vyama vile vya msingi vya ushirika ambavyo viko kule, vilikuwa vimefanya uzembe katika kugawa magunia haya kiholela; na mimi namuagiza Mrajisi wa Vyama vya Ushirika ambaye ndiye anayehusika na vyama hivi kwamba avunje bodi zote za msingi za vyama hivyo vya ushirika. Mimi nitafuatilia kwa ukaribu ili kuhakikisha kabisa kwamba hili jambo limefanikiwa na linatendeka kwa haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la (b) kuhusu wale wote ambao wamefanya ubadhirifu katika kuhakikisha kwamba zao la korosho haliendi jinsi vile ambavyo inapaswa.

Ninatoa rai kwa vyombo vya dola vyote, wale wote waliosababisha ubadhirifu huu katika zao hili la korosho wahakikishe vyombo vya dola kwamba wanawakamata, wanawapeleka mahakamni na hatua kali sana za kisheria zinachukuliwa na sisi kama Wizara kwa sababu huyu ni mtoto wetu tutafuatilia kwa karibu. Ahsante.

Na.36

Hitaji la Nyumba za Askari Wilaya ya Bukombe

MHE. DOTO M. BITEKO aliuliza:-

Askari wa Wilaya ya Bukombe wanazo changamoto nyingi zikiwemo ukosefu wa nyumba za askari.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia nyumba askari hao katika Wilaya ya Bukombe?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu Sali la Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko, Mbunge wa Bukombe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Jeshi la Polisi lina changamoto mbalimbali ikiwemo uchache wa nyumba za kuishi askari. Wilaya ya Bukombe ambayo ina jumla ya maafisa wakaguzi na askari 122 ni miongoni mwa Wilaya zenye changamoto za uhaba wa nyumba za kuishi askari.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kujenga nyumba za kuishi askari katika mikao ya wialaya kwa awamu. Katika Wilaya ya Bukombe, Jeshi la Polisi lipo kwenye mazungumzo na Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe ili kupatiwa eneo kwa ajili ya kujenga nyumba za kuishi askari. Baada ya kupatiwa eneo hilo Serikali itajenga nyumba hizo kwa fedha za bajeti kwa kadri fedha zitakavyopatikana kwa jinsi ilivyotengwa pamoja na kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo.

SPIKA: Mheshimiwa Doto Biteko, Mbunge wa Bukombe.

MHE. DOTO M. BITEKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, kabla sijauliza maswali yangu mawili ya nyongeza naomba nichukue nafasi hii, nilishukuru sana Jeshi la Polisi Wilayani Bukombe kwa kudhibiti uhalifu ambao umekuwa wa mara kwa mara na kwa kutumia kikosi cha *Anti-Robbery* cha Mkoa kwa kweli wametusaidia kudhibiti uhalifu huu ambao ulikuwa unasumbua sana wananchi.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza ukweli ni kwamba sisi wa Wilaya ya Bukombe tuna eneo tayari kwa ajili ya kuwapatia polisi waweze kujenga nyumba kwa ajili ya makazi ya askari wetu. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri anithibitishie sasa ni lini wataweza kujenga kwa kuwa eneo lipo?

Mheshimiwa Spika, la pili; kwenye Kata ya Namonge pamoja na Bulega wananchi wenyewe wameamua kujenga vituo vidogo vya polisi na wamefika mahali vinahitaji *finishing* kwa ajili ya kuweka askari. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri awaambie wananchi wa Bukombe, je yuko tayari kuwasaidia wananchi ambao wamejotolea kwa kiasi kikubwa sana, aweze kukamilisha vituo vidogo hivyo vya polisi? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo ya nyongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwiguli Lameck Nchemba.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii.

Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Doto Biteko kwa jinsi anavyofanya vizuri kazi za kibunge. Amesemea sekta

zote ambazo ziko jimboni kwake kwa ufanisi mkubwa sana, na nadhani wananchi wa Bukombe watakuwa wameiona tofauti kati ya Ubunge wa Doto pamoja na ule mwingine ambao ulikuwa ni wa mvua hadi mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nimhakikishie Mheshimiwa Doto Biteko kwamba kwa kuwa kiwanja kimeshapatikana, basi mimi naelekeza wataalam wangu watengeneze ramani zinazoendana na viwango ambavyo tumevisema kama Wizara na kama Makao Makuu ya Jeshi la Polisi ili baada ya fedha kuwa zimepatikana tuweze kuanza utekelezaji wa mradi huo ambao Mheshimiwa Mbunge ameuleta.

Mheshimiwa Spika, kuhusu la pili ambalo amelisemea, wadau pamoja na vijana wangu walishafanya kazi hiyo ya kujenga nyumba na zinahitaji ukamilishwaji, nielekeze watuletee makadirio yanayohitajika kwa ajili ya ukamilishwaji ili niweze kuwakabidhi wataalam wangu na watendaji wangu waweze kutafuta kwenye akiba ya bajeti yetu tuliyonayo ili tuweze kukamilisha ili vijana wangu waweze kuhamia. Na nikupongeze Mheshimiwa Doto kwa kuwasemea vijana wangu Jeshi la Polisi kwani polisi wanapofanya kazi vizuri na mimi nakuwa Waziri wa Mambo ya Ndani mzuri na naendelea kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ukitazama watu walivyosimama maana yake iko shughuli kubwa. Sasa katika swali la polisi akisimama Mbunge wa Kibiti Mheshimiwa Ally Ungando lazima umpe nafasi. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, na Mheshimiwa Salome Makamba na wewe utauliza pia. Mheshimiwa Ally Ungando kwanza. *(Makofi)*

MHE. ALLY S. UGANDO: Mheshimiwa Spika, ahsante nashukuru. Kwanza awali ya yote niishukuru Serikali sasa hivi amani Kibiti inazidi kuimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu, wananchi wa Kibiti wametenga takribani ekari 15 kwa ajili ya ujenzi wa Polisi Kanda Maalum. Je, ni lini watajenga kituo hicho?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu ya swali hilo la wananchi wa Kibiti.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayofanya na kwa kweli amekuwa bega kwa bega kuzileta hoja za wananchi wa Kibiti pamoja na ukanda ule. Nimhakikishie tu, kwa sababu kanda tayari ilishaanza tayari tumeshateua uongozi na uongozi uko kazini kwa hiyo hatua inayofuata ni ujenzi wa jambo hilo na tunalielewa, tunategemea tu kulitekeleza kufuatana na mtiririko wa fedha kwa tutakapokuwa tunapata. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona na ningependa kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kahama nyumba za Polisi zina hali mbaya kweli, na nimewahi kuuliza hapa na kumuomba Mheshimiwa Waziri akaniahidi kwamba watatusaidia kukarabatai zile nyumba. Kwanza hazitoshi na zina hali mbaya.

Je, ni lini Mheshimiwa Waziri atakuja kutusaidia kuweza kukarabati nyumba zile ili anglaupolisi nao waweze kuishi katika mazingira mazuri? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba tafadhali.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Salome kwa kuleta jambo hili. Nilishazungukia Wilaya ya Kahama. Kama tunavyojua Kahama ni moja ya eneo *potential* sana katika nchi yetu,

hata kimakusanyo; kwa hiyo hata vijana wetu wanaokaa kule na wanapokabilia na changamoto za eneo husika wanatakiwa wawe katika mazingira mazuri. Tunalitambua jambo hilo na kwa sababu limekuwa likiletwa mara kwa mara. Niseme tu kwamba tutalipa kipaumbele, tutalipa uzito ili hadhi za nyumba za askari wetu ziweze kulingana na eneo husika.

Na. 37

Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

MHE. DEVOTHA M. MINJA aliuliza:-

Idadi ya wanafunzi wanajunga na Vyuo Vikuu vya Mkoa wa Morogoro imepungua kutokana na wanafunzi wengi kukosa mikopo ya elimu ya juu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Devatha Mathew Minja, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika elimu ya juu nchini, ambapo mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imepanga kutumia shilingi bilioni 427.54 kugharamia mikopo kwa ajili ya wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu. Kiasi hiki ni kwa ajili ya wanafunzi 112,623, ambapo wanafunzi 30,000 ni mwaka wa kwanza na wanafunzi 92,623, ni wale wanaoendelea na masomo. Katika robo ya kwanza kiasi cha shilingi bilioni 147.06 tayari kimeshatolewa kwa wakati, hivyo Serikali haitarajii kuwepo kwa ucheweleshwaji wa mikopo kwa wanafunzi ambao wamekidhi vigezo.

Mheshimiwa Spika, aidha, wanafunzi 3,307 kutoka katika vyuo vitano vya mkoani Morogoro walipata mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 11.49 katika mwaka 2016/2017. Vyuo hivyo ni Chuo Kikuu Kishiriki cha Jordan, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Kiislamu cha Morogoro, na Chuo Kikuu cha Sokoine.

Mheshimiwa Spika, suala la mikopo pekee si sababu ya ongezeko au kupungua kwa wanafunzi. Mambo mengine ni pamoja na viwango vya ufaulu alama za ukomo katika udahili, ubora wa vyuo na programu zinazotolewa kulingana na uhitaji wa soko.

SPIKA: Mheshimiwa Devotha ameridhika, tunaendelea.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Spika, nimemsikiliza Waziri amesema Serikali haitarajii kuwepo kwa ucheleweshwaji wa mikopo kwa wanafunzi ambao wamekidhi vigezo.

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita mamia ya wanafunzi wenye vigezo walikuwa wakishinda katika Bodi ya Mikopo wakifuatilia upatikanaji wa mikopo. Wengi wa wanafunzi hao wanatoka katika familia maskini, na Bodi ya Mikopo vigezo wanavyoviangalia ni ufaulu. Wanafunzi wengi ambao wanasoma katika shule binafsi zikiwemo Feza na nyinginezo wana ufaulu wahali ya juu ukilinganiswa na shule za Serikali. Hata hivyo hivi sasa wanafunzi hao wanaotoka kwenye shule za *private* ambao wana ufaulu mkubwa wanapata fursa hii ya mikopo ikilinganishwa na wanafunzi maskini wanaotoka katika shule za Serikali. Je, ni lini Serikali sasa itaangalia vigezo stahiki vya wanafunzi ambao wana uhitaji wa kuingia vyuo vikuu?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, lengo la kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo ilikuwa ni kwa wenye uhitaji, lakini sasa lengo lile limebadilika na sasa hivi mikopo inatolewa kwa kozi, kwa mfano wanaosoma udaktari, *engineering* wanapata mikopo kwa asilimia 100. Ni nani

amesema kwamba nchi hii haihitaji *accountants*? Nani amesema nchi haihitaji waandishi wa habari? Nani amesema haihitaji *lawyers*? Naomba majibu ni kwa nini sasa Serikali isianganalie namna ya kutoa mikopo kwa kuangaliwa mahitaji ya wanafunzi wa hali ya juu?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo. Waheshimiwa upande wangu wa kulia yaani hata kinachoendelea huku hamna habari kabisa, ninyi mnapiga *story* tu. (*Makofi*)

Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba leo hii Wizara yetu itatoa Kauli ya Serikali kuhusiana na masuala ya udahili na mikopo, kwa hiyo tutaelezea kwa kirefu kidogo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo itoshe tu kwa ajili ya maswali ya nyongeza niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu wanafunzi kuandamana kwa sababu ya kucheleweshewa mikopo, naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba Bunge hili lilipitisha shilingi bilioni 427 kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa mwaka wa kwanza na wale wanaoendelea.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wa mwaka wa kwanza wanaotegemea kupata mikopo ni 30,000. Tayari Serikali imetoa mikopo kwa wanafunzi 29,578. Tofauti na huko nyuma wakati huu fedha ilitangulia kwenye bodi, wanafunzi ndio wanaenda kuomba, wakati huko nyuma fedha zilikuwa zinachelewa. Tayari Serikali imeshatoa shilingi i bilioni 147 kwa ajili ya robo ya kwanza ya mwaka. Kilichotokea ni kwamba taratibu za udahili ambazo wakati huu wanafunzi wenyewe ndio walikuwa wanachagua vyyo ndizo zimechelewesha utolewaji wa mikopo na ndiyo maana kuna hawa wanafunzi wachache ambao bado hawajapata mikopo. Lakini kama ninavyokwambia tayari wanafunzi 29,578 wameshapata mikopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili linalohusu vigezo vinavyotumika. Naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna vigezo vikuu vinne vinavyotumika kwaajili ya kutoa mikopo.

Mheshimiwa Spika, kigezo cha kwanza ni uyatima, kigezo cha pili ni ulemavu, kigezo cha tatu ni uduni halafu kingine ni ile kuangalia masomo ya kipaumbele kulingana na mipango ya maendeleo ya taifa. Sasa wanapochanganya vigezo hivi vyote ndipo tunapata idadi ya wale wanafunzi ambao watapata mikopo. Kwa hiyo baadaye Mheshimwa Waziri atakapotoa taarifa atatoa takwimu kuonesha kwamba vigezo hivi vimezingatiwa na wanafunzi wale ambao tunasema wanastahili zaidi ndio hasa wamekuwa walengwa na ndio wamepata mikopo. Nashukuru sana.

Na. 38

Hitaji la Bweni Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi

MHE.ESTHER A. MAHAWE (K.n.y. MHE. ESTHER M. MMASI) aliuliza:-

Kupitia fursa za ujenzi wa mabweni ya wanafunzi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwezi Aprili, 2017.

Je, Serikali imeweka jitihada gani katika kuongeza fursa za ujenzi wa mabweni kwa Taasisi za Elimu ya Juu hususani Chuo cha Ushirika Moshi Mkoani Kilimanjaro ambapo zaidi ya 70% ya wanafunzi wanaishi nje ya chuo?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Mmasi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji katika vyuo vikuu nchini, Serikali

imewezesha ujenzi wa mabweni mapya 20 katika chuo kikuu cha Dar es Salaam vyenye uwezo wa kubeba wanafunzi 3,840 na kukamilisha ujenzi wa Chuo Kikuu cha Taaluma cha Tiba (MUHAS). Aidha, Serikali imefanya juhudi za kuainisha hali ya miundominu katika vyuo vya elimu ya juu ili kubaini mahitaji halisi. Baada ya tathmini hiyo, kupitia Mradi wa Malipo kwa Matokeo (*P for R*) Serikali imeanza ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya vyuo vikuu vya Sokoine, Dares Salaam, Ushirika Moshi na Mzumbe.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi kina *hostel* zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 900 kwa wakati mmoja, idadi hii ni sawa na asilimia 25% ya wanafunzi wote. Ili kuhakikisha mazingira bora ya malazi kwa wanafunzi, chuo kina mpango wa kujenga *hostel* zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 3,500 kwa wakati mmoja. Mpango huu umebainishwa katika mpango mkakati wa chuo wa miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 chuo kupitia miradi ya maendeleo ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kinategemea kupatiwa fedha za ujenzi wa *hostel* zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja. Ujenzi huu ukikamilika utasaidia kutatua kwa kiasi kikubwa tatizo la malazi kwa wanafunzi na hivyo kuchangia katika kufanikisha azma ya Serikali ya kuzalisha wataalam wengi. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Esther Mahawe ameridhika, tunaendelea na programu. Nashukuru kwa uendeshaji wa kisayansi tumemaliza *exactly on time* leo.

Kuhusu wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ambao ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge tuna wageni 106 wa Mheshimiwa Antony Mavunde, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira ambao ni wanafunzi 101 wa kidato cha sita na walimu 5 kutoka shule ya Sekondari ya Dodoma ya Mkoa wa Dodoma; karibuni sana watoto wetu. Waheshiwa Wabunge Sekondari hii ni wale majirani zetu kabisa, ukivuka barabara tu, kwa hiyo karibuni sana. Zamani

ilikuwa inaishia *form four* tu kumbe sasa hivi ina mpaka *form six*. (Makofi)

Wageni 42 wa Waheshiwa Wabunge Cecilia Paresso, Kaimu Mwenyekiti wa APNAC na Mheshimiwa Daniel Mtuka, Katibu Mkuu wa APNAC ambao ni wanachama wa Mtandao wa *Policy Forum* kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana mjengoni, ahsante sana. (Makofi)

Matangazo ni hayo tu, tunaendelea, Katibu!

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

NDG. LAWRENCE MAKIGI-KATIBU MEZANI: Kauli za Mawaziri.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Haya Katibu nipe majina yao haraka haraka.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Spika, Sixtus Mapunda.

SPIKA: Hakuna haja ya kutaja Makatibu wanapaswa kuwajua.

Liko tangazo la ziada, Waheshimiwa Wabunge tangazo hili linatoka kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Selemani Jafo kwa kushirikiana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Uratibu na Bunge, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mheshimiwa Stella Manyanya, wanawaalika Waheshimiwa Wabunge wote, wafanyakazi wa Bunge na Wana Dodoma wote mtakaopenda kushiriki katika uzinduzi wa kampeni ya viwanda vyetu, Mkoa wetu inayolenga kuhamasisha ujenzi wa viwanda vidogo na vya kati katika mamlaka za Serikali za Mitaa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, uzinduzi huo utafanyika katika Ukumbi wa Chuo cha Mipango kuanzia saa nane mchana

hadi saa kumi jioni tarehe 9 Novemba, 2017 ambayo ni leo. Kwa hiyo kuna shughuli kule Chuo cha Mipango saa nane hadi saa kumi inayohusisha na kampeni ya viwanda vyetu, Mkoa wetu, Waheshimiwa Wabunge mtakapopata nafasi mnakaribishwa kufika kule. (*Makofi*)

MWONGOZO WA SPIKA

SPIKA: Sixtus Mapunda.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninasimama hapa kwa mujibu wa Kanuni ya 47, kutokana na muda naomba nisisome.

Mheshimiwa Spika, kwa nyakati tofauti Serikali iliitangaza Mikoa ya Ruvuma, Njombe, Iringa, Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi kama ndiyo mikoa pekee yenye dhamana ya kuhakikisha kunakuwa na usalama wa chakula nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na msukumo mkubwa wa Serikali wananchi wa maeneo hayo walilazimika kulima kwa nguvu zao zote, na hata ikafikia hatua mazao ya jadi ya kibiashara ya kahawa, chai na tumbaku kuathirika kutokana na msukumo huu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo *record* zinaonyesha nchi yetu imekuwa na mfumuko wa bei unahimilika wa chini ya *single digit* kutokana na uhakika wa mahindi kuwepo nchini kwa muda wote. Hivyo *stability* ya nchi yetu kwenye uchumi kwa asilimia 100 unatokana na uwepo wa zao la mahindi kwa wakati wote.

Mheshimiwa Spika, sasa mwongozo wangu ni hivi hali hii ya sasa iliyoko kwenye haya maeneo kuna mahindi yamerundikana kwa wakulima hayajanunuliwa na mwezi Novemba hii tunakwenda kwenye mfumo wa masika. Mahindi yasiponunuliwa au yasipochukuliwa kwa mkulima matokeo yake mwakani watashindwa kulima, na wasipolima mwakani tutakosa chakula. Hii ajenda ni ajenda

nzito kwa sababu ina sura ya kiuchumi ina sura ya kijamii na ina sura ya kisiasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikuombe Bunge hili liijadili hii hoja kwa kina; kwa sababu tusipotoka na suluhu, tusipoishauri Serikali vizuri mwakani *infection rate* itakuwa kubwa kwa sababu hakutakuwa na chakula, na chakula kingine ambacho si mahindi, mtakumbuka wa mwaka jana...

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Spika, mchele ulikuwepo lakini kwa sababu mahindi hayakuwepo watu wakalalamika kwamba kuna njaa.

KUHUSU UTARATIBU

SPIKA: Haya, kuhusu Utaratibu, nipe Kanuni.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, hoja ni nzuri sana lakini Mheshimiwa...

SPIKA: Kanuni yako?

MHE. MWITA M. MWAITARA: Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 47 ambayo Mheshimiwa msemaji anaitumia ni tofauti na ambacho yeye ameomba Mwongozo kwako Kanuni ya 68(7). Anatumia Kanuni ya 47 ambayo haihusiani na mwongozo, na hapa kanuni inazungumza jambo ambalo limetokea Bungeni mapema leo. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mapunda!

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu niendeleo. Hoja hii ya mahindi na si ya mahindi tu nina imani inagusa na tumbaku vile vile, ni ajenda nzito. Niombe Bunge lako liijadili hii na liishauri Serikali namna bora ya ku-*rescue* hali hii tukiacha mwakani hali itakuwa mbaya zaidi. Ahsante.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

SPIKA: Nawaona Waheshimiwa Wabunge mnavyouna mkono hoja, naomba make sasa. Ni hoja nzito na imeungwa mkono sana, lakini kama alivyosema Mheshimiwa Mwitwa Mwikabe kanuni zilizotumika zimejichanganya siyo. *(Makofi)*

Sasa Mheshimiwa Mapunda kwa vile umekosea kanuni sitaweza kulichukua jambo lako. Wakati mwingine Waheshimiwa Wabunge mjipange vizuri mnapokuwa na hoja. *(Makofi/Kicheko)*

Jambo la pili kwa ujumla Waheshimiwa Wabunge tunazo kamati mbalimbali, na mnakuja na mnatangulia kabla ya Bunge mnakuwa na *session* na ratiba mnajipangia ninyi wenyewe kwenye kamati kwa sehemu kubwa.

Mheshimiwa Spika, hivi Kamati hizi kwa nini zenyewe haziji na hoja muhimu kama hizo; kama Kamati ya Kilimo, Maji na kadhalika imeleta jambo, hapa kama Kamati? Huko kwenye Kamati mnajadili nini endapo kuna mambo mazito mnayoeleza endapo yapo? Kwa nini mambo haya hayapewi kipaumbele kwanza? Kwa mfano mngesimama kama Kamati mkatoa hoja kama hii kwa vyovyote vile hapa pangebadijika ratiba. Muda si mrefu.

MBUNGE FULANI: Mwenyekiti wa Kamati simama.

SPIKA: Hapana, asisimame, mimi nauliza Wanakamati wote. Hata wale wa kamati za Huduma za Jamii, kwa mfano, mbele kidogo tutakuwa na Kauli ya Serikali ya kuhusu mambo ya elimu. Kama Kamati ya Huduma za Jamii mngejipanga vizuri kwa yanayotokea tusingelazimika kutumia muda wetu kwa ajili ya jambo hilo, la sivyo Kamati ndio mngekuja na hoja hapa ya nini kifanyike. Na Kamati nyingine vivyo hivyo, yaani msione mambo yanatokea halafu ninyi mnakaa tu mnasubiri Spika awalettee wakati ninyi kama Kamati ndio mnaojipangia shughuli zenu za kufanya na mambo ya kushughulikia.

Kwa hiyo, nawachagiza Wenyekiti na Wajumbe wa Kamati wote kwamba mnapoona mambo yanaendelea basi myachukue mya-*own* kama Kamati.

SPIKA: Mheshimiwa Mlinga Goodluck.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba mwongozo kwa kanuni ya 68(7), jambo ambalo limetokea leo Bungeni mapema.

Mheshimiwa Spika, Mwongozo wangu una-*target* kwenye swali lililoulizwa kuhusiana na Mheshimiwa Lissu.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niweke wazi, Mheshimiwa Lissu ni mwanasiasa mwenzangu moja, mbili Mheshimiwa Lissu ni Mbunge mwenzangu, tatu Mheshimiwa Lissu ni Mwanakamati mwenzangu, mwisho Mheshimiwa Lissu ni Mbunge mwenzangu machachari, kwa hiyo nimeguswa kutokana na tukio lake lililomtokea.

Mheshimiwa Spika, ukiacha hayo yote, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama sikosei Ibara ya 12 inasema hivi, moja: "Binadamu wote ni sawa na ni huru" na mbili, "binadamu wote wanastahili kuheshimiwa na kutambulika utu wao."

Mheshimiwa Spika, hoja zangu ni kwamba, Mheshimiwa Mbowe ameomba ufanyike uchunguzi *specific* kwa ajili ya Mheshimiwa Lissu ambapo ni kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa vifungu ambavyo nimevitaja.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Mheshimiwa Mbowe hakuomba usaidizi wa uchunguzi wa kimataifa kwenye matukio ya mauaji ya albino, aombe kwa ajili ya Mheshimiwa Lissu au kwa sababu wanasema wanasiasa walikuwa wanahusika na mauaji ya albino na yeye ni mmojawapo anayehusika? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mbili, kwa nini Mheshimiwa Mbowe hakuomba usaidizi wa uchunguzi kwa taasisi za kimataifa kwenye matukio ya Kibiti; kwa nini Mheshimiwa Mbowe hakuomba usaidizi wa kimataifa kwenye uchunguzi wa mauaji ya vikongwe? Tukio la kifo cha Chacha Wangwe, tukio lililompata Mchungaji Christopher Mtikila, kwa nini hakuomba uchunguzi wa kimataifa?

Mheshimiwa Spika, Mwongozo wangu ni kwamba umekubali Bunge lako kutumika kama kitovu cha kuleta matabaka baina ya watu fulani na watu fulani? Naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)

SPIKA: Sasa mbona mnaongea sana, nitatoaje Mwongozo? Waheshimiwa Wabunge, hapo sina Mwongozo. Katibu tuendelee.

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

KAULI ZA MAWAZIRI

SPIKA: Kauli za Mawaziri, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Profesa Ndalichako, tafadhali.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, tarehe 7 Novemba, 2017 baada ya kipindi cha maswali uliagiza Serikali itoe kauli kuhusu udahili na utoaji mikopo kwa ajili ya wanafunzi wa elimu ya juu.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge wote nawaomba sana tusikilizane. Naomba tusikilizane tafadhali, tumsikilize

Mheshimiwa Waziri, kauli hii ni muhimu. Watanzania wengi wanaisikiliza, wazazi wanaisikiliza, walezi wanaisikiliza, wanafunzi wa elimu ya juu wanaisikiliza. Wale mnaotaka kuongea, mnaweza mkaenda kwenye *corridor* zetu huko nje mkaendelea.

Mheshimiwa Waziri, tafadhali endelea.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, tarehe 7 Novemba, 2017 baada ya kipindi cha maswali uliagiza Serikali itoe kauli kuhusu udahili na utoaji mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Maagizo hayo yalitokana na Mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Martha Mlata, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 49 ya Kanuni za Kudumu za Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kutoa kauli ya Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nitaanza na udahili wa wanafunzi kwa mwaka 2017/2018. Udahili wa wanafunzi umefanyika kwa wanafunzi watarajiwa kutuma maombi yao moja kwa moja kwenye vyuo wanavyovitaka na kuchagua programu wanazozitaka. Vyuo vilichakata maombi ya wanafunzi na hatimaye kuwasilisha majina Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ambayo kisheria ina jukumu la kudhibiti ubora wa elimu ya juu ikiwa ni pamoja na kuhakiki sifa za wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, TCU ilifanya kazi ya uhakiki kwa kutumia mfumo wa mtandao (*University Information Management System*) ulioandaliwa kwa ajili hiyo ambao umeunganishwa na kanzidata za Baraza la Mitihani la Tanzania pamoja na Baraza a Taifa la Elimu ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa ya kuhakiki ilihusisha mambo yafuatayo:-

(i) Usafirishaji wa taarifa ili kuondoa majina yaliyokuwa yanajirudia na kurekebisha taarifa zilizowekwa kwa mtiririko usio sahihi;

(ii) Kuhakiki taarifa za waombaji kupitia kanzidata za Baraza la Mitihani na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi;

(iii) Kuhakiki uwezo wa programu kulingana na idadi ya waombaji waliodahiliwa na idadi ya Wahadhiri walioko katika chuo husika;

(iv) Kubaini waombaji waliodahiliwa kwenye vyuo zaidi ya kimoja au programu zaidi ya moja katika chuo kimoja;

(v) Kuhakiki sifa za waombaji katika programu waliodahiliwa kwa kuzingatia matakwa ya programu husika; na

(vi) Kuhakiki programu zilizoruhusiwa kudahili wanafunzi wapa kwa mwaka wa masomo 2017/2018 ili kujiridhisha kama vyuo havikuchagua wanafunzi kwenye programu ambazo zilisitishiwa udahili au zisizo na ithibati.

Mheshimiwa Spika, udahili wa wanafunzi walioomba kujiunga na Vyuo Vikuu 2017/2018 umefanyika kwa awamu tatu na umehusisha vyuo vya elimu ya juu 67 na matokeo ya udahili yalikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza ilihusisha maombi yaliyopokelewa kuanzia tarehe 22 Julai mpaka tarehe 31 Agosti, 2017. Vyuo na taasisi ziliwasilisha *TCU* majina ya waombaji waliodahiliwa tarehe 18 Septemba, 2017 ili iyapitie kama nilivyoeleza hapo juu.

Mheshimiwa Spika, jumla ya majina 77,756 yalipokelewa na *TCU* na wanafunzi waliokuwa wamechaguliwa na vyuo kwenye awamu ya kwanza walikuwa ni 44,627. Waombaji ambao hawakuwa wamechaguliwa katika awamu ya kwanza walikuwa ama hawana sifa katika programu walizoomba au walikuwa na

sifa lakini walikuwa wamechagua programu ambazo zilikuwa na ushindani mkubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya uhakiki, waombaji 36,831 waliidhinishwa kujiunga na masomo ya shahada za kwanza katika vyuo mbalimbali hapa nchini. Kati ya wanafunzi walioidhinishwa 20,247 walikuwa hawana utata kwa sababu walikuwa wamechaguliwa kwenye programu moja tu au katika chuo kimoja tu.

Mheshimiwa Spika, waombaji 16,584 walikuwa wamechaguliwa kwenye chuo zaidi ya kimoja au programu zaidi ya moja. Aidha, waombaji 7,796 walikuwa na kasoro mbalimbali kwenye taarifa zao na hivyo kuwafanya kukosa sifa za kujiunga na chuo.

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako naomba nitoe tu maelezo ya ziada, kwamba kimsingi tulitakiwa kufanya udahili mara moja tu, lakini kutokana na idadi kubwa kama unavyoona ambayo wanafunzi kwenye awamu ya kwanza hawakupata na kwa kuzingatia kuwa lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wenye sifa za kujiunga na vyuo vikuu wanapata nafasi kadri inavyowezekana, Serikali iliona kuna umuhimu wa kutoa nafasi kwa wale ambao hawakupata sifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kuzingatia kuwa baadhi ya wanafunzi walikuwa na udahili zaidi ya chuo kimoja, pia wengine walikosa sifa, wamefaulu vizuri, ana *division one* lakini amechagua programu ambazo zina ushindani mkubwa. Kuna wengine walikuwa tu na kasoro ndogo ndogo, hawa ni vijana wetu, sisi kama Serikali tuliona kwamba kuna umuhimu wa kuwapa nafasi nyingine. Kwa hiyo, tukaruhusu udahili kwa awamu ya pili.

Mheshimiwa Spika, maombi ya awamu ya pili yalipokelewa tarehe 4 hadi 10 Oktoba, 2017 na lengo kubwa kama nilivyosema ilikuwa ni kuwa na udahili mmoja na lengo la awamu ya pili kimsingi lilikuwa linawalenga wanafunzi tu wale ambao walikuwa hawakupata udahili katika awamu

ya kwanza. Kwa bahati mbaya kilichotokea ni kwamba hata wanafunzi waliokuwa wamechagua awamu ya pili waliamua kuomba tena programu tofauti na zile walizokuwa wamekwishaidhinishiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya uhakiki wa udahili katika awamu ya pili jumla ya waombaji 19,488 waliidhinishwa kuwa na sifa ya kujiunga na chuo kikuu. Hata hivyo, waombaji 9,252 walikuwa tena wamechaguliwa zaidi ya chuo kimoja. Kwa hiyo, kwa mara nyingine kwa sababu lengo la Serikali ni kutoa fursa kwa wanafunzi bado tuliona kuna kundi kubwa. Pia kwa kuzingatia kwamba vyuo vilikuwa vinakaribia kufunguliwa tukaona tena tuwape wanafunzi vijana wetu nafasi kwa mara ya tatu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukawafungulia tena udahili, kuanzia tarehe 16 mpaka 22 Oktoba, 2017 ili kutoa nafasi ya mwisho kwa wanafunzi ambao walikuwa kwanza, ama hawajathibitisha wale waliokuwa na vyuo viwili watajiunga na vyuo vipi waweze kufanya hivyo, lakini na wale ambao waliendelea awamu ya pili kuomba katika vyuo ambavyo vilikuwa na ushindani mkubwa waweze kuomba katika programu ambazo zilikuwa na nafasi.

Mheshimiwa Spika, baada ya uhakiki katika awamu ya tatu, waombaji 7,418 walithibitishwa kujiunga na vyuo na idadi hiyo ikafanya jumla ya waombaji wote walioidhinishwa na TCU kujiunga na vyuo vikuu mbalimbali nchini hadi kukamilika kwa awamu zote tatu kufikia 63,737. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutokana na changamoto za vijana wetu ambayo niliahidi Bunge lako kwamba tutatoa elimu kwa watakaomba miaka inayokuja, bado wanakuwa hawajajua wanataka nini. Tulipofungua awamu ya tatu bado wale walioidhinishwa awamu ya kwanza na ya pili wengine wakawa wanaomba kubadilisha programu zao. Kwa hiyo, mpaka tunafunga udahili wanafunzi 28,466 walikuwa wamedahiliwa kwenye chuo zaidi ya kimoja.

Mheshimiwa Spika, *TCU* ilibaini kuwa baadhi ya waombaji ambao tayari walikuwa wamekwishapata vyo uo katika awamu za kwanza waliomba tena na kwa kuzingatia kuwa vyo vilikuwa vinafunguliwa kuanzia tarehe 30 Oktoba, tukawapa uhuru kama tunavyosema lengo la udahili mwaka huu ilikuwa ni kutoa uhuru kwa wanafunzi kuamua anaenda kusoma wapi. Kwa hiyo, wanafunzi ambao walikuwa wanadahili kwenye zaidi ya chuo kimoja tukawaambia wachague wenyewe kwamba ni wapi wanataka kwenda kusoma na wakajisajili pale walipochagua wenyewe.

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyojitokeza kwa kitendo cha baadhi ya wanafunzi kuendelea kubadilisha programu au vyo walivyochaguliwa baada ya kuwa wameidhinishwa na *TCU* kimesababisha kwamba upangaji wa mikopo, kwa sababu lengo la kuthibitisha na *TCU* ilikuwa tupate *clean data*, maana huwezi ukapeleka mkopo kwa mwanafunzi ambaye amedahiliwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, amedahiliwa na *SUA*. Tulikuwa tunataka tujiridhishe, ndiyo maana wanafunzi walikuwa wanapewa nafasi ya kuthibitisha ili yule ambaye ameshatuthibitishia kwamba mimi nitaenda katika chuo hiki ndiye tumpangie mkopo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kutokana na changamoto hii ya kubadilisha vyo hata katika awamu ya pili na ya tatu imeleta pia changamoto katika utoaji wa mikopo ambayo nitaelezea.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijielekeze katika utoaji wa mikopo kwa mwaka 2017/2018. Katika mwaka wa fedha Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha shilingi bilioni 427.54 kwa ajili ya kugharamia mikopo kwa ajili ya wanafunzi wenye uhitaji na waliidahiliwa katika vyo vya elimu ya juu nchini. Mikopo hii ilikuwa inawalenga wanafunzi 122,623 na lengo ilikuwa ni kutoa mikopo kwa wanafunzi 30,000 wa mwaka wa kwanza na wanafunzi 92,623 wanaoendelea na masomo.

Mheshimiwa Spika, kwa shukrani kubwa kabisa niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara tayari imepokea kiasi cha

shilingi bilioni 147.06 kwa ajili ya kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kwa robo ya kwanza na fedha hizi Wizara ilizipokea tarehe 9 Oktoba, 2017.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia kidogo mfumo uliotumika kupanga mikopo. Mfumo umezingatia vigezo vilivyowekwa ambavyo pamoja na mambo mengine, vimeangalia wanafunzi wenye ulemavu wamepewa kipaumbele, wanafunzi yatima na wanafunzi wenye uhitaji lakini hasa katika programu za kipaumbele. Upangaji wa mikopo umekuwa ukifanyika kwa awamu kama nilivyoeleza baada ya *TCU* kutoa majina yalikuwa yanapelekwa sasa wakapate mikopo.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa yangu nimeonesha awamu mbalimbali ambapo mikopo imetolewa...

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, bado una dakika tano tu.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Ooh! Sawa.Hadi kufikia tarehe 7 Novemba, 2017 jumla ya wanafunzi 27,578 walikuwa wamepata mikopo.

Mheshimiwa Spika, changamoto ambazo zimejitokeza katika utoaji mikopo ni baadhi ya waombaji kutozingatia maelekezo ya uombaji kama vile kutoambatanisha nyaraka muhimu kuthibitisha uhitaji wao. Pia baadhi ya wanafunzi ambao mikopo yao ilikuwa imeshapelekwa sehemu nyingine wameenda tofauti na sehemu ambazo wamekwishapangiwa. Kwa hiyo, hatua zinazochukuliwa ni kuendelea kupokea taarifa za ziada ili kuhakikisha kwamba wale ambao hawakuwa wameleta vielelezo wanashughulikiwa lakini pia kukamilisha taratibu za wanafunzi ambao hawakupangiwa mikopo lakini wanaona kwamba wana uhitaji kuendelea kuwasilisha katika Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa wanafunzi ambao mikopo yao imepelekwa katika vyuo vingine niwahakikishie

wanafunzi hao kwamba mikopo yao itahamishiwa huko wanakosoma kwa sababu tunaheshimu uhuru wa mwanafunzi kuamua akasome wapi. Kwa hiyo, hiyo itahamishwa mara baada ya wao kujisajili kule ambako wamekwenda tofauti na ambako awali walikuwa wamedahiliwa wakaenda chuo kingine.

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kusema yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali inaona mfumo wa udahili uliotumika ni mzuri kwa sababu umetoa uhuru kwa wanafunzi kutimiza ndoto zao kwa kusoma jambo ambalo wanalitaka. Hivyo basi, Serikali itaendelea kutumia mfumo huu hata kwa miaka ijayo kwa maslahi mapana ya vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu utatoa uwazi zaidi kwa namna ambavyo wanafunzi wanajunga na vyuo kwa sababu anachagua mwenyewe na wanapotoa majina wanakuwa wanaonesha nani amepata na nani amekosa.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itaendelea kuimarisha mfumo huu wa uchambuzi hasa katika kipengele cha wanafunzi kuthibitisha vyuo na hii kuondoa mwanafunzi kuendelea kuomba hata baada ya kuwa amethibitishwa ili kupunguza changamoto za kimfumo zilizojitokeza.

Mheshimiwa Spika, kwa wanafunzi ambao bado hawajakamilisha taratibu za usajili, Serikali inaelekeza wafanye hivyo mara moja ili wale wanufaika wa mikopo waweze kupata fedha zao ambazo tayari zimekwisha kwenda kwenye vyuo husika. Pia nitumie fursa hii kuwataka wanafunzi wanaoendelea na masomo ambao ni wanufaika wa mikopo kuhakikisha kwamba wanakamilisha taratibu za kuripoti vyuoni ili wapate fedha zao ambazo tayari ziko katika vyuo wanavyosoma.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Martha Mlata

alizungumzia kitendo cha wanafunzi kutakiwa walipe fedha za usajili kabla ya kupewa mkopo. Jambo hili hata wewe ulilizungumza kwa msisitizo mkubwa sana. Serikali imekwisha waagiza Wakuu wote wa Vyuo vya Elimu ya Juu nchini kuacha mara moja urasimu katika kutoa mikopo kwa wanufaika wa elimu ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba wanafunzi wana makubaliano na Serikali, huu ni mkopo, mwisho wa siku mwanafunzi ataurudisha. Kwa hiyo, hakuna mtu ambaye anatakiwa katikati kuingiza urasimu kati ya mkopo wa mwanafunzi na Serikali. Vyuo vinapaswa kuwasajili wanafunzi wote kwa kuzingatia taratibu zilizopo na mazingira halisi yanayojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako kidogo tu najua muda unakwenda, lakini niseme tu kwamba nilipokea hata malalamiko kwamba baadhi ya vyuo vikuu vya umma na Chuo Kikuu cha Dodoma kilitajwa, Sokoine na Mwalimu Nyerere kwamba vilikuwa na urasimu wa kukataa kupokea wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, nimeongea mwenyewe na wakuu wa vyuo na nimewasisitiza kwamba waache urasimu katika kuwasajili wanafunzi vyuoni. Mkuu wa Chuo, kwa mfano cha Dodoma amenihakikishia kwamba wanawapokea wanafunzi wote bila kuwabagua, bila kuwawekea masharti na nisisitize kama kuna kuna Mkuu yeyote wa Chuo ambaye anaweka vizingiti kwa wanafunzi ahakikishe anaacha mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, naviagiza vyuo vikuu vyote nchini kuhakikisha kwamba vinawasajili wanafunzi mara moja ili wanufaika wa mikopo waweze kupata fedha zao ambazo tayari ziko vyuoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kuona kwamba baadhi ya vyuo vinadiriki hata kuwakataa wanafunzi, wanawaambia kwamba nafasi zimejaa wakati wanafunzi

waliomba wenyewe, vyo vyenyewe vikawapokea, halafu leo mwanafunzi anaenda wanamwambia kwamba hii kozi imejaa omba kozi nyingine. Mfano ni Chuo Kikuu cha Mwenge, jambo hili halikubaliki hata kidogo. Jambo hili linaleta hata mashaka kuhusu uadilifu wa baadhi ya vyo vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiagiza Tume ya Vyo Vikuu kufuatilia kwa karibu haya yote yanayoendelea kwenye vyo vyetu vya elimu ya juu ili kuhakikisha kwamba, hatua kali zinachukuliwa kwa watu ambao wanaenda kinyume na matakwa ya Serikali. Serikali haitasita hata kufunga vyo ambavyo vinakuwa vinawasumbua watoto wetu. Hawa wanafunzi sio wazururaji wametoka nyumbani kwao ili wasome, kwa hiyo vyo viache kuwapotezea muda vijana wanakuwa kama wazururaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapohitimisha taarifa yangu sina budi kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Tano, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa uongozi wake uliotukuka na kwa kuwajali Watanzania wote, ikiwa ni pamoja na wanafunzi wa elimu ya juu. Haijawahi kutokea hata mara moja fedha kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu zikatolewa mwezi mmoja kabla ya vyo kufunguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakika Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli anawatendea haki Watanzania ambao ndio wamempa ridhaa ya kuongoza nchi hii. Kwa sababu hiyo, Wizara yangu haitakubali kwa namna yoyote ile mtu ambaye anataka kurudisha nyuma juhudi za Serikali za kuondoa kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara yangu haitakuwa na huruma na chuo ambacho kitachelewesha malipo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na hatuwezi kuruhusu mtu yeyote au chuo chochote, iwe ni cha umma au ni cha binafsi kuweza kuhujumu kazi nzuri ambayo inafanywa na Mheshimiwa Rais wetu. Fedha za mikopo tayari ziko chuoni na hivyo Wakuu wa Vyo nawaagiza kwa mara ya mwisho, kuhakikisha

kwamba wanafunzi wote wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu wapewe fedha zao mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**KAULI YA SERIKALI KUHUSU UDAHILI NA UTOAJI WA MIKOPO
KWA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU KWA MWAKA 2017/18
ILİYOTOLEWA NA PROF. JOYCE L. NDALICHAKO (MB)
WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA,
TAREHE 09 NOVEMBA, 2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA
MEZANI**

Mheshimiwa Spika, tarehe 7/11/2017 baada ya kipindi cha Maswali, uliagiza Serikali itoe kauli kuhusu udahili na utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu. Maagizo hayo yalitokana na mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Martha Mlata, Mbunge wa Viti Maalum. Kwa mujibu wa Kanuni ya 49 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, naomba kutoa Kauli ya Serikali kama ifuatavyo.

1.0 Udahili wa Wanafunzi mwaka 2017/2018

Mheshimiwa Spika, Udahili wa wanafunzi wanaojiunga na Vyuo Vikuu kwa mwaka 2017/18 umefanyika kwa wanafunzi watarajiwa kutuma maombi yao moja kwa moja kwenye vyuo wanavyovitaka na kuchagua programu wanazozitaka. Vyuo vilichakata maombi hayo na hatimaye kuyawasilisha Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) ambayo kisheria ina jukumu la kudhibiti ubora wa Elimu ya Juu, ikiwa ni pamoja na kuhakiki sifa za waombaji. TCU ilifanya kazi ya uhakiki kwa kutumia mfumo wa mtandao, "University Information Management System-UIMS", ulioandaliwa kwa ajili hiyo ambao umeunganishwa na kanzidata (database) za Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE). Kazi kubwa ya uhakiki ilihusisha mambo yafuatayo:

i) Usafishaji wa taarifa (data cleaning) ili kuondoa majina yaliyojirudia (duplicates) na kurekebisha taarifa zilizowekwa kwa mtiririko usio sahihi (misallocated entries).

- ii) Kuhakiki taarifa za waombaji kupitia kanzidata za NECTA na NACTE;
- iii) Kuhakiki uwezo wa programu kulingana na idadi ya waombaji waliodahiliwa na idadi ya Wahadhiri waliopo kwenye Chuo husika;
- iv) Kubaini waombaji waliodahiliwa kwenye vyuo zaidi ya kimoja au programu zaidi ya moja katika chuo kimoja;
- v) Kuhakiki sifa za waombaji katika kila programu waliyodahiliwa kwa kuzingatia matakwa ya programu husika;
- vi) Kuhakiki programu zilizoruhusiwa kudahili wanafunzi wapya mwaka wa masomo 2017/18 ili kujiridhisha kama Vyuo havikuchagua wanafunzi kwenye programu zilizositishiwa udahili au zisizo na ithibati.

2.0 Matokeo ya Udahili

Mheshimiwa Spika, Udahili wa wanafunzi walioomba kujiunga na Vyuo vya Elimu ya Juu 2017/18 ulifanyika kwa awamu tatu na ulihusisha jumla ya Vyuo na Taasisi za Elimu ya Juu 67. Matokeo ya Udahili yalikuwa kama ifuatavyo:

i) Udahili Awamu ya Kwanza

Awamu ya kwanza ilihusisha maombi yaliyopokelewa kati ya tarehe **22 Julai** na **31 Agosti 2017** Vyuo na Taasisi ziliwasilisha TCU majina ya waombaji waliowadahili tarehe **18 Septemba 2017** ili iyapitie na kuyaidhinisha kabla hayajatangazwa na vyuo husika. Matokeo ya uhakiki wa TCU katika awamu hii yalibainisha yafuatayo:

- a) Jumla ya majina **77,756** (wanaume 47,501 wanawake 30,255) yalipokelewa na TCU. Wanafunzi waliokuwa wamechaguliwa na vyuo kwenye awamu ya kwanza walikuwa ni **44,627** (wanaume 27,116 wanawake 17,511).

Waombaji ambao hawakuwa wamechaguliwa awamu ya kwanza walikuwa ama hawana sifa katika programu walizoomba au walikuwa wameomba vyuo na programu zilizokuwa na ushindani mkubwa.

b) Baada ya uhakiki waombaji **36,831** (wanaume 22,319 wanawake 14,512) waliidhinishwa kujiunga na masomo ya shahada za kwanza katika vyuo mbalimbali hapa nchini katika awamu ya kwanza, Kati yao, waombaji **20,247** walioidhinishwa wanaume 12,396 na wanawake 7,851 walikuwa hawana utata kwa sababu walikuwa wamechaguliwa kwenye programu moja tu na kwa Chuo kimoja tu. Waombaji **16,584 (37.2%)**, wanaume (9,923 wanawake 6,661), walikuwa wamechaguliwa kwenye zaidi ya chuo kimoja. Aidha, waombaji **7,796 (17.4%)**, wanaume 4,797 wanawake 2,999, walikuwa na kasoro mbalimbali kwenye taarifa zao na hivyo kuwafanya kukosa sifa za kujiunga na vyuo vilivyowapendekeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wenye sifa za kujiunga na Vyuo Vikuu wanapata udahili kulingana na nafasi zilizopo kwa kuzingatia idadi kubwa ya wanafunzi waliokuwa na udahili kwenye Vyuo zaidi ya kimoja, waliokosa sifa kwa sababu ya ushindani mkubwa kwenye programu walizoomba awali na waliokuwa na dosari kwenye taarifa zao, Vyuo vilitoa fursa ya kuwasilisha maombi Awamu ya Pili. Lengo likiwa kuwawezesha wanafunzi hao kuomba upya kulingana na sifa zao na programu ambazo zilikuwa bado zina nafasi.

ii) Udahili Awamu ya Pili

Mheshimiwa Spika, maombi ya awamu ya pili yalipokelewa kuanzia tarehe **4 hadi 10 Oktoba 2017**. Pamoja na kwamba Awamu ya Pili ililenga waombaji waliokosa udahili, baadhi ya waliokuwa tayari wameidhinishwa katika Awamu ya Kwanza waliamua kuomba tena na kuchagua ama programu nyingine au vyuo vingine tofauti na walizoidhinishwa. Baada ya uhakiki wa TCU katika awamu

hii, jumla ya waombaji **19,488** (wanaume 11,791 na wanawake 7,697) waliidhinishwa kuwa na sifa za kujiunga na masomo ya Elimu ya Juu. Hata hivyo waombaji **9,252** (kati ya 56,319) walikuwa wamechaguliwa zaidi ya Chuo kimoja.

iii) Udahili Awamu ya Tatu

Awamu ya Tatu ilifunguliwa kuanzia tarehe **16 hadi 22 Oktoba 2017** ili kutoa nafasi ya mwisho kwa wanafunzi waliokosa Vyuo na ambao walikuwa bado hawajathibitisha watajiunga na Vyuo vipi waweze kufanya hivyo. Baada ya uhakiki katika Awamu hii jumla ya waombaji **7,418** (wanaume 4,669 na wanawake 2,749) waliidhinishwa kujiunga na vyuo. Idadi hiyo inafanya jumla ya waombaji wote waliidhinishwa na TCU kujiunga katika vyuo mbalimbali nchini hadi kukamilika kwa Awamu ya Tatu kufikia **63,737** (wanaume 38,779 wanawake 24,958). Hata hivyo waombaji **28,466** (wanaume 17,035 na wanawake 11,431) kati yao walikuwa wamechaguliwa zaidi ya chuo kimoja.

Mheshimiwa Spika, TCU ilibaini kuwa baadhi ya waombaji ambao tayari walikuwa wamekwisha pata vyuo katika Awamu ya Kwanza na ya Pili bado waliendelea kuomba tena katika awamu hii ya Tatu. Kwa kuzingatia kuwa vyuo vilikuwa vinafunguliwa kuanzia tarehe 30/10/2017, TCU iliwatangazia wanafunzi ambao walikuwa hawajathibitisha vyuo watakavyojiunga wachague chuo ambacho wanapenda kujiunga na waende kuripoti moja kwa moja. Aidha, TCU iliviagiza vyuo kutoa taarifa kamili ya udahili baada ya zoezi la usajili vyuoni kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha baadhi ya wanafunzi kuendelea kubadilisha programu au vyuo wanavyochagua imekuwa ni changamoto kubwa ambayo imefanya dhamira ya Serikali kupanga mikopo kwa wanafunzi ambao wamethibitisha chuo watakachoenda kuwa ngumu kutekelezeka. Hii ni kwa kuzingatia kuwa hata baada ya kuthibitisha katika awamu ya kwanza ya udahili na kupangiwa mikopo, waliendelea kubadilisha vyuo kwenye awamu zinazofuata.

3.0 Utoaji Mikopo kwa Mwaka 2017/2018

Mheshimiwa Spika Katika mwaka wa fedha 2017/18, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imepanga kutumia **Shilingi Bilioni 427.54** kugharamia mikopo kwa ajili ya wanafunzi wenye uhitaji na waliodahiliwa na Vyuo vya elimu ya juu hapa nchini. Mikopo hii ni kwa ajili ya wanafunzi **122,623**, ambapo wanafunzi **30,000** ni wa mwaka wa kwanza na wanafunzi **92,623** ni wanaoendelea na masomo. Katika robo ya kwanza ya mwaka huu wa masomo, Wizara imepokea **Shilingi Bilioni 147.06** kwa ajili ya ada za wanafunzi na kwa ajili ya kugharamia chakula, malazi, vitabu, viandikia na mahitaji maalumu ya masomo. Fedha hizo zilipokelewa tarehe 09/10/2017.

3.1 Mfumo wa Utoaji Mikopo

Utoaji wa mikopo umezingatia vigezo vilivyowekwa ambavyo ni pamoja na Ulemavu, Uyatima na Uhitaji hasa katika programu za kipaumbele. Upangaji wa mikopo umekuwa ukifanyika kwa awamu kwa kuzingatia namna ambavyo TCU ilikuwa ikiidhinisha majina ya wanafunzi wenye sifa za kudahiliwa na ambao walikuwa wamethibitisha vyuo watakavyojiunga. Hivyo, utoaji mikopo ulifanyika kama ifuatavyo.

Mchanganuo wa Wanafunzi wa Mwaka wa Kwanza Waliopangiwa Mikopo

Tarehe	Batch Namba	Idadi ya Wanafunzi	Kiasi cha Fedha (TZS bilioni)
17/10/2017	Batch Namba 1	10,196	34.6
25/10/2017	Batch Namba 2	11,481	37.6
04/11/2017	Batch Namba 3	7,901	24.3
	Jumla	29,578	96.5

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe **7 Novemba, 2017** jumla ya wanafunzi **29,578** wa mwaka wa kwanza waliokuwa wamekidhi vigezo walikuwa wamepangiwa mikopo. Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inaendelea

kupokea malalamiko ya waliokosa mikopo. Imebainika kuwa, wapo baadhi ya wanafunzi wenye sifa za kupata mikopo lakini hawakuwa wamepangiwa mikopo kwa sababu ya mapungufu katika maombi yao kama vile kutowasilisha vithibitisho muhimu. Bodi ya Mikopo itaendelea kupokea nyaraka zao na kuzihakiki kabla ya kufanya maamuzi.

3.2 Changamoto zilizojitokeza katika Utoaji wa Mikopo

Mheshimiwa Spika, katika utoaji wa mikopo kwa mwaka 2017/2018, Bodi ya Mikopo imekumbana na changamoto zifuatazo:

(i) Baadhi ya waombaji kutozingatia mwongozo na maelekezo ya uombaji mikopo, na hivyo kutoambatisha nyaraka muhimu zinazothibitisha uhitaji wao;

(ii) Baadhi ya wanafunzi waliopangiwa mikopo kuamua kuripoti kwenye vyuo tofauti na walivyothibitisha udahili awali. Hatua hii imesababisha mikopo yao kulipwa kwenye vyuo tofauti na waliporipoti; na

(iii) dhana kuwa mikopo ya elimu ya juu ni kwa ajili ya wanafunzi wote na hivyo hata wanafunzi wasio na uhitaji kutaka wapate mikopo.

3.3 Hatua zinazochukuliwa kukabiliana na Changamoto zilizojitokeza

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia changamoto zilizojitokeza, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu imechukua hatua zifuatazo:

i) Kupokea **taarifa na nyaraka za ziada**, na kusahihisha taarifa za maombi kutoka kwa wanafunzi wahitaji walioshindwa kukamilisha taarifa husika wakati wa kipindi cha maombi. Mara tu taarifa na nyaraka zinapowasilishwa, maombi ya wanafunzi husika yanapitiwa na kupangiwa mikopo kwa wale wenye sifa stahiki.

ii) Kukamilisha utaratibu wa kufungua dirisha la rufaa ili baadhi ya wanafunzi watakaokuwa hawajapangiwa mikopo kufikia tarehe **10-11-2017** waweze kuwasilisha rufaa zao ili wale watakaofanikiwa kwenye rufaa wapangiwe mikopo kabla ya tarehe **30-11-2017**

iii) Kupokea taarifa za usajili za wanafunzi wenye mikopo ili wale ambao mikopo iko vyuo tofauti ihamishiwe kwenye vyuo walivyoripoti.

3.4 Hatma ya Wanafunzi walioripoti Vyuo Tofauti na mikopo yao ilipo

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa baadhi ya wanafunzi waliendelea kuomba upya vyuo na programu hata baada ya kuwa wamethibitishwa na TCU, wapo wanafunzi ambao wameripoti kwenye vyuo ambavyo ni tofauti na mahali ambapo fedha zao za mikopo zimepelekwa. Wanufaika wote wa aina hiyo, mikopo yao itahamishiwa kwenye vyuo walivyodahiliwa mara baada ya kupokea uthibitisho kutoka katika vyuo vilivyowapokea. Hivyo wanafunzi husika wanaelekezwa kukamilisha usajili kwenye vyuo waliko sasa ili kuwezesha taratibu za kuhamisha mikopo yao kukamilika mara moja.

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, Serikali inaona kuwa mfumo uliotumika wa udahili ambapo wanafunzi wamechagua wenyewe vyuo na programu wanazozitaka ni mzuri kwa sababu unawawezesha kutimiza ndoto zao kwa kusoma kozi wanazozitaka. Hivyo Serikali itaendelea kutumia mfumo huo kwa maslahi mapana ya vijana wetu. Aidha, mfumo huu unatoa uwazi zaidi (transparency) wa namna wanafunzi wanavyochagua Vyuo wanavyovitaka tofauti na awali ambapo maombi yao yalikuwa yanafanyika kupitia TCU.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itahakikisha kuwa mfumo wa uchambuzi wa taarifa za wanafunzi unaimarishwa ili kuwa na uwazi zaidi

hasa kwa wanafunzi waliochaguliwa chuo au programu zaidi ya moja. Ni muhimu wanapofanya uamuzi wao wa mwisho kuhusu programu watakayoisoma, TCU ipokee taarifa hizo moja kwa moja badala ya kusubiri ziwasilishwe na vyo husika.

Mheshimiwa Spika, kwa wanafunzi ambao bado hawajakamilisha taratibu za usajili Vyuoni, Serikali inawaelekeza wafanye hivyo mara moja. Hii itawawezesha wanafunzi wanufaika wa mikopo, kupata fedha zao ambazo tayari zimekwishatumwa Vyuoni. Pia nitumie fursa hii kuwataka wanafunzi wanaoendelea na masomo kuhakikisha wanakamilisha taratibu za kuripoti Vyuoni ili waweze kupata fedha zao za mikopo ambazo pia zimeshatumwa Vyuoni.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Martha Mlata pia alizungumzia kitendo cha wanafunzi kutakiwa walipe fedha za usajili kabla ya kupewa mkopo. Jambo hili hata wewe Mheshimiwa Spika ulilizungumza kwa msisitizo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshawaagiza Wakuu wote wa Vyu Vya Elimu ya Juu kuacha urasimu katika utoaji wa fedha kwa wanufaika wa mikopo, ambao wana makubaliano na Serikali, na mwisho wa siku watapaswa kuzirejesha fedha hizo. Hivyo, Vyu vinapaswa kuwasajili wanafunzi wote kwa kuzingatia taratibu zilizopo na mazingira halisi yanayojitokeza.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine naviagiza Vyu Vyote vya Elimu ya Juu nchini, kuondoa urasimu katika kuwasajili wanafunzi vyuoni. Inasikitisha sana kuona kuwa baadhi ya Vyu vinadiriki hata kuwakataa wanafunzi waliowadahili wao wenyewe, au vinawalazimisha wachukue programu tofauti na walizokuwa wamechaguliwa awali na vyo husika. Jambo hili halikubaliki hata kidogo na linaleta shaka kuhusu uadilifu (Integrity) Vyu Husika. Hivyo, naiagiza TCU na Kurugenzi ya Elimu ya Juu ya Wizara yangu, kufuatilia kwa karibu mambo yote yanayoendelea vyuoni wakati wanafunzi wanaripoti na kubainisha wote wanaokiuka taratibu na kuwanyima wanafunzi haki yao ya kusoma programu

wanazozitaka. Serikali haitasita kuchukua hatua kali, kwa Vyuo vyote vitakavyoleta usumbufu usio wa lazima kwa wanafunzi, na kuwafanya wapoteze muda ambao wanapaswa kuutumia kwa masomo.

Mheshimiwa Spika, ninapohitimisha taarifa yangu, sina budi kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais wetu wa awamu ya tano, Dkt John Pombe Joseph Magufuli kwa Uongozi wake uliotukuka na kwa kuwajali watanzania wote ikiwa ni pamoja na wanafunzi wa Elimu ya Juu. Haijawahi kabisa kutokea, fedha kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu zikatolewa mwezi mzima kabla ya vyuo kufunguliwa. Hakika Mheshimiwa Rais Dkt John Pombe Joseph Magufuli, anawatendea haki watanzania ambao ndiyo walimpa ridhaa ya kuongoza nchi yetu. Na kwa sababu hiyo, Mheshimiwa Spika, Wizara yangu haitakuwa na huruma na Chuo ambacho kitachelewesha malipo kwa wanafunzi wanufaika wa mikopo. Hatuwezi kuruhusu mtu yoyote, au Chuo chochote, **iwe ni cha Umma, au cha Binafsi**, kuhujumu kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Rais wetu Mpendwa wa awamu ya Tano. Fedha za mikopo tayari zimeshatumwa vyuoni. Hivyo, Wakuu wa Vyuo wanaagizwa kuhakikisha kuwa, wanafunzi wote wanufaika wa mikopo wanapatiwa fedha zao mara moja.

MHESHIMIWA SPIKA NAOMBA KUWASILISHA

SPIKA: Tunashukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Ndalichako kwa Kauli hiyo ya Serikali. Kama mnavyofahamu Waheshimiwa Wabunge Kauli za Serikali huwa hatuzijadili, kwa hiyo, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri.

Msisitizo tu hapa ni kwamba kama ulivyoeleza hapo umeeleza vizuri sana katika kumaliza, umeeleza vizuri sana. Wako wanafunzi, acha wale wanaoonekana vyuoni ambao hata hawajaenda vyuoni kwa sababu utaratibu uliokuwepo ni kwamba unapoenda chuoni lazima ulipe kwanza halafu uwe *registered* ndio upate mkopo. Kwa hiyo, mtu hawezi kufunga safari, hata kama ana mkopo kwa sababu hana

hela za kulipa. Kwa hiyo, tunashukuru kwa maelezo uliyotoa hapa kwamba, sasa hao walioko huko Tanzania nzima, wanafunzi, nendeni vyuoni sasa mkasome na mkikwama Waziri yuko hapa na Bunge liko hapa, tujulisheni ni chuo gani hicho. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

KAMATI YA MIPANGO

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mchangiaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Peter Serukamba.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru umenipa nafasi nichangie mpango huu. Nimekuja na mipango mitatu, nimekuja na Mpango wa mwaka 2016/2017; 2017/2018 na 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na Deni la Taifa. Kwenye Mpango wa 2016/2017 tuliambiwa ilipofika Oktoba, 2015, Deni la Taifa lilikuwa dola bilioni 19 ikilinganishwa na dola bilioni 18 za mwezi Oktoba, 2014. Tulipokuja Mpango 2017/2018, tukaambiwa Deni la Taifa limekua dola bilioni 18, ongezeko la asilimia 9.76. Sasa mwaka uliopita ilikuwa bilioni 19, mwaka unaofuata tunaambiwa ni bilioni 18, lakini kuna ongezeko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawakuishia hapo, wanasema ongezeko hili wanalinganisha na dola bilioni 16

za kipindi cha 2015. Kwenye mpango huu wa mwanzo wanasema Oktoba ilikuwa bilioni 19, kwenye mpango huu wa pili wanasema Oktoba ilikuwa bilioni 16. Sasa kwenye mpango huu mpya wanasema Deni la Taifa limefika bilioni 26 ukilinganisha na Dola bilioni 22 za mwaka 2016 Juni, lakini kwenye ripoti ya Juni tunaambiwa dola bilioni 19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, moja ya tatizo tunalo hapa ni *data* hizi zinazoletwa na Wizara ya Fedha. *Data* ni za kwao haiwezekani tukawa na *fatal mistakes* za zaidi ya Dola bilioni tatu, jamani hatusomi *documents* hizi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini ninachotaka kusema, ukiangalia mipango yote mitatu kwa kweli, ni *copy and paste*. Ukipitia yote wamebadilisha *language*, kinachosemwa ni kile kile. Kwa hiyo, hapa tunapanga, lakini ni kwa sababu, ni Katiba lazima tupange, yanayokwenda kufanyika wao wanajua, Bunge lako haliyajui. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema deni la Taifa linapanda. Sasa hivi linapanda kwa triloni nne kwa mwaka kulingana na ripoti za *BOT*. Maana yake ni nini? Maana yake tumeamua, kama Serikali kwamba, kila kitu kinafanywa na Serikali, hatuwezi kuendelea! Halipo Taifa duniani ambalo kila kitu wanajenga kwa fedha zao. Kwangu hata ukikopa ni fedha zako sina shida, ukikopa bado ni fedha zako. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe shahidi tumekwenda Moscow uwanja wa *Moscow International* unajengwa na mtu binafsi. Hivi humu ndani tunasema tutafanya *PPP*, ukitafuta miradi ya *PPP* haipo, Serikali hii haiamini katika *private sector*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Bunge hili tukubaliane Waziri wa Fedha atuambie Serikali hii haikubaliani na *private sector* kwa sababu mipango yake Mheshimiwa Waziri mwanzo mpaka mwisho haongelei *private sector*. Kama tumerudi kwenye ujamaa tuambiane wote tujue, lakini

haiwezekani tunaimba ujamaa halafu tunataka matokeo ya Kibepari, haiwezekani! Hakuna katikati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, soma mpango huu hakuna *production*. Hatuongelei kukuza tija, angalia kwenye kilimo, angalia mazao yote ya kilimo hakuna anayeongelea kukuza tija, maana nilitarajia wangesema mwaka huu tumezalisha tani fulani za mahindi, mwaka kesho ni tani fulani za mahindi, hakuna! Pamba hakuna, kahawa hakuna, tumbaku hakuna, korosho hakuna, sasa tunapanga nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunapanga vizuri sana, lakini mwisho wa siku ukiangalia mpango uliopita yale yale yamesemwa. Huku kwenye mipango yote wanasema wataweka fedha *TIB*, fedha hizo zisaidie ku-*leverage* kwenye miradi, toka wameanza kusema hawajaweka senti tano *TIB*. Naomba watusaidie mambo ambayo wanajua hawawezi kuyafanya wasiyaandike *unless* wanaamini Bunge halisomi *documents* hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda humu ndani utaona kabisa kwamba, kwa mfano leo tunaongelea bei ya mahindi. Naomba nikwambie bei ya mahindi kinachofanya bei imeshuka watu hawataki kusema, Zambia wameanzisha *Commercial Farming*, wamelima mahindi mengi sana sasa yanauzwa mpaka Somalia, kwa vyovyote hatuwezi ku-*compete* kwa sababu wao wanaongeza *production*, hatuongelei *production*, sisi tunahangaika kubanakubana, sasa mmegeuza ni uchumi wa kubana tu, leo tunaleta sheria hapa ya kubana! Hakuna anayeongelea kupanua! Hakuna. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukaanzisha kiwanda cha pamba una marobota 240,000 kwa mwaka. Bangladesh kiwanda kimoja kinatumia marobota milioni tano, leo tunaongelea viwanda vya pamba kwa marobota 240,000, tunamdanganya nani hapa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwonea huruma sana Mheshimiwa Rais anahangaika, lakini wenzake

hawamwambii ukweli, mtanisamehe. Leo Rais anakwenda kuwaambia viwanda ndio vizalishe sukari, lakini tumesema hapa siku zote hakuna aliyetuelewa kwenye hili Bunge, lakini kwa sababu Rais amesema viwanda vitazalisha sasa.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, twende kwenye *records* tumesema, waongezeeni maeneo walime. Ilovo waliomba maeneo wakanyimwa, Ilovo wameenda Zambia leo ni *number two* kwa *sugar production in Africa*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ardhi tunayo ni *over regulations* ni *over regulations*. Humu ndani Waziri anaongelea kodi tu, haongelei kukuza biashara, anaongelea kukusanya kodi peke yake, tunakusanya kodi kwa nani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mabenki yanakufa, mabenki yote yana-*record less profit* hata mabenki makubwa. Uchumi unaofanya vizuri unaangalia mambo haya mawili, *performance ya banking industry* na *performance ya stock exchange*. Go to Dar es Salaam turn over ya *Stock Exchange* Dar-es-Salaam imeshuka kutoka bilioni 20 mpaka bilioni mbili na *no one is talking about 85 percent*, Waziri wa Fedha hasemi wala sidhani kama ana *interest* na sioni yeyote mwenye *interest* na hili jambo, ni nini hii? Jamani hii nchi ni yetu wote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaombeni, haiwezekani viwanja vya ndege tujenge kwa pesa, reli kwa pesa zetu, umeme kwa pesa zetu, barabara kwa pesa zetu, hivi sisi ni nani? Dunia yote imeenda kwenye *private sector, the whole world!* China kuna *toll road*, Malaysia kuna *toll road*, kokote unakokwenda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni mambo mawili, moja; tunaleta hapa sheria ambayo humu ndani hawajasema ya kuleta *NASACO*, unajua kwa sababu gani, tunaongelea Tanzania tuna-*manage* ma-*container* 600,000 Singapore wana-*manage* ma-*container* milioni 34. Badala

ya kuongelea kuongeza mzigo, tuongeze ma-*container* yatoke laki sita yaende milioni nne hadi milioni tano, tunafikiria ku-*regulate* hayo, kulinda hizo hizo laki sita zetu, ni nini hii? Hakuna anayewaza kuongeza biashara, kuongeza *production*, hakuna! Soma mwanzo mpaka mwisho hatuongelei kukuza biashara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukienda kwenye mabenki kila kitu kimeshuka, *everything*. Naomba nikupe *data* mbili au tatu. *Personal landing* mwaka 2015 ilikuwa asilimia 25.5, leo ni asilimia nane. *Trade* 2015 ilifika asilimia 24.6 leo ni asilimia tisa. *Manufacturing it was 30 percent*, leo ni asilimia tatu. Hakuna anayesema, tunaona mambo ni mazuri, ukisema tutaanza kupewa majina. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo hayako sahihi kwa sababu moja tu, ukiangalia sababu yetu ni moja tu, mpango wetu wa mwaka huu ndiyo wa mwaka jana, ndiyo wa mwaka juzi na ndiyo wa mwaka unaokuja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Bunge lako tuamue, tuiombe Serikali iseme sasa inataka ujamaa twende kwenye ujamaa *per se*, kama ni ubepari au uchumi wa soko tuende kwenye uchumi wa soko *per se*, *short of that* ukivichanganya hatuwezi kwenda kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (Makofi)

MWENYEKITI: Ni kengele ya kwanza, malizia.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, nataka kusemea suala la Kigoma, *REA*. Alisema jana Mheshimiwa Obama, kinachoendelea *REA* leo kwa watu wa Kigoma ni dhambi. Kigoma tumepata mkandarasi amepewa kazi, ni Kigoma na Katavi, anataka kuanza *CRB* inakuja inasema huyu hafai. Hivi *CRB* Miko yaote hamkuona umuhimu wa kuangalia *procurement*, mnaangalia kwa ajili ya Mkoa mmoja na kwenye Sheria ya *Procurement CRB* inakujaje? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu tunazijua, aliyekuwa anataka kazi ya Kigoma na Katavi ndiye Mwenyekiti wa *CRB*, ni *conflict of interest* na Mawaziri leo, Waziri Kamani hawezi kuamua ana kigugumizi, Waziri Mbarawa hawezi kuamua ana kigugumizi kwa sababu wote tunazijua. Watu wa Kigoma mnatuweka wapi, kwani sisi siyo Watanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *unfortunate*, hivi sisi ni nani? Nataka kusema suala la *REA* na suala la Kigoma kwenye *REA III* naombeni mfanye maamuzi. Kama suala labda kumpa huyo ambaye najua ni mpendwa ambaye yuko *CRB*, mpeni tufanye kazi, yule maskini mwenzetu ambaye alifanya *REA II* leo hamwoni wa maana mnyang'anyeni basi mpeni mnayemtaka ili twende watu wa Kigoma wasipate hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, lakini mipango yetu kwa kweli ni ya mwaka jana ndiyo ya mwaka juzi. Sielewi maana yake ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Peter Serukamba. Tunaendelea na uchangiaji, lakini kabla hatujaendelea Waheshimiwa Wabunge nikwambieni Katiba iliweka utaratibu kwamba mipango ya nchi itapita hapa ninyi muijadili kwanza, hilo halikuwekwa hivyo kwa bahati mbaya, iliwekwa hivyo ili ninyi msemi kwa niaba ya wananchi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, katika mambo ya msingi kama haya fungukeni ili wasikie, usijifungefungu hapo ooh, mimi CCM, mimi, CCM ndiyo haitaki mipango mibovu, kabisa. Kwa hiyo, ni wakati wenu wa kusema tumsaidie Waziri, tuisaidie Serikali ili tusonge mbele. Hivyo, unapoomba nafasi ya kusema hapa uwe umejiandaa, siyo ile tu unaunga mkono, unafanya hivi, unakaa chini. *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ally Saleh.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa fursa hii na nitaitumia vizuri, *Insha-Allah*. Nataka nianze kwa *premises* mbili, kwanza ni ile ambayo umeizungumza sasa hivi kwamba, mara nyingi ukichangia katika hali ya kukosoa unaonekana kana kwamba, unakosa uzalendo hivi. Kana kwamba, wewe unatoka kwenye sayari ya *Mars* umekuja hapa na huna haki ya kusemea. Ndiyo maana Msemaji wa mwisho akasema inafika mpaka unapewa majina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *premises* ya pili ninayotaka nisemee ni Serikali kuwa *very defensive*. Wakati mwingi Wabunge wakitoa michango mara nyingi utasikia, labda pengine hilo lililosemwa sasa hivi lingekuwa limetoka upande huu kungekuwa na miongozo kama kumi, kumi na tano, lakini pengine imetoka upande ule kuna stahamala kidogo. Naomba Serikali isikilize Wabunge, *listen up*, tusikilizeni mtakuwa na nafasi ya kusema na miongozo haisaidii kitu kwa sababu miongozo *at the end of the day* Watanzania wanatusikiliza na zile hoja zinabaki palepale tusiwakalize watu kwa miongozo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nataka kusema kwamba, kama Watanzania kama Wabunge tuna-*appreciate* ambacho kinafanywa na Serikali, si kweli kwamba, kila kitu hatuoni. Tunaona na tunajua, lakini tuna wajibu wa kusemea. Kwa mfano, tunajua kwamba, kuna *improvement* kubwa ya *doing business in* Tanzania. Tumetoka nafasi ya 144, *according to World Bank* hata juzi tu tumekuja nafasi ya 52, *which is very good* na hiyo ni pongezi kwa Serikali kwa sababu, ina maana kwamba, tunaweza kuvutia watu kuleta mitaji yao kwa sababu *it is easier to make business in* Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tuko *proud* kama Watanzania kwamba, kuna vitu vingi vinafanywa, maendeleo yetu ya kila aina, lakini tunapotofautiana ni kwamba, je, tunapaswa kuyafanya haya yote kwa wakati mmoja? Tunapotofautiana kama alivyosema Msemaji wa mwisho, tunapaswa kutumia *resources* gani katika kuyafanya

haya kwa kipindi hiki? Hiyo ndiyo tofauti yetu kubwa inapokuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kusoma kwenye mtandao kujitayarisha kwa *presentation* hii, sina hakika kama hii ni hakika *statement* ya *World Bank or not* lakini wanasema *projection* yetu wamei-*down* kidogo kutoka 7.1 ya *growth* mpaka 6.6. Kwa hivyo, matarajio ya kukua kwa uchumi hiki kipindi kinachokuja haitokuwa tena 7.1, itakuwa 6.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Waziri hili aje alizungumzie na vitu gani vitafanya hiyo tushuke, wao wamesema hivyo. "*there appears to have been an overall deterioration in business sentiment due to perceived risks resulting from unpredictability of policy actions related to the Government intensified efforts to collect revenue and it is anti-corruption drive.*" Kwa maana hali ambayo Serikali na sera zetu za kukusanya kodi, Serikali na sera zetu za kupigana na rushwa kunaweza kufanya mapato katika mwaka unaokuja yakashuka kutoka 7.1 mpaka 6.6 maana yake nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba tunafanya vitu kwa nia nzuri ya kukusanya kodi, kuondoa rushwa lakini zina *boomerang*. Wale ambao wanajua maana ya *boomerang* ni kwamba kule Australia kuna ubao unachongwa unaurusha uende mbali kama usipotahadhari utarudi tena utakupiga wewe mwenyewe. Kwa hivyo, kuna makosa hapa tunayoyafanya na wenzetu wanaona kwamba makosa haya yanaweza kutu-*cost*. Kama ni suala la kupigana *corruption* na kupigana na suala la *revenue* ambalo kuna mashaka katika ukusanyaji wake, mimi kama Mheshimiwa Ally Saleh ningependa kuongeza haya pia yana athari katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya ni *rule of law*, *political stability*, usalama wa raia na Katiba. Mimi naamini hayo yana *relation* ya moja kwa moja baina ya uchumi na mambo haya ya utulivu wa kisiasa, utawala wa kisheria, usalama wa raia na Katiba yenyewe. Pengine ingekuwa kila

kitu kipo vizuri *theoretically* hayo yote yamekaa sawa pengine *FDI's*, uwekezaji kutoka nje ungekuwa mkubwa zaidi kuliko hali ilivyo hivi sasa, lakini tatizo letu nchi hii tuna tatizo la *denial*, tunakataa kwamba siasa yetu iko sawa hakuna kinachobadilika; raia wetu wako salama hakuna kinachobadilika, lakini vitu vingine vidogo tu, tunaona katika *stock market* za nchi nyingine; suala dogo tu linaweza likashusha *stock market point* tano au sita. Kwa hiyo, haya tusiyadharau nami nitaelezea kwa nini nayasemea hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tunasema tuna utawala mzuri lakini inatokea mtu ambaye ameshutumiwa kwa rushwa, ambaye amesemwa waziwazi kwamba amenunua Madiwani anapandishwa cheo, mtu ambaye ameshtakiwa kwa kesi iko Mahakamani anachaguliwa nafasi kisha Serikali ina-*enter nolle prosequere*. Wasiojua maana ya *nolle* ni kwamba Serikali kwenda Mahakamani kusema hatuendelei na mashtaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unamchagua mtu ambaye unajua kama ana kesi Mahakamani, unampa cheo kisha unakwenda kufuta mashtaka, *what message are you sending? Definitely* wa nje wanaona kumbe nchi hii ina utaratibu mbaya wa kisheria. Katika wakati ambao tunapigana na rushwa Serikali inakwenda ina-*enter nolle* kwa watu kadhaa, msururu wa watu ambao wana mashitaka ya rushwa, wameshaka miaka mitano, sita, saba jela lakini je, *is this a proper timing?* Inaonesha nini katika suala la kwamba nchi hii inapigana na rushwa. Kwa hivyo tuna tatizo katika suala la *rule of law*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo unajiliza Serikali *what has it show* kupigana na rushwa mpaka hivi sasa, kuna kesi gani ya *conviction* ambayo imeonekana kupigana na rushwa ambayo itamfanya mtu wa nje aseme kwamba nchi hii kweli inapigana na rushwa. Katika *doing business* je, mfumo wetu uko mzuri kiasi gani wa kuhakikisha kwamba hakuna rushwa kwa sababu hilo tatizo linalalamikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kuzungumzia ni suala la *political stability*. Hapa Bungeni tumeshuhudia jinsi gani Chama kimoja kilivyogawanywa. Inafika wakati humu ndani hatuwezi kukaa na kushauriana kama Wabunge pamoja kwa sababu CUF imekatwa katikati. Una-*send message* gani kwa wengine huko nje kwamba wewe unaendesha siasa vizuri na unathamini mchango wa Wabunge. Ikiwa kama Wabunge wa CUF hawawezi kushirikiana kwa umoja wao unatarajia *input* gani upande wa CUF ije kwa Serikali ikusaidie? *What do you gain?* (Makofi)

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ally Saleh ukae kidogo tupate taarifa. Taarifa inatoka upande gani?

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, huku.

MWENYEKITI: Ohh! Samahani, Mheshimiwa Maftaha samahani.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Natumia Kanuni ya 68(8) nimpe taarifa mzungumzaji ambaye anajitahidi kupotosha umma kupitia Bunge hili Tukufu pale anaposema kwamba nchi hii imekigawa Chama cha Wananchi (CUF) na ipo vipande viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ninayomba ni kwamba mgawanyiko wa CUF haujafanywa na mtu kutoka nje ya Chama cha CUF isipokuwa ni ubinafsi wa Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF) Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, ndiyo tumefikia hapa tulipo na siyo Chama cha Mapinduzi wala Chama kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba apokee taarifa hiyo. (Makofi)

SPIKA: Taarifa hiyo, wala Bunge hili halihusiki na kugawanya mtu yeyote yule. Mheshimiwa Ally Saleh unaipokea taarifa? *(Makofi)*

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei kabisa taarifa kwa sababu Bunge limehusika na iko siku nilitaka nikueleze juu ya mgawanyiko huu ukaniambia kwamba nikisema utanipeleka Kamati ya Maadili. Kwa hiyo, Bunge limehusika katika hilo, tuache. Haijawahi kutokezea popote pale unaichukua Kamati Kuu nzima ya Chama unapeleka Polisi kwenda kuihoji, tuna-*send message* gani kwa watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chama gani kinaweza kikapelekwa chote Mahakamani wakati chama kina *Principals* wake, lakini unachotaka kufanya ni kuonesha kwamba unataka kuminya watu kujieleza na hilo hali-*hog well* na ujenzi wa uchumi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sasa Mheshimiwa rudi kwenye mpango.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, *no*, haya yote yanahusiana na mpango kwa sababu mpango hautotekelezeka, mikopo haitokuja, riba haitakuwepo na wananchi watakuwa, haya yanahusika na mpango moja kwa moja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Maana yake sijamwona Waziri wa Fedha ameshika hata kalamu toka umeanza, maana yake hujaongelea mambo yake. *(Kicheko)*

MHE. ALLY SALEH ALLY: Usijali, muhimu *message* imefika siyo lazima hata ku-*note* kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi tulimsikia Waziri Mkuu hapa anasema kwamba Serikali hii itafanya suala la Katiba wakati Watanzania watakapomaliza matatizo yao. Kwanza siamini kama tutamaliza matatizo yetu kama Watanzania, shida ya maji, elimu na shida nyingine

zitaendelea kuwepo, lakini katiba ndiyo msingi wa huu mpango.

Mheshimiwa Spika, huwezi kuwa na Katiba ambayo wananchi wake wamegawanyika, mambo yake yanabishaniwa katika nchi halafu ukatarajia utakuwa na mpango mzuri wa kuzalisha lakini matokeo yake ndiyo kama haya ambayo tunayaona hivi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia pia kuhusiana na suala zima la Tanzania kama nchi. Najjuliza kama Mtanzania *what are our best products, what are we marketing, branding* yetu ipo kwenye kitu gani? Kama Mtanzania najjuliza mpaka sasa huwa nachachiwa. Katika *production* tume-*specialize* katika kitu gani ambacho tunaweza tukajivuna katika Afrika Mashariki na katika Afrika tukasema kama Sri Lanka wanauza chai basi *brand* yao ni dunia nzima, kama Israel wanauza vifaa vya umeme basi *brand* yao ni dunia nzima, mimi sioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo basi naona Mpango wakati mwingine ndiyo mwenzetu mmoja alisema pale kwamba ni *copy and paste* ilivyokuja lakini ingekuwa angalau tunaji-*specialize* katika maeneo madogo ambayo yanatusaidia vizuri tungeweza kufanya vizuri sana kuliko ambavyo tupo tupo hivi sasa. *We are master of all* lakini vinginevyo sio vizuri. Kwa hiyo, hatuko vizuri sana, ningependekeza basi tuwe na utaratibu ambapo tuna *major brands* tunazitengeneza ili ziweze kuuzika kama nchi tuweze kumiliki soko la wenzetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *private sector*. Amezungumza msemaji wa mwisho kwamba hawaonekani Serikali kama ina nia ya kuwashirikisha *private sector* kama inavyofaa, hayo ndiyo maoni yangu. Mfano mdogo tu nikitazama kule Zanzibar, pengine Zanzibar ni ndogo lakini unaona *impact* ya Said Salim Bakhresa, amejenga *City* na vitu gani vingine lakini huku upande wa Tanzania Bara na pengine hata Zanzibar kwa kiasi fulani ile kuwavuta wale wateja wa ndani siyo sana kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tumekwenda kukopa nje na tumekopa *commercially Swiss Bank* na kwingine kote kwa maana kwamba mkopo ni mkubwa, lakini tunakwenda kukopa mkopo ambao unatakiwa ulipwe kwa asilimia tisa na tumeacha mkopo ambao pengine ungetaka ulipiwe asilimia moja. Mkopo ambao ungetaka ulipwe kwa muda mrefu zaidi tumekwenda kukopa mikopo ambayo inatakiwa ilipwe kwa muda mfupi zaidi, wakati tungeweza kutumia *resources* za ndani za watu wetu wakaweza ku-*absorb* baadhi ya zile fedha zikabakia ndani na matokeo yake wao wakiwa ni wawekezaji wa ndani ina maana kwamba yale matunda yanabakia ndani zaidi kuliko kwenda kukopa nje matokeo yake matunda yanakwenda nje zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao wote wanaokuja hapa *at the end of the day* ni mabepari ambao kutengeneza faida kwao ndiyo jambo la muhimu kuliko kitu chochote kwa hivyo ni lazima watakuwa na masharti. Ndiyo hao ambao tukikosana nao wanatupeleka Paris au London kwenye Mahakama. Nashauri kwamba tungetazama eneo hilo tukafanya vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *blue economy* ambalo linatajwa kila siku...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ally Saleh hiyo ni ya pili, ahsante sana kwa mchango wako.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Anayefuata hapa ni Seneta Richard Ndassa. Kwa Waheshimiwa Wabunge msiomfahamu Mheshimiwa Ndassa ni Mbunge aliyeingia Bungeni mwaka 1995 na humu Bungeni wamebakia watatu tu, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa William Lukuvi na Mheshimiwa Andrew Chenge akiwa AG wakati huo nafikiri kama sikosei. Kwa hiyo, mnaweza mkaona turn over ya Bunge ilivyo kubwa. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mary Nagu pia.

MWENYEKITI: Na Mama Nagu duh! samahani sana.

WABUNGE FULANI: Mheshimiwa Mbatia pia.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbatia anakuja na kutoka bwana, hiyo haiwezekani, sisi tunasema watu ambao wamekuwepo muda wote. Mheshimiwa Ndassa tafadhali. *(Kicheko)*

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana lakini ni kweli kama ulivyosema kwamba baadhi yetu ni wakongwe kidogo humu ndani. Kwa sababu ya ukongwe wetu nikuombe sana wewe mwenyewe lakini nimwombe pia Waziri Mkuu wetu, Mkuu wa Kambi ya Upinzani na Wabunge wote, nimesikiliza michango kuanzia mwanzo siku ya kwanza mpaka jana, siyo kawaida ya Bunge letu hata siku moja, tunatoka kujadili Mpango tunajadili ukanda. Bunge lako sasa limeshapelekwa lipande basi la ukanda kwamba kanda fulani, Kanda ya Kusini, Kanda ya Kati na Kanda ya Kaskazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tukishatoka kwenye ukanda tunaenda wapi? Tutakuja kwenye ukabila, tukitoka kwenye ukabila tunakuja kwenye rangi na dini zetu. Ningeomba sana Waheshimiwa Wabunge kwa sababu sisi ni wawakilishi wa wananchi na kwa sababu tukisema jambo humu ndani, wananchi wetu wanatusikiliza vizuri, tusifike mahali tukawagawa wananchi wetu kwa maana ya ukanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamesemwa mambo mengi sana kuhusu Rais sijui amefanya nini Kanda ya Ziwa, lakini ukitazama kwa nchi nzima na bahati nzuri Kanda ya Ziwa ni moja ya sehemu ya Tanzania. Rudi uangalie maeneo mbalimbali kwa mfano hata hapa Dodoma, uamuzi mzito alioutoa Mheshimiwa Rais wa kuamua kuhamishia Makao Makuu Dodoma, hakusema kuhamia Mwanza hapana.

Uamuzi mkubwa na mzito wa kuihamishia Serikali Dodoma ni uamuzi mzito, sasa tusije tukafika hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana chonde chonde Waheshimiwa Wabunge! Kwa sababu jana nimeona yale mashambulizi, watu wanatokwa mapovu kwa sababu ya ukanda. Hivi Mwalimu Nyerere ndivyo alivyotuachia maneno hayo? Tukitoka kwenye ukanda tutakwenda kwenye udini na ukabila, hatuwezi kufika. Ili tujenge nchi yetu, Wabunge lazima maneno yetu yanayotoka kwenye vinywa vyetu lazima tuyachuje kabla hatujayatoa. Naomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya mshikamano kama mnakumbuka, mwaka 1979 kwenye vita vya Kagera tulimpiga Idd Amin kwa sababu ya mshikamano na umoja. Mwalimu alitumia maneno matatu, uwezo wa kumpiga tunao, sababu ya kumpiga tunayo na nia ya kumpiga tunayo. Sababu ya umoja ule Watanzania wote Tanzania nzima mwenye kuku, mbuzi, trekta, basi na mwenye lori tukashikamana pamoja ndiyo maana ile vita tukashinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo vita yetu kuu siyo ya Kagera, vita yetu kuu kwa sasa ni ya kiuchumi. Vita ya uchumi tutaishinda kama tutakuwa pamoja tukaachana na mambo ya ukanda, tukawa Watanzania wamoja tukaungana kumuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu, anatuonyesha njia kama alivyotunesha Baba wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba wa Taifa alituunganisha pamoja akasema kwa sababu huyu jamaa ametuchokoza na tunao maadui wengi wa kiuchumi Mheshimiwa Rais wetu Magufuli anatuonesha njia, ni lazima tumuunge mkono sio kwa kumbeza kwa kazi nzuri anazofanya jamani. Niwasihi sana Waheshimiwa Wabunge tumuunge mkono Mheshimiwa Rais, lakini kama Wabunge lazima tuwe wamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba nakujua ni mtu

makini, endapo itatokea mimi Mbunge na mwingine labda akasimama humu ndani na kuzungumzia ukanda, mamlaka unayo ili kulinda heshima ya Bunge na nchi yetu. Tukianza kuzungumzia ukanda tutakwenda mbali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu jirani tu hapa kama mmesikia baada ya uchaguzi kwa sababu ya kabila hili na kabila hili, wanasema wanataka kujitenga kila mtu awe na nchi yake. Tukiruhusu kwa sababu mambo haya huwa yanamea polepole, tunaweza tukaruhusu tukafika huko. Hili ilikuwa ni ombi langu kwako na kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na Wabunge wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye mpango, nitasema kidogo tu. Nimwombe sana Mheshimiwa Dkt. Mpango, Mheshimiwa Rais anazungumzia kuhusu uchumi wa viwanda, yeye na kila mtu anajua. Katika mpango wake humu ndani sijaona sababu za makusudi hasa upande wa umeme, hivi viwanda anavyotaka kuvianzisha anakwenda kuweka ma-*generator* au anaweka nini.

Mheshimiwa Spika, viwanda hivi ili viende na vizalishe lazima viwe na umeme wa kutosha na siyo vinginevyo, vinginevyo labda kama tunataka kupiga *sound, well*, lakini kama tunataka tutoke hapa tulipo, leo tuna *megawatts* 1,437, au 1,400, lakini tunasema *okay, Stiegler's Gorge* mwaka 2021 tunategemea itazalisha *megawatts* 2,100, hivi leo tukijijuliza kwa sababu ya umeme huu tulionao tunataka viwanda vichipuke kwa haraka kwa umeme upi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, lakini achilia mbali viwanda, tumeanzisha *REA III*, ambayo ipo inakwenda Kongwa. Sasa kwa utaratibu huu wa umeme wenye mashaka hata hiyo *REA III* nafikiri itaishia njiani tu. Sasa ni lazima Mheshimiwa Dkt. Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango, kwanza nimwombe, bahati nzuri Waheshimiwa Wabunge wa CCM wanamheshimu sana, lakini ana ka-*arrogance* fulani hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia lugha nyepesi ya kidiplomasia, sasa hiyo *arrogance* hebu ajaribu kuiondoa, kwanza haisaidii Bunge, lakini haisaidii sana Serikali. Kwa sababu naweza nikaja na hoja ya msingi ya kutaka kuisaidia Serikali na nikwenda kwake mara chungu nzima, nikamwambia kuna mwanya hapa tunaweza tukapata pesa, lakini namna ya kumpata utafikiri unataka kumpata nani sijui. Sina uhakika kama hata simu za Waheshimiwa Wabunge huwa anapokea, sina uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni Wabunge wenzake, wote humu ndani, wa upande ule kule na upande huu, sisi ni Wabunge wenzake. Tunataka tuisaidie Serikali kwa sababu yeye ndiyo amekamata mfuko wa pesa. Sasa mfuko wa pesa hawezi kwenda kutafuta pesa peke yako. Sisi ndiyo wasaidizi wa kumsaidia, mipango ambayo tunamshauri na yeye angekuwa na uwezo wa kupokea basi angalau kama siyo asilimia 75 basi hata asilimia 50, basi hata 25. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitabu hiki nimekisoma, Mdogo wangu Peter hapa tumesoma pamoja, unajua wengine hatuna zile lugha kali, tuna lugha za kidiplomasia. Namwomba sana Mheshimiwa Dkt. Mpango wa Mipango, hebu ajitahidi kwanza kusikiliza Kamati ya Bajeti, aisikilize mipango yake, ushauri wao, ajaribu kuusikiliza pamoja na wataalam wake. Kwa sababu ilishafikia mahali wanakwenda kwenye Kamati ya Bajeti, mnakaa mnazungumza, mnaishauri Serikali, lakini hakuna kinachochukuliwa, *as if* Kamati ya Bajeti haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ile maana ya kuwa na Kamati ya Bajeti inakuwa haipo kwa sababu yote tunayoshauri kwenye Kamati ya Bajeti yakichukuliwa sana labda ni mawili. Sasa nini maana ya kuwa na Kamati ya Bajeti ya kuishauri Serikali? Maana yake inakuwa haipo.

Mheshimiwa Spika, sasa nimwombe sana Mheshimiwa Dkt. Mpango wa Mipango, mipango yake ili iende vizuri ni lazima awasikilize Waheshimiwa Wabunge.

Peke yake na Wataalam wake watafika mahali ipo siku watakwama, watatuomba tuwasaidie kuwakwamua lakini tutafika mahali tutasema hapana na tutamwambia Mheshimiwa Spika kwa utaratibu huu hatuwezi kwenda hata siku moja kwa sababu sisi ushauri wetu tunashauri lakini hatusikilizwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umesema vizuri sana wakati Mheshimiwa Peter Serukamba akizungumza hapa, kwamba wasikie. Sasa nafikiri na mimi nimemwambia Mheshimiwa Dkt. Mpango asikie. Wenzake wote wanasikia isipokuwa Dkt. Mpango wa Mipango, hasikii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia tena na ukiona Seneta anasema ameshasikiliza mengi huko nje. Dkt. Mpango wa Mipango yeye siyo msikivu kwa Waheshimiwa Wabunge, ajaribu kubadilika kwa sababu wote tuko kwenye boti moja, tunataka tuifikishe hii boti yetu mahali pema, hakuna mtu hata mmoja anayetaka kutoboa mtumbwi hata mmoja, wote tunakwenda katika mtumbwi mmoja, twende salama salmini ili tuifikishe salama nchi yetu mahali ambapo patakuwa na neema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nisisitize tena umeme, lakini pili suala la ukanda. Baada ya maneno hayo, nikushukuru sana kwa nafasi lakini kama nilivyoshauri na nilivyokuomba, suala la ukanda litatufikisha mahali pabaya sana endapo tutaliendekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Ndassa. Anayefuata ni Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri kabisa kwamba Seneta Ndassa amenifilisi kidogo ni kama vile ameingia kwenye hotuba yangu ya siku ya leo, kwa sababu nami sikupendezwa na mijadala, hususan

ya siku ya jana ambayo ilikiuka kabisa Ibara ya 28 ya Katiba, ambayo inatutaka sisi Waheshimiwa Wabunge, au Watanzania wote kuwa na Utaifa. Pia inakiuka Ibara kadhaa ambazo nitapenda kuzizungumza hapo mbele, lakini nitajaribu kuzungumza kitaalam zaidi ya vile ambavyo Mheshimiwa Mzee Ndassa amezungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana wewe, tarehe 17, mwezi Oktoba, nilipata fursa ya kutembelea *Lenin's Mausoleum*, ni kaburi la Vladimir Lenin, Baba wa Taifa la Kirusi na nilifanya hivyo kwa sababu mimi ni mmoja wa wapenzi sana wa siasa za ujamaa na nimesoma vitabu vyake vingi sana. Nilifanya hivyo pia kukumbuka dhima ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ya Ujamaa na Kujitegemea lakini pia ya kuchapa kazi na kuwaunganisha Watanzania kuwa kitu kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi napenda kusema kwamba Mwalimu Nyerere ni Baba wa Taifa letu kama alivyo Vladimir Lenin ambaye amehifadhiwa pale Moscow Kremlin - *Russia* na anapewa uangalizi mzuri na wananchi wa Kirusi. Pia kama Watanzania napenda kunukuu maneno ya William Shakespeare aliyewahi kusema katika Hamlet moja, mbili mpaka 187; alisema kwamba: *"He was a man take him for all in all, I shall not look upon his like again"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda nimnukuu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa sababu alituunganisha Watanzania bila kujali itikadi zetu pamoja na imani zetu za dini pamoja na ukanda na ukabila. Hayo yote nimeona niyaseme kwa sababu nami sikuridhika sana na mijadala hususan ya siku ya jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtanzania asiyeona kazi nzuri inayofanywa na Rais, Dkt. John Pombe Magufuli huyo ni mgonjwa. Nasema kwa sababu yuko Mwandishi mmoja wa vitabu anaitwa Said Nusi, mwaka 2016 alitoa kitabu chake kinachosema Ujumbe kwa Wagojwa. Said Nusi alisema kwamba Mwenyezi Mungu ameshusha magonjwa kwa wanadamu na ameweka dawa yake katika famasia

za ardhi na akawateua wanadamu kuweza kuwatibu walio wagonjwa kwa kuwapa uwezo yeye mwenyewe japokuwa yeye Mwenyezi Mungu ndiyo anatoa maradhi na yeye mwenyewe ndiyo wa kuyaponywa maradhi hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, uzalendo mkubwa anaoufanya wa kulinda rasilimali za Taifa hauwezi kupimwa na mtu yeyote katika nchi yetu hii na hauwezi kupingwa hata kidogo. Nami binafsi natambua maandiko yaliyowahi kutolewa na Shaaban Robert katika tenzi zake alizowahi kumsifu Siti Binti Saadi, kwa wale wasomaji wa vitabu watawiana na mimi. Itafika wakati Watanzania tutahitaji kuenzi mambo mazuri yanayofanywa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ambaye amekuja kutibu na akipigania rasilimali, kupambana na rushwa, ufisadi na mambo mengine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kikubwa zaidi nimpongeze sana Rais huyu kwa kupambana kuhakikisha kwamba Ibara za tatu na tisa za Katiba ya Ujamaa na Kujitegemea inalindwa katika nchi yetu. Binafsi napenda sana kuamini katika ujamaa na kujitegemea na Tanzania bado tupo katika ujamaa na kujitegemea, hakuna anayeweza kupinga jambo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niseme hili kwa sababu mwandishi wa vitabu Martin Harok aliwahi kusema na kunukuliwa kwamba siasa hizi za ujamaa na kujitegemea ambapo nchi yetu inafuata *command economy* ni moja ya siasa bora kabisa ambazo zinadhamiria kujenga dhamira moja ya Kitaifa yenye kutoa matokeo chanya, kuwa na *National Goals* na *as a results of the National goals often defensive and generally ruthless commitment to a single goal*, ambapo sasa hapa tunaona kuna viwanda, reli *standard gauge* pamoja na suala zima la *Stiegler's Gorge*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya nane ya Katiba inazungumzia kwamba nchi ni ya wananchi na wananchi ndio wenye nchi hii ya Tanzania na Serikali ina mkataba na wananchi na tutapimwa 2020 wakati tunapokwenda tena

kuomba kura kuelezea yale mambo mazuri tuliyoafanya. Naomba ninukuu Ibara ya 9(g) ambayo inazuia Serikali na vyombo vyake vyote vya umma kwamba: “Kwamba Serikali na vyombo vyake vyote vya umma vitatoa nafasi zilizo sawa kwa raia wote, wake kwa waume, bila ya kujali rangi, kabila, dini au hali ya mtu.”

Pia Ibara ya 13(4) pamoja na Ibara ya 13(5) pamoja na Ibara ya 28 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimezuia ubaguzi na mijadala yote yenye dhamira ya kuwatenga au kuwabagua Watanzania kwa kufuata ukanda, ukabila au udini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mijadala hii kwa mujibu wa Ibara ya 28 ya Katiba inayotutaka Watanzania kulinda Utaifa, basi uizuie na iwapo Mheshimiwa Mbunge yeyote atazungumzia mambo haya ya ukanda basi azuliwe na asiruhusiwe kuzungumza mbele ya Bunge lako hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ya jana ilikuwepo mijadala mingi na mizito. Kwanza kabisa ni kuhusu ujenzi wa uwanja wa ndege wa Chato. Binafsi kuna watu ninaowaamini sana ndani ya Bunge lako hili Tukufu, sijawahi kuhoji hata siku moja uwezo wa Mheshimiwa Dkt. Mukasa, namwita Dkt. kwa sababu naamini ni mtu mwenye uwezo mkubwa, lakini sijawahi kuhoji uwezo wa ndugu yangu Mheshimiwa Innocent Bashungwa kwa sababu naamini ni watu wenye uwezo mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo lazima asimame mtu wa Kanda ya Ziwa kutetea uwanja wa ndege wa Chato, wananchi wa Jimbo la Rufiji tunaweza tukasimama na tukatetea vema kwa sababu maandiko yanasema *a good defender is the one who knows how to defend*. Wanasheria tunaamini kabisa kwamba Mwanasheria bora ni yule anayejua wapi pa kuitafuta ile sheria, *a good Lawyer is the one who knows where to find the law*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niliseme hii kwa

sababu ukisoma Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ukurasa wa 55 mpaka 58 unazungumzia ujenzi wa viwanja vipya vya ndege, pia kuboresha viwanja tulivyonavyo. Hii ni Sera na Ilani ya Chama cha Mapinduzi, haihitaji mtu wa Kanda ya Ziwa kuitetea, ni Sera ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo Serikali inaelekeza mambo yake kutokana na Ilani ya Chama cha Mapinduzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanja vinavyojengwa ni vingi, siyo kiwanja cha Chato peke yake, tunacho Kiwanja cha Kigoma ambacho kitajengwa, kuna Kiwaja cha Mafia ambacho kitajengwa, kipo kiwanja cha Mtwara ambacho kitajengwa. Hii ni kwa mujibu wa Ilani lakini pia ni kwa mujibu wa mpango ambao umewasilishwa na Mheshimiwa Waziri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna ujenzi wa reli, ujenzi huu unakwenda kusaidia uchumi kwa sababu dhamira ya Chama cha Mapinduzi ni kunyanyua njia kuu za uchumi ili kuwafanya Watanzania waweze kutoka kwenye uchumi wa kawaida na kwenda kwenye uchumi wa kati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Serikali kwa mchakato wa ujenzi wa Bwawa la *Stiegler's Gorge*, hii ni fikra ya Mwalimu mwaka 1956 Mwalimu Nyerere alidhamiria kwamba baada ya uhuru atajenga Bwawa la *Stiegler's Gorge* ili kuweza kusaidia nchi yetu kuweza kupata umeme wa kutosha na kuweza kuuza nje ya nchi. Niwapongeze sana wananchi wa Jimbo la Rufiji, hususan wa Kata ya Mwaseni ambao wamelitunza bwawa hili kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2015 muda kama huu nilisimama mbele ya Bunge lako Tukufu na nikahoji ni kwa nini Wilaya yetu ya Rufiji, Kilwa pamoja na Kibiti tunakosa umeme kwa siku tunapata umeme kwa saa nne, wakati tunayo *Stiegler's Gorge*. Mwaka 2016 nilihoji pia ndani ya Bunge lako hili Tukufu ni kwa nini nchi hii tunauza umeme ghali wakati tunayo *Stiegler's Gorge* ambayo tunaweza kuzalisha umeme na tukasambaza nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunategemea kujenga reli ambayo inakwenda kutumia umeme, lakini pia tuna viwanda ambavyo vinajengwa kila siku. Nimpongeze ndugu yangu, Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo kwa kuzindua mchakato wa ujenzi wa viwanda, viwanda hivi vitahitaji umeme na umeme huu ni wa *Stiegler's*.

Mheshimiwa Spika, ninachoiomba Wizara ya Nishati ni kuzingatia umeme huu wa *Stiegler's Gorge* uweze kuwanufaisha pia na wananchi wa Rufiji. Nimwombe Waziri wa Nishati atakaposimama hapa aseme, baada ya ujenzi wa *Stiegler's Gorge* mchakato mzima upitie katika Wilaya yetu ya Rufiji ili Kata ya Mwaseni iweze kunufaika, wananchi wa Mloka na maeneo mengine waweze kunufaika, wananchi wa Kata ya Kipugila waweze kunufaika, wananchi wa Kata ya Mkongo waweze kunufaika, wananchi wa Kata ya Ngorongo waweze kunufaika na wananchi wa Jimbo zima la Rufiji waweze kunufaika kutokana na mradi huu mkubwa wa umeme kwa sababu wananchi wa Rufiji ndio waliolitunza bwawa hili toka mwaka 1956 mpaka leo hii. Haya ni maneno ambayo nimeyazungumza kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miundombinu natambua dhamira ya Serikali ya kujenga miundombinu mbalimbali ili kuweza kuboresha njia kuu za uchumi, Rais wa Jamhuri ya Muungano, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, tarehe 3 Machi, aliwaahidi wananchi wa Tarafa ya Ikwiriri kwamba kabla ya mwaka 2020 atajenga barabara ya Nyamwage kuelekea Utete. Niombe sana, kila Mbunge anatamani kuacha *legacy* atakapoondoka, mwaka 2020 nitakaposimama kuomba kura na mimi nitaacha *legacy* yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Rufiji tunasema, labda pengine hakuna mwingine yeyote zaidi ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli iwapo barabara hii ya Nyamwage kuelekea Utete itajengwa, Makao Makuu ya Halmashauri yetu. Rufiji ilianzishwa wakati wa mkoloni ni Wilaya ya sita wakati huo, lakini hatuna hata nusu kilometa ya barabara ya lami.

Mheshimiwa Spika, tunaamini kabisa Rais wetu akijenga barabara hii ya Nyamwage – Utete aliyoahidi mwenyewe kwamba kabla ya mwaka 2020 barabara hii itakuwa imekamilika, lakini katika mpango sijaliona hili, kama kuna uwezekano walirekebishe ili wananchi wangu wa Jimbo la Rufiji waweze kunufaika na uchumi huu ambao wanachangia kupitia malliasili na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo barabara yetu ya Ikwiriri kuelekea Kata ya Mwaseni, naomba sana, kwa kuwa Serikali inakwenda kujenga bwawa la *Stiegler's Gorge*, hakuna namna tutaepuka kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba Serikali kutokana na makusanyo tunayoyapata, ianze kujenga barabara ya kutoka Nyamwage kueleka Utete ili wananchi waweze kupata barabara yao ya Halmashauri kwa mara ya kwanza toka tumepata uhuru. Pia barabara ya Ikwiriri kuelekea Mwaseni ni barabara muhimu sana, hali kadhalika barabara ya kutoka Bungu kuelekea Nyamisati katika Wilaya ya Kibiti ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Serikali sana kwa kutuletea miradi mingi ya maji. Naipongeza Serikali na nampongeza Waziri wa Maji, baada ya kuteuliwa tu kuwa Waziri alifika Rufiji na kujionea miundombinu mbalimbali ya maji.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Maji ahakikishe kwamba ile miradi anayotuletea ambayo nilimwomba mwenyewe inayokwenda katika Kata za Mbwara, Chumbi, Utete, Mkongo, Ngarambe, Kipugira na nyingine, basi iweze kukamilika kwa wakati ili mwaka 2020 tuweze kutamba kwamba tumeweza kuwafanyia wananchi jambo fulani ambalo litakuwa na manufaa kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo, kilimo kimezungumzwa katika makaratasi, namwomba Mheshimiwa Dkt. Mpango, Rufiji tuna ardhi ya kutosha na wakati fulani tulipewa taarifa na Waziri wa Viwanda kwamba atatujengea kiwanda cha sukari katika Kata za Chumbi, Mbwara pamoja na Muhoro. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, tunatambua wapo wawekezaji mafisadi waliochukua ardhi yetu wananchi wa Rufiji na kuishikilia ili kutafuta wawekezaji wapate cha kwao cha juu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali na nimwombe Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa ukali anaoufanya katika kujenga uchumi wa nchi yetu, anyang'anye ardhi hii mara moja ili tuweze kupata kiwanda hiki cha sukari kwa mara ya kwanza katika nchi yetu na kwa mara ya kwanza katika eneo letu la Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Magufuli, anyang'anye ardhi hii ambayo imechukuliwa na mwekezaji mmoja mfanyabiashara aliyemiliki na hataki kujenga kiwanda, amezuia Serikali kuweza kupata mwekezaji wa kujenga kiwanda hiki, ardhi hii iweze kunyang'anywa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niikumbushe Serikali, Rufiji tuna *square kilometers* 500,000 ambazo ziko ndani ya Bonde la Mto Rufiji. Naiomba sana Serikali kuona namna ya kuboresha kilimo katika maeneo yetu ili wananchi wa Rufiji pia tuweze kunufaika na Serikali yetu na tuseme kwamba tunatembea kifua mbele kwamba Serikali ya Awamu ya Tano sasa imedhamiria kuunyanyua uchumi wa wananchi wa Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee katika elimu. Sote kabisa tunatambua kilichotokea Rufiji na Kibiti kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja tumeshindwa kufanya siasa,

wananchi wameshindwa kushiriki katika kilimo lakini kitu kikubwa ambacho kinatukwamisha ni tatizo kubwa la elimu.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Elimu, kama ambavyo aliweza kutenga fedha za uboreshwaji wa shule za sekondari za Kibiti, Muhoro na sekondari ya Utete namwomba pia aone uwezekano wa kuboresha miundombinu ya shule zetu, hususan shule ya Sekondari ya Ikwiriri pamoja na miundombinu ya shule zetu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua, ukiangalia takwimu tulizonazo leo hii katika maeneo ambayo yameathirika sana na elimu ni eneo la Rufiji, Kibiti, Kisarawe na maeneo mengine ya Pwani. Leo hii tuna watoto zaidi ya 300,000 nchi nzima ambao wanaacha shule bila sababu maalum. Nimwombe Waziri wa Elimu akisimama hapa atuambie mpango mkakati ambao Serikali itakuja nao wa kudhibiti utoro katika shule na kuacha shule mara moja.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Elimu akisimama atuambie Serikali inafanya mchakato gani wa kubaini watoto ambao waliacha shule miaka kumi iliyopita na kuweza kujua wako wapi leo hii. Bila kufanya hivyo, watoto wengi leo hii wanaoacha shule, wanakwenda kujiunga katika vikundi mbalimbali vya kigaidi. Hii inatuletea shida kwa sababu vijana wetu wengi wanapotea na Serikali haielewi wamekwenda wapi.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. (Makofi)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ni wajibu wangu kila wakati kuwakumbusheni sisi wenzenu ni wa siku nyingi kidogo, kidogo Bunge letu mnataka kulishuka viwango. Hapa kinachojadiliwa ni Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa yaani mkianza kutaja vijiji vyenu, kata zenu mimi hata sielewi yaani kijiji hicho na Mpango wa Taifa yaani kina *fit* vipi na hiyo kata yako uko, unafiti vipi kama nchi inataka kwenda wapi inataka kufanya nini, Waziri katuletea nini sisi tunashauri nini kama Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hayo mengine kwenye bajeti kule mtasema, Kitongoji nini hayo mtaeleza kule hapa ni Mpango wa Taifa kama huna la kusema usilete jina hapa sawa jamani nchi yetu ya Tanzania, hapa tulipo na tunapotaka kwenda mwaka 2018/2019 tanamwambiaje Waziri wa Fedha na Mipango. Je, huu Mpango anaotuletea sawa sawa au unahitaji kuboreshwa wapi na kadhalika, tuangalie Taifa zaidi ndo hii mambo ya kanda sijui jimbo, kata, kijiji hiyo haitusaidii sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Mbilinyi, atafuatiwa Mheshimiwa Bashe. *(Makofi)*

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, *za katari chizilekaje chityate za lulubaha. This is between me and you. (Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Ananiambia ya zamani tuyaache. *(Kicheko)*

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kutuhakikishia juzi wakati unafungua tunaanza Bunge ulituhakikishia kuwa tusiwe na wasiwasi safari hii tuko salama tukiwa Dodoma.

Sasa naiomba na *excutive* nao watuhakikishie usalama tunapokuwa kwenye maeneo mengine mbalimbali ya nchi kwa sababu ni uwazi dunia yote sasa inajua Wabunge wa Upinzani na watu wengine wenye mawazo mbadala hawako salama. Sasa hatuwezi kujadili mipango katika mazingira ambayo sio salama, *so please don't shoot me*, natoa ushauri, mawazo maoni yangu kwa Serikali, tubishane

hoja na sio *bullets*, mfano tunazungumzia mipango ya kubana matumizi, lakini ukiangalia Baraza la Mawaziri limeongezeka, Mawaziri wameongezeka Makatibu Wakuu wameongezeka. Viongozi wa kawaida wana ulinzi wa kupita kiasi, Naibu Spika ana walinzi wawili, wasaidizi ambao akisafiri nao nje wote wanalipiwa *business class* zile ni fedha ambazo zinakatwa tiketi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Menyekiti, nakumbuka Mheshimiwa Spika wakati ule ukiwa Naibu Spika nilikuwa nakuona unatembea na Katibu tu na gari moja. Lakini leo hii unakuta Naibu Spika ana *motorcade* ya magari kibao, Bashite ana *motorcade*, ana walinzi kuliko hata Waziri Mkuu. Sasa unajiuliza gharama zote hizi zinazotumuka kwa Bashite ulinzi *motorcade* kuliko Waziri Mkuu, ni majukumu gani aliyopewa ambayo yanalazimika apewe ulinzi wa gharama kiasi hicho?

T A A R I F A

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Wewe tuliza wenge wewe, hebu kaa! (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Taarifa! Mheshimiwa Mbilinyi upokee Taarifa tafadhali,

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Weka *stop watch*.

MWENYEKITI: Dakika zako nazitunza, Mheshimiwa!

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbilinyi ni Mbunge mwezetu sawa, wote tunaongea Kiswahili viongozi wa nchi hii tunawafahamu. Afunguke basi atuambie Bashite ndo nani wengine hatumwelewi. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mbilinyi unapokea taarifa, endelea na kuchangia.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Hiyo sio taarifa hilo ni swali na hiki siyo kipindi cha maswali, kipindi cha maswali kimeshakwisha. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia mipango, lakini mipango bila utaratibu haiwezi kuwa mipango. Sasa watu wanawaka sana tukizungumza kuhusiana *airport* ya Chato, hamna mwenye tatizo na *airport* ya Chato, lakini tatizo ni namna ilivyokuja na bajeti yake na utaratibu wake ndiyo tatizo lililopo. Sasa ukiangalia kama *project* kama hizi inanikumbusha enzi ya Mobutu Sese Seko Kuku Ngbendu Wa Za Banga wa Zaire alikwenda kijijini kwake Gbadolite akajenga Ikulu ya ya vyumba zaidi ya 100. Akaja na *project* ya *airport* ya kimataifa, lakini leo vyote vile kwa sababu vilikuja/vilizuka bila mipango ya nchi vinakaliwa na popo na panya. Kwa sababu ndege gani itaenda kutua Chato Mheshimiwa Rais atakapomaliza muda wake, mnakosa muda wa kwenda Butiama kwa Baba wa Taifa mtaenda Chato? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachozungumza hapa *its not personal* ni *principals*, mipango. Tunajisifu kupanda kwa bei ya korosho zao moja tu ambalo mazingira yake wote tunajua ni kama mazingira yaliyopandisha kahawa enzi za Mrema, Mrema akawa anatafuta *credit* miaka yake yote kwa kupanda bei ya kahawa, kumbe tatizo lilikuwa kwamba kulitokea ugonjwa wa kahawa huko Brazil kahawa ikawa inahitajika. Kwa sababu kama korosho imepanda bei kwa mipango vipi mipango ya kupandisha bei ya kunde, choroko, mbaazi, tunasikia sasa hivi mbaazi bei imekuwa mpaka shilingi 100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama suala ni mipango na mikakati ya kutafuta masoko ya mazao basi tutumie maarifa tulyopandisha bei ya korosho kufika shilingi 4,000 na mbaazi nayo ifike hata shilingi 1,500 au 2,000 ili kuondoa kilio hiki cha wakulima wa mbaazi, tumbaku, choroko na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda sasa hivi tuna zunguka kuzindua barabara, lakini barabara zote ni za Mzee Kikwete, *flyovers* za Mzee Kikwete, Daraja la Kigamboni Mzee Kikwete Awamu ya Tano barabara pekee tunayoijua ya approve ni ile kutoka Mwenge mpaka Morocco ambayo wali-*divert* fedha za sherehe ya uhuru ikaenda kujenga kile kipande cha barabara, lakini barabara zote tunazozindua sasa hivi ni za Mzee Kikwete mwana dipromasia aliyetukuka Mungu ampe maisha marefu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwasihi Mawaziri hasa hawa wapya achene kushindana kwa matamko, mshaurini Rais maana yake kila siku matamko mara tunataka viwanda 100 kila Mkoa halafu ilo jukumu unampa Mkuu wa Mkoa ambaye hata *allowances* zile anazostahili kupelekewa azipolekwi hazitoshi kabisa. *OC* hamna, Halmashauri hamna fedha, leo unamwambia anajukumu la kusimamia ujenzi wa viwanda 100 huu sio upangaji wa mipango, huku ni kudanganyana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe sana Mawaziri wapya hasa vijana *be humble, cool down, show your talent, will recognize and appreciate you*, acheni misifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili suala la makinikia naona hamna anayelizungumza hili ni suala nyeti ambalo kama Taifa tulikuwa tunalifuatilia sana, lakini kuna *dilemma* nyingi sana katika taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tuliambiwa tuna tarajia kupata trilioni 400 *plus* kutoka kwa hawa mabwana waliokuwa wanatuibia kwamba kila Mtanzania angeweza kupata Noah moja na mafuta tungejua sisi wenyewe namna ya kupata, lakini kila mtanzania angeweza kupata noa moja. Lakini baadaye baada ya muda tunaambiwa kwamba wezi wamekubali kulipa bilioni 700 tu kutoka trilioni 400 *plus* na baadaye tunaanza kusikia tena jamaa wamegoma kwamba hawawezi hiyo kutoa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hamna taarifa *we turned to be the wealth laughing stock*, dunia nzima inatucheka *International media* zina tuandika vibaya, zinamwandika vibaya Rais wetu kutokana na vitu kama hivi. Huyu mtu kama msemaji wa Serikali badala ya kukaa kusemea mambo kama haya yeye amekalia tu kufungia magazeti kwa vifungu ambavyo ni *wrong*. Mtu anakuja anafunga gazeti kwa kutumia kifungu namba 54(1) cha sheria mpya ya habari ya mwaka 2016 wakati ile sheria *straight and direct* inasema adhabu ni kifungu au faini kwa mtu *a person*, sio gazeti lakini Msemaji Mkuu wa Serikali anatoka anafungia gazeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anafungia magazeti kwa kifungu ambacho ni *wrong* anafikiri watu ni wajinga, watu wanatafuta sheria hata kwenye mitandao wanaenda wanasoma kile kifungu ndiyo maana wanaharibu sifa ya Mtukufu Rais wa Awamu ya Tano mpaka watu wanamuita dikteta kwa sababu ya watu kama huyu Msemaji wa Serikali kwa sababu udiktekta ni ku-*dictate*, ni kulazimisha, unalazimisha sheria ambayo ahusiani kuchukua hatua ambayo haihusiani *which is very wrong*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni jukumu la hili Bunge sasa kuwaambia hawa Mawaziri mnapokaa kwenye Baraza la Mawaziri muangalie Rais usoni na mumshauri, yule ni binadamu kama nilivyosema alikuwa anakaa kiti cha pale mi nilikuwa nakaa kiti cha pale havipiti hata viti sita/saba kutoka nilipokuwa nakaa. Tulikuwa tunaandikiana nae vinoti humu tukiwa na ishuhari mbalimbali, ninyi mnashindwaje kumshauri kwamba *this is wrong, this right. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu inafika mahali sasa Watanzania hawaamini tena kauli za Serikali inakuwa *flip-flop*, Rais anasema hivi, Waziri anakuja nasema vile matokeo yake mnabaki kuwa *defensive* wakati mlikuwa kwenye *position* ya ku-*offensive*, tulivyoanza anza apa sisi Bunge hili kama Kambi ya Upinzani...

MWENYEKITI: Zimebaki dakika tano, sasa urudi kwenye Mpango sasa.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amekuja hapa Waziri wa Elimu, majukwaani mnasema Rais anaenda vizuri sasa hivi hakuna tena migomo wala maandamano ya wanafunzi, juzi tumeona mgomo, leo Waziri wa Elimu anakuja hapa anapiga longolongo, karatasi nyingi unamaliza miti tu, kutengeneza karatasi unaleta jangwa unamaliza miti, maelezo mengi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ni kwamba watoto wanaangaika mikopo juzi wameandamana na ninyi mlikuwa mnasema kwamba maandamano hakuna, mnatengaje fedha za wanafunzi 30,000 wakati *projection* ni wanafunzi 61,000 wanafunzi 31,000 wote waende wape waende mitaaani wakatukabe hii haiwezekani, kwa hiyo, lazima tuwe *realistic* kwenye mipango yetu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tulivyofika hapa tulivyoanza hili Bunge mambo tukasema mpaka wapinzani ni ukweli tulikuwa tunasema dah, bwana sasa huyu jamaa aliyekuja tutakuwa na hoja gani mnaleka hoja wenyewe Rais hayumo humu ninyi ndo mnatakiwa mje na vitu ambavyo vita-*reflect* uongozi wa Awamu Tano sisi tukose hoja lakini mnaleta hoja wenyewe tukisema mnashindwa kujibu hoja, mnatusubiri tutoke nje ya geti wakati mnaingia kwenye nyumba zetu mtupige *pyuu pyuu, that is wrong, that is very wrong.* *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ulisema tusiulize tena...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbilinyi huo nao ni Mpango pia? *(Kicheko)*

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: ...za kata halafu ukiuliza unawauliza wahusika unawaambia kwamba aah,

mmeanza mambo gani tena ya ku-*shoot*, wanakuambia aah, usijali we haumo, nani yumo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nakushuru sana. (*Kicheko*)

SPIKA: Huu Mpango wa Dkt. Mpango mwaka huu, nilimtaja Mheshimiwa Bashe, anafuatia Mheshimiwa Jesca Kishoa. Mheshimiwa Bashe tafadhali.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri ambao wamebaki kwenye nafasi zao na Mawaziri wapya na Naibu Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais katika mabadiliko ya Baraza la Mawaziri la hivi karibuni, niwatakie kila la kheri katika kutimiza wajibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 wakati tunajadili mpango ndani ya Bunge hili nilimtahadhalisha Waziri wa Mipango nikimwambia kwamba mpango unaouleta hatutofikia *economic growth* ya *seven percent* kwa sababu Mpango huu unaacha sehemu kubwa ya Watanzania nje, sio mpango *inclusive*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 wakati tunajadili Bajeti nilirudia maneno haya na mwaka huu wakati tunajadili Bajeti nilimwambia kuna *conflict* kati *fiscal policy* ambazo Wizara za Fedha inazisimamia na *monetary policy* *these two policies* zinapambana zenyewe na matokeo yake yataonekana. Naomba nitumie takwimu zifuatazo kama alivyosema Ndugu Serukamba uchumi wowote duniani una *mirror* (kioo) na kioo cha uchumi wowote unaokuwa ama unaosinyaa ama unaoshuka moja ni *financial Institution*, mbili ni *trade*, tatu ni *stock exchange*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *personal landing* mwaka 2015 ilikuwa ni 50% *today* ni 8.9 percent. *Trade* ilikuwa ni 24% *this is a landing to trade* ilikuwa 24%, leo ni 9% na maneno haya siyatoe kwingine ni ripoti za *BOT* na *quarterly report* ya

BOT ya inayoishia Juni, lakini taarifa zingine ni mwongozo wa Bajeti alioleta yeye na ni mpango wake alioleta yeye. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *agriculture leo ni negative nine from six percent land capacity* ya mwaka 2015, *manufacturing from thirty percent landing to three percent, transport and communication from twenty four percent landing to negative twenty five, bulding from twenty two to sixteen.* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *our economy it is said* inakua, ukisoma *projection* ni 6.8. Lakini taarifa ya mwisho ya *economic bulletin for the quarter ending June, 2017* imetuambia ni 5.7 sio maneno yangu. *Food inflation lets go categorically its 10.1 percent* sio maneno yangu taarifa ya Septemba ya *BOTHii* hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *why are we facing this, it's not a rocket science.* Waziri wa Fedha ukurasa wa sita wa Mpango unasema *export* naomba iingie kwenye *Hansard* ya Bunge. Nimeangalia taarifa za *monthly* za *BOT* toka mwaka 2011 mpaka Septemba mwaka huu, *for the first time in the history* hamjaweka *performance export and imports, why?* Mnaficha nini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, alisema ndugu Abdulrahman Kinana, wakati anaongea katika *function* ya Kigoda pale *Universty of Dar es Salaam* alisema hivi namnukuu, Katibu Mkuu wa chama chetu; "Jambo muhimu la kiongozi ni kusikiliza watu wake." Viongozi hamna *monopoly right wisdom*, viongozi hawana *monopoly right* ya *trueth*, viongozi hawana *monopoly right* ya wao wako sahihi kila siku. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna jambo muhimu katika kupanga mipango yoyote duniani kama takwimu. Ukurasa wa saba wa *document* ya mapendekezo ya Mpango unaonesha mwenendo wa ukuaji wa Pato la Taifa toka mwaka 2011 hadi 2017, *2011 our growth was 9.1 percent. Today its projected 6.8* lakini *as per this report* ni 5.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ninukuu maneno yafuatayo , ukurasa wa saba unasema; kufikia Juni, 2017 *export* zilikuwa zimeshuka kwa asilimia 29.8. Lakini Waziri anatupa *a counseling statement* kwamba matarajio ni kurejea kwa *exportation*, kuongezeka eti kwasababu tunajenga kukuza viwanda sasa twendeni tukasome hivyo viwanda vya *export*, siyo maneno yangu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mpango Waziri ametaja viwanda, ukurasa wa 26, kiwanda cha kuchenjua madini kulichopo Geita, kusindika nyama Kisivani Shinyanga-*Mitobotobo Farmers Company Limited*, kuzalisha mafuta ya kula, kuchambua pamba, kiwanda cha kuzalisha vifungashio (*Global Packing*), kiwanda cha kuzalisha vinywaji baridi (*Sunny Food Company - Sayona*) hivi ndiyo tuta-*export* kurudisha asilimia 29. Kuzalisha bidhaa za ujenzi; *brother* tumeahidi kuondoa umaskini wa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo maneo yangu mimi na-*quote* maneno ya Waziri wa Mpango. Twendeni ukurasa wa 68 - sekta ya kilimo *look at this*, hii ndiyo sekta imeajiri asilimia 65 mpaka 70 ya wananchi wetu na tafiti zilizofanyika Watanzania zaidi ya asilimia 80 walioko kwenye sekta ya kilimo yaani ile *70 percent, 80 percent* ya hiyo *70 percent* inafanya kazi mbili (*dual*), inalima na inafuga kama siyo ng'ombe, mbuzi, kuku, bata na vitu vya namna hiyo, anafanya *dual, now look at this two things*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mifugo, Serikali imepanga kufanya uhimilishaji, tunahimilisha, kufanya *insemination* ng'ombe 450,000. Lakini tunapanga kuzalisha chakula *hay*. *Hay* ni yale majani ya ng'ombe, tunapanga kuzalisha chakula kwa mwaka hey 445,000 kitakwimu *hay* moja ina uzito wa kilo 25, chakula hiki ukikigawa kwa siku 360 kinalisha ng'ombe 1,600 huku unapanga kuzalisha ng'ombe 400,000 lakini unaandaa mpango wa chakula ng'ombe 1,600. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Wabunge wamejadili suala la kilimo, hakuna sehemu Waziri wa Kilimo ana-*plan*

kuanzisha *price stabilization* ya mazao ya chakula. Leo kuzalisha kilo moja ya mahindi, gharama ya shambani ni shilingi 357, haya siyo maneno yangu, *it is scientifically proved*, halafu huyu mkulima anayetumia shilingi 357 kuzalisha kilo moja ya mahindi bado gharama ya kupeleka *store*, gharama ya kuweka mifuko...*(Makofi)*

MWENYEKITI: Bado dakika tano.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama ya kuweka dawa halafu atakapoweka *store* yake kuna kauli inasemwa hapa walanguzi ndiyo wana mahindi, *this is total misconception ya business principal*. Kote duniani kuna *producer*, kuna *distributor*, kuna *retailer* kwahiyo unataka kuniambia mimi ninayelima Nzega-Nata Mahindi yangu niyabebe, niende nikayauze Nairobi? Kuna *intermediaries and this is the duty of your fiscal mono-policies* kufanya *intermediaries* wafanye biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikupe mfano mwingine, *profitability ya financial institution* imeshuka *over 50 percent*, Waziri ana hoja moja dhaifu sana anaitumia ndani ya mipango. *Money circulation* imepungua kutoka bilioni 222 mpaka bilioni 12 na hoja anayosema ni nini? Matumizi yasiyokuwa ya lazima ya Serikali yamepungua. Sasa najuliza bajeti ya *recurrent* imepungua? Kutoka mwaka 2011, 2012, 2013 imepungua *recurrent budget*? *No, spending ya government* ipo, kwa hiyo nilitarajia kwamba itakuwa *wisely* tutaiona imeleta *positive impact*, lakini hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushauri wangu kwa Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Mpango narudia *this is the third time*, naheshimu your *academic background*, sijawahi ku-*doubt*. Kaka hauwezi kuondoa umaskini wa nchi hii bila kuwekeza kwenye kilimo, *never*. Hauwezi kuleta mapinduzi ya viwanda bila kuwekeza kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima wa nchi hii ndiyo kageuka *punching box* ya nchi hii. Tuna-*control inflation* ya chakula kwa gharama ya mkulima, *how come?* Haiwezekani, hatuwezi kufanikiwa kwa namna hii. Yaani sisi tunadhibiti mfumuko wa bei kwa kumtia umasikini mkulima, aina gani za *economy*hizi? (Makofi/Vigelegele)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikupe mfano mdogo tena aangalie, hatuwezi kuondoka kwenye umaskini kama mawazo ya Wizara ya Fedha hayatakuwa ni *productive oriented* badala ya kuwa *tax base approach*. Angalia Mpango huu unakuwa *financed* namna gani. Waheshimiwa Wabunge tuchukue *document* ya Mpango muusome *how are we going to finance* Mpango. *Page number 29* ya muongozo wa maandalizi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilindie dakika zangu dakika moja tu. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anasema kwamba *how to finance*, anazungumzia kwamba ata-*improve EFD machine*, ataanzisha maabara ya *TRA*, *it is all about tax base approach*. Haumsikii anasema kwamba tutawekeza bilioni moja kwenye kilimo cha mahindi ili tuweze ku-*yield X* hausikii, hauwezi kukamua maziwa ya ng'ombe usiyemlisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *VAT, Pay As You Earn* zimeshuka hazifikii *target* aliyojiwekea kwenye bajeti ya 2017 na hapa anasema kwamba makampuni yamepunguza wafanyakazi an unajua ni kwa nini? Is *not a rocket science*, tulimshauri kwenye Kamati ya Bajeti kwamba unaongeza *exercise duty* kwenye *TBL* utapunguza uwezo wa uzalishaji wa hawa watu, hakisikia! Tumemwambia kwenye Kamati ya Bajeti *I was there*. Tumemwambia Waziri wa fedha unaua viwanda vya *soft drink* kwa ku-*impose 10 percent* eti kwa udhaifu wao *TRA* wa kusimamia sukari inayoingia wameweka asilimia 10 tena *on top* kwa hiyo *Coca cola* akiingiza sukari kwenye nchi hii analipa *25 percent instead of 15 percent*, *what kind of economy is this?*(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge hasa wa chama changu, tumepewa dhamana ya nchi hii na Watanzania, *let not allow mistake* za Waziri Mpango kuharibu nafasi ya kuchanguliwa kwa Rais wetu mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani nikupe mfano mdogo, kampuni zote za vinywaji baridi zilikuja mbele ya Kamati ya Bajeti na sisi tukawaita Wizara ya Fedha, hawana *capacity* ya kwenda kukagua *bonded warehouse*, hawana *capacity* hiyo madhara yake unajua wamefanya nini? Wameamua kuanzisha kodi mpya ya ku-*withold*. Sasa hivi *private sector* inadai *TRA over eight hundred billion shillings* za *returns on tax*, hawalipi...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Wana-*sufocate*, *this is very wrong* na mimi nimalizie samahani...

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Kama Waziri wa Fedha hatobadilika...

MWENYEKITI: Nakushukuru sana.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Hatuwezi kutoka hapa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Bashe, ahsante sana. Ahsante sana nashukuru sana. *(Makofi)*

Nafikiri mnanielewa baada ya kuchangia Mpango sasa badala ya kijiji cha Kongwa kule, ile barabara ya kilometa nanii hii pale, *culvert* la pale, hayo kwenye bajeti huko, Waziri huyu huyu lakini huko mbele hapa tu-*focus* zaidi

kwenye Mpango. Ndiyo maana mnaona mnapochangia *culvert* mnaona Mawaziri wote hawapo maana anaona hata nikikaa pale kuna nini watu wanachangia habari ya *culvert* nini sasa lazima tuchangie Mpango. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Kishoa nilikutaja.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Kwanza kabisa nitoe pongezi kwa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa hotuba nzuri ambayo imegusa maeneo *strategic* kwa ajili ya kulisaidia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongea kwa ufupi sana kwasababu haya yaliyoandikwa kwenye Mpango ambayo tumeelezewa na Mheshimiwa Mpango ni masuala ambayo yamekuwa yakijirudia, kwa hivyo tusipoteze muda kuendelea kurudia mambo ambayo tumekuwa tukiyarudia mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala moja la msingi sana Mheshimiwa Mpango naomba utakapokuja kuhitimisha unisaidie kulijibu nalo ni kuhusu umakini wa uandaaji wa Mpango. Huu Mpango unalenga kutekeleza Dira ya Taifa 2020/2025. Nilichokuwa nakitegemea ni Mpango huu kuonesha una lengo la kutekeleza Dira ya Taifa ya 2020/2025 kwa asilimia ngapi ili ije kuwa rahisi kuhoji.

Mheshimiwa Mpango wewe unajua, Mpango unapokuja kuleta humu Bungeni ni lazima uwe *smart* kwa maana aya lazima uwe *specific, measurable, uwe realistic, uwe attained* na uwe *frame timed*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni Kenya. Kenya wanapokuja kuanda Mpango wanakuwa *very serious*. Unakuta wanaadika kwamba Mpango huu umelenga inapofikia wakati fulani ajira mpya zitazaliwa kwa asilimia kadhaa, hiyo inakuwa inasaidia tunapokuja kurudi humu ndani kuangalia tumefikia wapi na tumetokea wapi, nafikiri hili litakuwa ni tatizo la uhaba wa wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mpango ambao unakuwa wanaleta Bungeni kuwa na mapungufu kama haya ndiyo maana mambo mengi yanakuwa hayaendi sawa sawa, ndiyo maana Taifa hili bado linaendelea kuwa katika mazingira magumu, wananchi wanakuwa wanaishi maisha ya kimasikini, maisha ya mateso, ukata ni mkubwa kweli kweli na hili mnaweza mkalikataa lakini ni kitu ambacho kimekuwa *proved*. Mna mamlaka kubwa ambazo zinahusika na tafiti mbalimbali, mfano, nimeona katika ripoti ya *BOT* Juni, 2017 na Juni, 2015 inaonesha mzunguko wa fedha umeporomoka kutoka asilimia 15 mpaka *negative three percent* ambacho hiki ni kiwango kikubwa cha *run rate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *BOT* pia wanaonesha kwamba mikopo isiyolipika yaani *non-performing loans* imengonezeka kutoka asilimia tano mpaka tisa na hii ndiyo sababu kubwa ya mabenki yetu ku-*collapse*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *World Bank Report* ya mwezi huu imeonesha pia kwamba urahisi wa kufanya biashara yaani *easy of doing business*, Tanzania tumeporomoka kutoka nafasi ya 132 ya mwezi huu mpaka 137. Deni la Taifa ambalo linapaa kwa kasi ya ajabu linaongezeka kwa asilimia 17. Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa hesabu ya kawaida tu kama deni linakuwa kwa asilimia 17 na uchumi unakua kwa asilimia 6 katika hali ya kawaida ni vigumu kulipa deni hili kwasababu huwezi kushindanisha baiskeli na bodaboda. Deni linakwenda kwa *speed* kubwa sana ambayo inakuwa siyo ya kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali na viongozi wake mmekuwa mkijinasibu mara kwa mara kwamba nyie ni Serikali ya watu wanyonge, ninyi ni Serikali ya watu mnaojali maslahi ya watu maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 70 ya wakulima wa Kitanzania asilimia 75 ni wanawake, sijaona *effort* zozote za Serikali za kuweza kusaidia hawa wakulima wa Taifa hili hasa katika suala kubwa la mbolea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napitia *report* ya *Poverty and Human Development* ambayo imeonyesha kwamba kwa wastani, mwananchi/mkulima wa Tanzania anatumia kilo tisa kwenye ekari moja ya shamba lake, lakini kwa nchi ndogo kama Malawi, mwananchi wa kawaida kwa wastani anatumia kilo 27 kwa ekari moja. Sasa ninashindwa kuelewa na natafuta *reflection* ya Serikali ambayo inajinasibu kwamba yenyewe ni Serikali ya wanyonge, natafuta *reflection* ya matendo yake na hawa wanyonge. *Reflection* ya Serikali ya wanyonge haipo kwenye kujenga kiwanja cha ndege wapi kule?

MBUNGE FULANI: Chato!

MHE. JESCA D. KISHOA: Chato! *Reflection* ya Serikali ya wanyonge haipo kwenye kununua bombadier ambazo hata uwezo wa kusimamia bado ni mdogo zaidi ya kuingiza hasara tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *reflection* ya Serikali ambayo inajinasibu kwamba ni ya wanyonge sitegemei kama inaweza ikawaumiza sekta binafsi kwa sababu wote humu ndani tutajua umuhimu wa sekta binafsi katika maendeleo ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hebu tujaribu kuwa wakweli, hebu tuwasaidie hawa Watanzania, ninyi mnafahamu namna ambavyo mambo yanakwenda ambavyo siyo vizuri, lakini mnashindwa kusema hapa. Mshaurini Mheshimiwa Rais vizuri na nimefurahi kuona baadhi ya Wabunge wa CCM wamefunguka na wameonyesha *concern* yako ka Mheshimiwa Dkt. Mpango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Dkt. Mpango, ukweli ni kwamba kama haya unayoambiwa hautayazingatia huko mbele ya safari kila kitu kitakuja kukurudia wewe, kwa sababu nchi inaporomoka. Ukiangalia Mheshimiwa Mkapa alivyokuja alikuta deni ni kubwa sana akalishusha mpaka ikawa trilioni 10, akaja Mheshimiwa Kikwete akaacha deni la trilioni 45 sasa kipindi kile kama mnakumbuka vizuri mwaka jana nilitoa

maelezo binafsi kuhusiana na Deni la Taifa kutoa angalizo kwa Serikali na ninsahukuru na wewe ulikuja ukatoa maelezo kwa kuonesha *concern* yako kwamba umeyakubali na unayafanyia kazi, lakini cha kusikitisha ni kwamba ile *concern* ambayo uliionesha. Mheshimiwa Mpango unakataa, lakini tulizungumza na uliniambia. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natamani kuona Taifa la Tanzania ambalo kwa muda mrefu sana limekuwa ni Taifa la kimasikini tunaliangalia kwa jicho la tofauti katika kuleta maendeleo. Kama nilivyotangulia kusema kwamba sitakuwa na mengi ya kusema maana mengi tumeshayasema kwenye Mipango mingine iliyopita kwahiyo haya hata nikiendelea kuongea tutaendelea kurudia tu mambo ni yale yale hakuna kinachobadilika, hakuna kinachofanyika, kinachopangwa hapa sicho kinachofanyika, tunajadiliana mengine, yanafanyika mengine. Ukifuatilia matumizi ya pesa nyingi nyingine hazipitishwi na bajeti ambazo tunakuwa tunazipanga hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Mary Nagu, *no, no*, kabla ya Mheshimiwa Mama Mary Nagu, Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni halafu Mama Nagu utamalizia. Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi leo nichangie kidogo mambo machache ya msingi ambayo nafikiri ni vyema tukakumbushana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira ya kawaida, ya namna utawala wa nchi yetu ulivyo Chama cha Mapinduzi kina dhamana kubwa kwa sababu ndicho chama kilichozalisha Serikali. Lakini wakati wa uchaguzi, wakati tayari imeshatoka ilani ni Chama cha Mapinduzi tulisikia kauli yenye ukakasi, badala ya kuwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi mkaona raha sana kujiita Serikali ya Magufuli. Juzi katika ziara ya Mheshimiwa Rais amerudia kauli

hiyo akisema CCM kuna majizi, kwenye vyama vya siasa kuna majizi alichanganya vyama vyote, vyote vya upinzani na chama chake akasema ndio sababu yeye anasema Serikali ni ya kwake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunajuliza hivi tuna Serikali ya Chama cha Mapinduzi, chama kinachosimamia Serikali yake ama tuna Serikali ya mtu, anajisimamia mwenyewe. Napata wakati mgumu sana ninaposikia Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, Wabunge wenzetu wanajirasibu Serikali yetu ameshawaambia Serikali ni yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimesikia michango ya Waheshimiwa Wabunge wote wa pande zote mbili nimshukuru sana Mheshimiwa Bashe na Mheshimiwa Serukamba wamekuwa *honest*yna hatutaisaidia nchi hii kwa kuwa wanafiki, tutaisaidia nchi hii, tutaisaidia Serikali yetu, tutawasaidia wananchi wetu wote kwa kuwa wakweli, kuwa *critical*/kwenye mambo ambayo tunafikiri ni ya lazima, tupongeze pale ambapo tunafikiri kuna haki ya kupongeza tuko tayari kupongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati tunapokosea tusipoikemea Serikali, tusipoiambia Serikali ukweli na wale wanao-*criticize* wanaonekana wana stahili ya kufa, wale wanaikosa Serikali wanaonekana wana stahili ya kuumizwa, hatutafika. Chama cha Mapinduzi, chama chochote cha siasa kikifikia hatua ya kutokutaka ushauri, kikifikia hatua ya kuweka pamba masikioni kutokusikiliza watu wanasema nini, chama hicho hata kingekuwa kina nguvu kiasi gani za kijeshi lazima kitakufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo, naomba Chama cha Mapinduzi kifanye wajibu wake, mtanisamaehe, nimefuatilia ndani ya vikao vya Chama cha Mapinduzi kama hata mambo haya yanajadiliwa kwenye vikao vya chama. Lazima tuambiane ukweli ninyi mna dhamana kuliko sisi, sisi ni wapinzani lakini ninyi ndio watu ambao mmepewa dhamana ya nchi hii maumivu yanapotokea kwa wananchi

nyinyi mko *responsible* kuanzia Rais ninyi Mawaziri, Wabunge wa Chama cha Mapinduzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachokiuliza ni kwamba tuna mfumo upi? mmesimama wapi kwenye msingi wa kiitikadi? Ninachokiona kinachofanyika kwa juhudi sana ni kujaribu kulirejesha Taifa hili kwenye ujamaa. Ndugu zangu *policy* za ujamaa zinapendeza sana na ni tamu sana kuzitungumza, lakini ukweli wa uhalisia wa hali halisi ya binadamu inakwambia tukijaribu kung'ang'ania siasa za kijamaa *we are bound to fail*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya makusudi nika-*tweet* asubuhi jana asubuhi nikizungumzia kuhusu suala la mahusiano ya Serikali na *private sector*. Nika-*tweet* halafu nione *reaction* ya watu watasemaje. Wakajitokeza watu wengi wakisema wapinzani mnajifanya ninyi mna mawazo mazuri sana, lakini nilichokuwa nakisema hatutajenga uchumi wa nchi hii kwa kutumia bunduki, hatutajenga uchumi wanchi hii kwa kutumia ubabe na vitisho, ni lazima Serikali itambue kwamba *private sector* ndio injini ya *economy* na Serikali ni bodi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili gari liende linahitaji *engine* linahitaji matairi linahitaji bodi, bodi ni Serikali, matairi ni Serikali, *engine* ni *private sector*. Hakuna Taifa lolote limeendelea duniani kwa kuipuuza *private sector*, hakuna Taifa lolote limeendelea duniani kwa ku-*disturb private sector*, hakuna Taifa lolote limeendelea duniani kwa kufikiria *private sector* ni wezi tu. Kufanya biashara katika nchi hii chini ya Awamu ya Tano ni kياما, wafanyabiashara wote wa ndani na wa nje wanalia, Mheshimiwa Mpango tumemwambia kwenye Kamati ya Bajeti. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwona Rais anahimiza viwanda unashangaa hivi Watanzania mnajua tumeanza sera ya *industrialization* lini? Soma historia ya *industrialization process in Tanzania* na *challenge* zake. Hakuna kipindi ambacho tunakabiliwa na tatizo kubwa kama kipindi hiki kwenye masuala ya uwekezaji kwenye upande wa viwanda,

kwa sababu tunaandika *paper*nyingi, tuna-*policy document* nyingi, tatizo letu kubwa ni utekelezaji. Tunapanga mipango mingi ambayo hatuitekelezi sio awamu hii peke yake kuanzia awamu nyingi zilizopita. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasoma maandiko ya wasomi wetu fulani wanasema; *policy is crafted in Tanzania, modified in Uganda, implemented in Kenya.* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani Watanzania ni wazuri sana wa ku-*craft policies*, ndio nilikuwa nasema ukiangali *policy* mbalimbali ambazo zinazungumzia suala la viwanda nchini linasema nini, kwa miaka 10, 15 iliyopita tumekuwa na *Industrial Development Policy*, tumekuwa na *Vision 2025* najaribu ku-*define* na kutoa ile *frame work* tumekuwa na kitu kinachoitwa *Tanzania Integrated Industrial Development Strategy* ya 2025. Tumekuwa na *Mini-Tiger Plan* ya 2020, tumekuwa na *plan* hizi za miaka mitano, mitano zipo tatu ambazo Mheshimiwa Mpango utakuwa unazijua, tuna *National Trade Policy*, tuna *Small Medium Enterprises Development Policy* ya 2003. Sasa ukiangalia *policy* zote hizo zinazungumza kitu kimoja na hakuna hata moja unaweza kusema imekamili kwa asilimia 10 ama 15. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza habari ya kilimo kwanza tumezungumza haya mambo ya *agrarian revolution* tunazungumza mageuzi ya viwanda ya kilimo imezungumzwa sana chini ya Kilimo Kwanza, Kilimo Kwanza jamani leo kimeishia wapi? Tumetumia fedha chungu mzima, watu wamefanya *plan* chungu mzima *where is consistency* katika *planning* ya nchi haipo. Leo Rais anahimiza viwanda ili Tanzania *by 2025* iwe nchi yenye uchumi wa kati. Nchi yenye uchumi wa kati ambayo inaweza ikaitwa ni *industrialized country* lazima viwanda vya kuzalisha yaani *manufacturing* na *processing* viweze kuchangia angalau asilimia 40 ya *GDP*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *industrial* hiyo Tanzania inachangangia *less than 5% of the GDP*, lakini tunajuliza vilevile hivi viwanda vinavyohimizwa vijengwe soko liko

wapi? Huwezi ukajenga uchumi wa viwanda kwa kutegemea soko lako la ndani ni lazima *the biggest part of your production* iende katika masoko ya jirani na ndio sababu wenzetu wa Asia walivyokuwa na ile *Asia Mini Tiger Plan* ya Asia ya *Southern Eastern* ya Asia na Vietnam walifungua kwanza mipaka yao, wakatengeneza *National integration policies* ili kwamba *product* inayotoka Tanzania inaweza ikauzwa Kenya, ya Kenya ikaenda Uganda lakini ukiangalia mahusiano yetu namna tunavyojenga mahusiano Afrika Mashariki *actually* leo tunafunga mipaka hatufungui mipaka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoma vifaranga, tunauza ng'ombe za watu, tunaharibu mahusiano yetu, katika misingi kama hiyo tunategemea tutawezaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala la utawala bora hili jambo tunalizungumza wenzetu mnaliona kama ni utani hili jambo sio utani, hali ya nchi yetu leo kiusalama, ukizungumza leo unashatakiwa, ukichambua uchumi leo unashitakiwa, sisi wapinzani tufanye nini huo ndio wajibu wetu? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatoa takwimu za uongo, Benki Kuu inatoa takwimu zinazotofautiana na Wizara ya Fedha na watu wa takwimu kila mmoja anatoa takwimu zake pengine ili kuilinda Serikali. Ndugu zangu ninachowambia ni kwamba kama tusipojipa ujasiri wa kuikosoa Serikali pale ambapo inabidi, tukaacha kuunda sheria ndogo ndogo za kudhibitiana humu ndani, za kudhibitiana nje ya Bunge tukawazuia Watanzania wasiongee, msiba utatuumbua, msiba utaumbua. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali yetu ya uchumi ni ngumu na uchumi sio *fly over* wala uchumi sio ndege sita, uchumi ni kipato cha wananchi wa kawaida waweze kuboresha maisha yao kutoka pale walipo kwenda maisha bora zaidi. Watanzania wanazidi kuwa maskini na kundi dogo la watu ndilo ambalo linaweza kuona faida ya kukua kwa uchumi wa Taifa hili. Kukua tunakoambiwa kwa uchumi

haku-reflect kwenye maisha ya wananchi, wananchi wanazidi kuwa maskini kila siku hili jambo tukilisema wenzetu mnaona labda sisi ni wachokozi, lakini ukweli ni kwamba yako mambo mengi yanaendelea nchi hii leo kama hamkumwambia Rais hamumsaidii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia na rafiki yangu Ndassa, ndugu yangu rafiki akizungumza suala la ukanda nakubaliana naye 100%; lugha ya kuanza kusema kanda hii kanda ile sio nzuri. Vilevile hebu tujipe ujasiri wa kufikiria chanzo cha maneno hayo ni nini? Kwa nini maneno hayo hayakuzungumzwa miaka minne iliyopita, hayakuzungumzwa miaka mitatu iliyopita, kuna mambo ambayo lazima tufike mahali tuelezane ili tuishi kama Taifa la Watanzania kila mmoja akionekana ana haki katika Taifa hili, tuache kuwa na *double standard*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni chama cha siasa tuna wanachama nchi nzima, tungependa tuwe kama Watanzania, tusingependa tuanze kunyoosheana vidole huyu ni kabila fulani, huyu ni dini fulani, huyu ni rangi fulani sio lugha inayopendeza. Lakini yako mambo yanayofanyika katika nchi yetu leo ambayo yanabagua baadhi ya watu wanaonekana wao wanakuwa *disenfranchised*, haya yasipozungumzwa misiba itakuja kutuumbua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mengine mumwambie bwana mkubwa kwamba unapofanya mambo mengine tenda haki pande zote, tutampongeza tutamsifu, lakini unapokuwa kwamba wewe haki hiyo labda unaipeleka mahali fulani na ukanda mmoja unawanyima. Niseme mfano mmoja ambao ni dhahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchaguzi unazalisha viongozi kutoka maeneo mbalimbali na watu wote wana haki ya kuchagua na kihistoria katika nchi yetu viongozi waliotangulia Marais wetu waliotangulia walihakikisha kwamba hata nafasi za uteuzi katika Serikali, katika mashirika, katika taasisi za umma zinagawiwa kwa Watanzania kwa wote kwa kadri iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo sio hali inayofanyika leo katika nchi hii na mkitaka nilete takwimu nitaleta takwimu za *appointment* zote za bwana mkubwa tangu ameingia madarakani kwamba kuna baadhi ya watu na baadhi ya mikoa ambayo makusudi kabisa imekuwa *disenfranchised*. Huu ni ukweli ambao ni lazima tuuseme mambo haya hayapendezi kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukija kwenye mambo ya msingi sana Awamu ya Nne ya Serikali iliyopita tulizungumza uchumi wa gesi, ukiangalia kwenye Mpango wote huu uchumi wa gesi ni kama vile umesahaulika hivi ni chama kilekile ama ni chama kingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekwenda ukanda wa kusini kutembelea hiyo miundominu ya gesi ni mambo ya aibu, ni mambo ya kulia, tumejenga bomba la gesi kutoka Kusini kuja Dar es Salaam...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Naambiwa ni kengele ya pili ahsante sana Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mama Dkt. Mary Nagu tafadhali una dakika kumi na tano pia. Atakuwa msemaji wetu wa mwisho mchana huu.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakupa shukurani kwa kunipa fursa hii na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge kuwapongeza Mawaziri walioteuliwa na kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuwateua watu ambao nafikiri wataongeza kasi yake ya kuendesha nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi ni siasa na siasa ni uchumi na uchumi ambao unategemewa ni ule ambao una mipango mizuri au mpango mzuri. Waheshimiwa Wabunge mtakubaliana na mimi kwamba mpango wa miaka mitano

ambao unatekelezwa kila mwaka ni mpango mzuri ambao tumeupitisha na kilichobaki sasa ni utekelezaji. Kwa hiyo, mpango ni mzuri na aliyeuandaa ni Mpango huyu Mheshimiwa Waziri, na ninajua alivyohangaika na kuja na mpango huu mzuri kwa kweli kwa hilo nampongeza. Na azma ya Taifa kupitia mpango wa miaka mitano unaotekelezwa kila mwaka kwa vyovyote vile ni kufikia dira ya 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mpango watu wengi wanakutegemea na nina hakika umefanya hivyo kuona kwamba dira yetu ya 2025 inataka nini na kuona mipango hii kila mwaka kama inatupeleka kule. Na mpango huu unatekelezwa kupitia bajeti ya kila mwaka na azma yetu ni kuwa na uchumi wa kati na wa viwanda, sasa katika mipango hii kuna vipaumbele vilishaonyeshwa na ni kiasi gani cha uchumi kitakuwa ambacho kinatufikisha kule ambako tulitegemea kwenda. Kama tunaenda kwa mpango wetu uchumi wa mwaka huu ungekuwa unakuwa kwa 8% mpaka 10% kufidia kule ambako nyuma tulikuwa hatujafikia kule tunakotakiwa na inawezekana kwa sababu miaka iliyopita tulishafika 8% na zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ilivyobaki sasa ni kuangalia kwanini sasa uchumi unakuwa kwa 6.8% ambayo ametuletea sisi ambayo sio 8%, na kazi yetu Waheshimiwa Wabunge ni kuonyesha mapungufu yako wapi na kuishauri Serikali ifanye nini kusudi tusonge mbele na mimi nitatumia muda wangu zaidi katika kuonyesha tufanye nini ili tupige hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaotekeleza mpango huu sio Serikali peke yake, sekta binafsi na wananchi kwa ujumla tunapaswa kutekeleza mpango huu. Tutakachouliza kwa Serikali na ninachoomba kwa Serikali ni kuiwezesha sekta binafsi na wananchi kusaidiana na Serikali kutekeleza mpango huu utufikishe mbele na kwa upande wa Serikali unachangia kupitia bajeti ya Serikali, kwa hiyo, tuseme kwa

kiingereza tuwe na *consistency* ya kukusanya mapato bila kuuu uchumi. Mimi ndio ushauri wangu kama VAT inapunguza *production* angalieni! Kama VAT inapunguza ajira angalieni! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niwaambie hakuna shamba linalovunwa bila ya kupanda, hakuna uchumi utakaokuwa bila *investment* au uwekezaji haiwezekani. Kwa hiyo, tuangalie kama uwekezaji unakwenda kwa *principal* ambayo tunataka uchumi wetu ukue. Kuna jambo ambalo siku zote nimelishauri na hata mimi mwenyewe nimejitahidi ni kuweka *One Stop Center* kwa ajili ya *investors* ili wasihangaikie hangaikie na kupoteza muda. Muda ukishakwenda haurudi ndugu zangu.

La pili ni kwamba, pale sasa hivi huu uchumi unaokuwa kwa 6.8 unatokana na *sectors* ambazo sio za watu wengi, wamesema wengine. Kwa hiyo, ndugu zangu tuangalie ni sekta zipi na bila mjadala na wengi wamesema kwamba sekta ambayo itaifanya viwanda vifanye kazi nchi hii ili vipate malighafi na chakula kwa wafanyakazi ni sekta ya kilimo, Mheshimiwa Mpango angalia bajeti ya mwaka juzi na mwaka jana kama tunaongeza bajeti ya kilimo bila ya kutafuta visababu sababu. Bila ya kilimo kama walivyosema wengine ndugu zangu hatuwezi kwenda popote kwa sababu malighafi itatokana na kilimo lakini kilimo ndicho kinachoajiri watu wengi nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sio hivyo, hata wafanyakazi wa viwandani baadaye watapata chakula chao wapi? Ni kutokana na kilimo. Lakini sio hivyo, leo utaona ajabu, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo ambayo Mheshimiwa alitaja asubuhi kwamba unaona Songea na Kusini kule bei ya mahindi ni shilingi 25,000 kwa gunia lakini Serengeti na Maswa ni shilingi 80,000 mpaka 100,000 na zaidi. Kwa nini kuna tofauti hii? Lazima kuna tatizo na ndilo ambalo tunapaswa kuliangalia. Mimi siamini kama uchumi umerudi kwenye ujamaa, huu ni uchumi wa soko lakini Serikali lazima *i-regulate*, ione kwamba bei ya Kusini inapanda na ione kwamba bei ya chakula kule Kaskazini inashuka na

tulimwambia Mheshimiwa Waziri kwa nguvu zote na nilitegemea ametekeleza kwamba hakikisha *NFRA* iweze kwenda kununua mahindi kule ili bei kidogo ipande na ipeleke kule ili bei kidogo ishuke kwa chakula. Lakini hatujui kama amefanya hiyo ripoti kama sekretarieti inaleta itakuwa imefika kwako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alipaswa aeleze ame-*act* namna gani na hapo ndipo ambapo tunaleta matatizo, lakini kwa kilimo lazima kuwe na tija. Tija ya kilimo inatokana na pembejeo na zana, lakini ukiwa umelima sana hamna soko ni sawasawa na kutupa shilingi chooni. Lazima tuwe na masoko, lakini kazi ya masoko ya kilimo haiko kwenye Wizara ya Kilimo, iko kwenye Wizara ya Viwanda na hatujawahi kusikia viwanda ikiongelea masoko ya mazao ya kilimo hata siku moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sio hivyo, namna ambavyo Wizara ya Viwanda inaweza kutengeneza masoko ya mazao ya kilimo ni kuanzisha viwanda vitakavyoongeza thamani ya mazao ya kilimo, hilo ndilo soko la uhakika. Kwa hiyo, tuangalie bajeti kama inafanya hivyo, kama hivyo vipaumbele tunaviweka kama inavyotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba Mwenyezi Mungu amejiatia Tanzania. Tuna rasilimali nyingi, tuna madini, tuna vito, tuna ardhi na tutakachoweza kufanya nchi hii iendelee ni kuongeza thamani ya rasilimali hizi. Sasa wamesema kwamba kuna mfumko wa bei, kuna mfumko wa bei nzuri na mfumuko wa bei mbaya. Kama mfumko wa bei unatokana na *credit squeeze* au kuondoa *money* kwenye *circulation* hiyo sio nzuri sana. Mfumko wa bei unapaswa kupungua kwa kuongeza uzalishaji na chakula nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tu-*manage* hayo mambo, tunataka au hatutaki lazima tuya-*manage*. Sasa sio mfumko wa bei tu kuwa chini ndiyo sifa, umetokana na nini? Tujue kwa nini hakuna hela kwenye *circulation*, na kama hakuna hela namna ya kuwekeza ndani ya nchi ni kutokana

na mikopo au *equity*. Hamna namna nyingine, kutokana na hela yako mwenyewe au kutokana na mikopo. Angalieni wenye hela kama wanawekeza, angalieni mabenki kama yanatoa mikopo kwa ajili ya uwekezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani nilivyokuwa viwandani nilikuwa kwenye bodi ya benki moja. Ilikuwa inatoa hela kidogo sana kwenye kilimo na ilikuwa inatoa hela kwenye biashara nyingi. Kwa hiyo zile hela zikawa zinakwenda kuzungusha vitu ambavyo havitokani na *production* ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuangalie hayo mambo na mimi mwenyewe na Mheshimiwa Mpango kama unataka tunaweza tukakaa pamoja, tukaangalia hayo mambo tutayafanyaje? Na fahari yangu ni wewe ufanye vizuri na kufanya kwako vizuri ni kufanikisha uchumi wa nchi hii. Serikali imefanya makusudi kuweka uwekezaji na Wizara ya Fedha pamoja, sasa usiuzuie uwekezaji ukawa mdogo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo tunapaswa kuwa na kipaumbele ni miundombinu kwa sababu bila miundombinu soko haliwezi kufikika na pembejeo haziwezi kufika kwenye kilimo. Lingine jamani ni kwamba tuone ajira kama inapungua nchi hii au inaongezeka, vijana ni wengi na nguvu kazi ni nyingi, kama ajira haiongezeki maovu yataongezeka ndani ya nchi yetu na hilo lita-*affect* uchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nisisitize kwamba jamani *One Stop Center* iko kule Rwanda tukaiangalie, tuilete Tanzania na halafu tuweke ile *Logistic Centre* pale Kurasini ndipo tutaona *demand* kubwa ni ya nini halafu tunawekeza na mengine yote ambayo tunaweza kuyafanya ili uchumi wetu uweze kupiga hatua. Serikali ijaribu kuona kwamba *private sector* jamani inakuwa na *confidence*, Serikali iweze kuona kwamba *private sector* iwekeze na wakipata faida watoe kodi, bila kodi na wao hawawezi kuendelea kuwepo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tuangalie upya kama sera inatekelezwa vizuri kwa sababu kuwa na sera nzuri si jambo la muhimu sana ni kuwa na sera ambayo inatekelezeka na inatekelezwa. Kwa kweli huu ni uchumi wa soko na *private sector* kama walivyosema wengine ndiyo *engine* na hiyo *engine* isipokuwa inafanyiwa *maintenance* kila wakati na kuangalia mahitaji yao itabaki Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja nataka nilisahihishe, mahali ambapo *private sector* haifiki, Serikali lazima iende. Kwa hiyo, kama *shipping* haiendi vizuri kwa kuwaachia *private sector* peke yake sioni ajabu kama Serikali inakwenda pale. Kwa hiyo, Serikali haiendi sana kwa ajili ya faida, Serikali inaenda kwa ajili ya mahitaji. Kama wananchi wanahitaji jambo na sekta binafsi haiendi lazima Serikali iende, kwa hiyo makampuni ya Serikali lazima yaendeleo kuwepo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo ndugu zangu tukosoe Serikali lakini tukosoe kwa namna ambayo tunaishauri na tunasaidiana nayo kufanya uchumi wa nchi hii kushamiri na nina hakika ni rahisi kutoka katika ukuaji wa uchumi wa asilimia 6.8 kwenda 8 mpaka 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilifanya *thesis* yangu ya kuondoa umaskini na kukuza uchumi. Wakati nilipofanya nafikiri ni mwaka 2002 au 2003, niliona kwamba kukua kwa uchumi kwa asilimia 11 ndiyo mahali ambapo tuna uhakika na kuondoa umaskini wa Tanzania. Inaweza kuwa chini, inaweza kuwa juu zaidi lakini asilimia 11 ndiyo ukuaji wa uchumi ambao utatuhakikishia Tanzania kupiga hatua mbele kiuchumi na kupunguza umaskini na kuongeza ajira na kuleta maisha mazuri kama dira yetu inavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Bunge linarejea.

(Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tutakaporudi jioni tutaanza na Mheshimiwa John Kadutu, Mheshimiwa Adadi Rajabu, Vedasto Manyinyi, Mheshimiwa Zainab Mndolwa na wengine watafuata. Ninachoendelea kukisisitiza tu ni kwamba, kwakweli soma huu mpango angalia hali halisi. Ninyi ni sehemu ya Watanzania, ukija hapa ongea kitu kinachoeleweka. Huu sio uchangiaji wa bajeti kwamba utakuja hapa unababaisha babaisha hapana. Tuoneshe kweli sisi ni Wabunge kwa sababu hawa Mawaziri kwa kweli mahali wanaposhauriwa ni hapa Bungeni, sasa sisi tusiwe sehemu ya Watanzania wanaolalamika lalamika huko nje. Sisi tumechaguliwa na wananchi kuja hapa, tuseme.

Kama nilivyosema wakati ule, habari ya jimbo sawa unaweza ukafanya kama mfano. Hili watu wengi huwa wanalichanganya sana, jimbo ulilochaguliwa ni namna ya kupatikana kwako, yaani nchi hii tumekubaliana Wabunge wetu tuwapate, ili tupate Wabunge wa kutoka Mtwara, Tarime, Bukoba, Pemba na kutoka wapi ili Bunge hili liwe *national* ndiyo maana Katiba yetu ikasema tupatikane namna hiyo na wengine wanateuliwa na Rais, na wengine wanakuja Viti Maalum yaani hiyo yote ni namna ya kupatikana. Lakini tukishapatikana sisi wote kwa madirisha yote yaliyotuleta hapa sisi ni Wabunge wa Taifa la Tanzania. *(Makofi)*

Sisi ni Wabunge wa Tanzania, lile jimbo lako ni namna ya kupatikana kwako. Ndiyo maana nashangaa watu wengine wanalinganisha Mbunge na *DC*, sitatoa majibu lakini hakuna nchi yoyote unaweza ukalinganisha watu hawa wawili halafu ukasema huyu ni mkubwa, unatoa wapi majibu hayo? Huyu ni Mbunge wa Taifa, unalinganisha Taifa na Wilaya? Haiwezekani! *(Makofi)*

Kwa hiyo tuna nafasi kubwa katika nchi yetu na hii ni moja ya nafasi ambayo tumepewa kikatiba tushauri mwenzetu ametuletea Mpango na Mheshimiwa Dkt. Mpango ni mtaalam wa mipango, kwa hiyo, unapokuja jiandae! Na

mimi nitafurahi sana kwa sababu ndiyo namna ya kuisaidia nchi yetu ili tuweze kutoka hapa tulipo tuweze kwenda mbele. (Makofi)

Kama walivyosema baadhi, na mimi nilibahatika kwenda Urusi juzi hapa, tulikuwa Mji mwingine unaitwa St. Petersburg, lakini nikalazimisha kuja Moscow nikatembelea Bunge lao na nikaenda Makao Makuu ya Chama cha Kikomunisti rafiki zetu CCM, niliwatembelea. Kule sasa hivi Chama cha Kikomunisti ni chama kidogo sana, wamekaa wanyonge namna hii. Urusi huoni ujamaa uko upande gani, wamebadilika kabisa. Ni nchi inayokuwa kiuchumi, *one of the fastest* kabisa. Moja ya mambo hayo ni hayo hayo mambo ya *private sector*.

Reli niliyoitumia toka St. Petersburg kuja Moscow ile reli ni ya Serikali, lakini mabehewa yaliyomo mle ni *private sector* na kiwango cha hata hayo mabehewa na ubora wake na nini ni kama unasafiri kwenye ndege tu. Kwa hiyo, *private sector* unaona, Serikali, *private sector* haya maneno sio utani. Hatuwezi kwenda bila mchanganyiko huo vizuri, Serikali na *private sector*. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na mjadala wetu vizuri jioni kuanzia saa 11.00 jioni kwa hiyo naahirisha shughuli zetu mpaka wakati huo.

(Saa 07:13 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi saa 11:00 Jioni)

(Saa 11:00 Jioni Bunge lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti

HOJA ZA SERIKALI

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae. Katibu!

NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Tukae Waheshimiwa!

Waheshimiwa Wajumbe tunaendelea na mjadala wetu. Tunaanza na Mheshimiwa John Kadutu na badaye Mheshimiwa Adadi Rajabu, ajiandae.

MHE. JOHN P. KADUTU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kunipatia fursa hii ili na mimi niweze kuchangia machache juu ya mpango huu. Kwanza kabisa nimshukuru Spika, kwa asubuhi ya leo amefungua milango ya namna ya uchangiaji na kuttoa hofu. Wapo watu wamekuwa na hofu namna ya kuchangia wakihofia labda mtu anaweza kutumia maneno yakasababisha kupelekwa kwenye Kamati ya Maadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama ndivyo, ushauri wangu sasa kwa Wabunge wote lakini zaidi kwa vijana wasomi, mnayo nafasi ya kuisaidia Serikali, kuishauri kwa uwazi na kwa haki ili mawazo yenu na ushauri uweze kupokelewa. Hatuna haja ya kuwa na wasiwasi na bahati nzuri uteuzi umepita mpaka 2020 naamini tusiwe na hoja ya kufikiri kwamba, kuna uteuzi au mambo gani. Kwa hiyo, tujikite kuishauri Serikali kwa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwapongeza Mawaziri, kwanza wale waliobaki kwenye Baraza la Mawaziri, lakini pili ni wale ambao wamepata fursa ya kuingia kwenye Baraza la Mawaziri, ni imani yangu nafasi hiyo wataitumia vizuri kutusaidia kusonga mbele kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia liko jambo ambalo ni vizuri nikalisema ambalo ni tatizo lililoko jimboni kwangu, lakini kwa maana ya kitaifa juu ya hifadhi. Wananchi wetu sasa wanateswa. Tunazungumzia mipango ya maendeleo, wakati huo huo kuna watu wanapitisha mabango kusema shughuli za kibinadamu zisifanyike, watu baada ya wiki mbili wahame, unazungumzia Wilaya ambayo

asilimia 90 ni hifadhi, lakini ndani ya hifadhi kuna vijiji ambavyo vimesajiliwa, kuna shule ambazo zimesajiliwa, tunaenda wapi? Unapowaambia watu eneo lote la Ulyankulu ni hifadhi, halafu watu wako mle kabla, si ajabu hata ya Sheria ya Hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuiombe sana Serikali kama kweli tunazungumzia maendeleo hebu tusiwabughudhi watu wetu, tusiwaone watu bora wakati wa kufikia uchaguzi. Wakati tunapo-*approach* uchaguzi mambo yote haya tunaambiwa kaeni, chapa kazi muishi kwa amani, lakini hapa katikati anakuja mtu wa *TFS* anavuruga kila kitu, unataka watu waishi wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani jimbo zima, wilaya nzima tunatunza miti, ifike mahali tujue nani bora, bora msitu au bora binadamu? Itatusaidia sana badala ya kuwa tunawavuruga wananchi wetu, wanapanga na wao mipango yao ya maendeleo, leo unawaambia kuanzia sasa shughuli za kibinadamu zisimame, maana yake maendeleo yasimame. Maeneo hayo yanayoambiwa hivyo, labda wiki moja u mwezi mmoja nyuma Waziri Mkuu amepita na hata yeye kuchangia.

Kwa hiyo, Serikali hii iangalie huyu anasema hivi, kesho mwingine anasema hivi na mwingine atakuja weka ndani. Imefikia hatua Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya anawekwa ndani kwa jambo kama hili. Kwa hiyo, niombe sana Serikali itusaidie kutuliza hali hiyo na ninajua mdogo wangu Mheshimiwa Kigwangalla atalirekebisha pamoja na Mheshimiwa Hasunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa twende kwenye kilimo. Kilimo ndio uti wa mgongo tunavyozungumza kila siku na kilimo ndicho kinachotuletea pesa nyingi za nje, hapo tunakuwa tunazungumza habari ya mahindi. Nawashangaa sana watu wanaotetea wakulima wasiuzze mahindi, sisi mishahara yetu hakuna anayetupangia matumizi. Iweje mkulima ambaye kalima bila mkopo, kwa fedha zake, halafu apangiwe namna ya matumizi ya mahindi yake? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Ulyankulu tunalisha Mwanza, tunalisha Shinyanga kwa mahindi yanayotoka Ulyankulu. Ni kwa vile tu mnaowataja hamuitaji Tabora, lakini kumbuka kwamba watu wa Mwanza, watu wa Shinyanga, Kahama, mahindi wanayokula yanatoka Ulyankulu na sisi tuko tayari kuza. Kama ni hivyo mimi siko tayari kuhimiza kilimo kwa sababu watu wanafanya juhudi, wanalima chakula kipatikane, lakini tunaanza kuweka vikwazo kwa mkulima kutumia rasilimali zake. Mbolea amenunua mwenyewe kwa pesa zake, kila aina ya pembejeo amenunua, lakini inafika amevuna anapatikana mtu wa kumpangia, haijapata tokea, hayo ni mahindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumbaku hii ya sasa imekuja mwaka 1967, na mimi mkubwa tu mwaka 1967, sasa tumbaku hiyo huko nyuma tarehe 5 au 6 Julai, kabla ya Sikukuu ya TANU ilikuwa ni lazima wakulima wote wawe wameshapata pesa; haijapata tokea safari hii masika mvua inanyesha tumbaku bado iko kwenye ma-*godowns*, tumeweza kwenye makinikia eti tunashindwa kwenye tumbaku, haiwezekani. Nini kipo hawa wazungu wa tumbaku wawe na kiburi kuliko wa makinikia? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi tena siko tayari, nasema kabisa, yaani siwezi kusimama jukwaani kuhimiza kilimo ambacho watu wanateseka, tumbaku limekuwa zao la kuleta umaskini sasa. Hiyo korosho ya wenzetu Mtwara huko, Lindi zamani isingesikika, lakini kwa sababu nia ya Serikali ilikuwa kuhakikisha kuwakomboa wenzetu wakulima wa korosho, leo hii wanafurahia. Lakini tumbaku tunahangaika. Tumbaku iko kwenye ma-*godown*, mvua zinanyesha, lakini utashangaa tunasema tumbaku hii ni zao linaloleta pesa kuliko mazao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kampuni ile iliyochukua mali za TAT inauza mpaka ma-*godown*, itauza kwa *tender* ma-*godown* yote nchi nzima yametangazwa yanauzwa, hiyo tumbaku itakuwepo, haitakuwepo. Na leo hii tunazungumza hivi kama mzaha, watu wameuza tumbaku wale ambao hawakuwa kwenye mpango kwa maana ya

bajeti ile ya tumbaku wameuza mpaka ile bajeti ime-*burst*, wale wakulima sasa waliochelewa wanaambiwa mna tumbaku ambayo hamkupangiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linaleta taabu. Sisi wanasiasa wa Tabora na hasa Wabunge tunapata kigugumizi, iko shida lazima, iko shida hapa katikati. Tumesafisha *WETCU*, lakini iko shida hiyo shida huko mbele najua itakuja kuumbua watu, hatuwezi kukaa jambo moja tu tunarudia, Waziri Mkuu amekuja karibu mara nne, lakini hakuna ufumbuzi. Wazungu wameona kwamba, wao ni zaidi ya Serikali, lakini tunaambiwa watu tutafute masoko wenyewe, hivi mkulima mmoja mmoja aanze kwenda Uchina, Indonesia, wapi, kutafuta soko, haiwezekani, maendeleo gani hayo tunayataka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa muda si mrefu tutaanza kusimama majukwaani kuwaambia acha kulima tumbaku. Nitawaambia watani zangu Wasambaa na Wadigo leteni katani tuanze kulima katani kwa sababu sasa tumbaku haitusaidii. Watu wetu wamekuwa maskini, sio vizuri na Serikali muangalie kule ambako Serikali inapata mapato, nayasema haya kwa uchungu. Jimbo la Ulyankulu ndio linalotoa mahindi kwa wingi, tumbaku kwa wingi. Aah, hii kengele tayari? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maji, tumesema hapa leteni mpango kuhakikisha nchi nzima inapata maji kama ilivyo *REA I*, *REA II* na sasa tunakwenda kwenye *REA III*, shida gani ipo? Maji yakipatikana hayo mambo mengine yanakwenda vizuri, lakini maji haya imekuwa tatizo, maji ya Ziwa Viktoria wanatumia wenzetu kule Misri, wanatumia Ethiopia, wanatumia sijui Sudan, wapi, sisi eti tukitaka kutumia, tayari kaja mtu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tu miradi hiyo amekuja mtu kutembelea Tanzania, hatujui walichonong'ona, lakini tetesi ni kwamba wanapata hofu. Maji tunayo tele yanaweza yakasambaa nchi nzima, kwa nini tusifanye hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malagarasi pale kuna maji, ingawa yana shida, lakini maji ya Ziwa Victoria ni maji mengi sana, leteni huku. Tunakaa tunahangaika ooh, mvua, kwa nini tusipate maji kutoka Ziwa Victoria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara. Barabara tumekuwa na mipango. Ukiangalia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ziko barabara nyingi sana, acha mbali ahadi za Mheshimiwa Rais, lakini je, utekelezaji wake uko kwa kiwango gani? Leo tuna miaka miwili tunazo barabara nyingi, mojawapo barabara kutoka Mpanda – Ulyankulu mpaka Kahama, tunazungumzia ujenzi wa lami, barabara ni pori, hata upembuzi yakinifu hatuoni, mipango gani hii sasa?

Kama hatuna barabara zinazopita kwenye maeneo ya uzalishaji tunajidanganya. Ndio hii sasa mazao yanabaki sehemu yana bei ndogo, tunapiga kelele. Mheshimiwa Mpango jaribuni kuliangalia hilo barabara zetu zikae vizuri. Kuwe na nia ya dhati kwamba, sasa tunataka kutengeneza barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini reli hiyo *standard gauge* sina hakika tutachukua miaka mingapi, hapajaelezwa, lakini lazima kama ni hivyo reli zetu tuziimarishe. Tunayo reli ya kati, tunayo reli ya Singida, tunayo reli ya Moshi – Tanga, hebu tuingize nguvu zaidi kule wakati tunaendelea na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umeme *REA III*. Aah, *speed* imekuwa ndogo kabisa, Mheshimiwa Kalemani sijui *speed* yake imeshia wapi. Sijui baada ya kufika huko aliko, *speed* ya *REA III* ni ndogo sana. Tuiombe Serikali iongeze *speed* kwenye huu mradi, lakini kuhakikisha vijiji vyote ambavyo havikupitiwa, lakini taasisi zote, lakini na sisi wanasiasa tusiweke fitina maeneo mengine. Huko kuna uhakika kwamba, wanasiasa wakati mwingine tunapindisha maeneo mengine yasipate umeme kwa sababu za kisiasa, hebu tuache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za maendeleo kwenda kwenye Halmashauri bado ni tatizo. Iko Halmashauri moja ilipangiwa kupelekewa bilioni 11 imepelekewa bilioni moja, hebu tuone hivi kweli kuna jambo litaendelea? Kutoka shilingi bilioni 11 inapelekewa shilingi bilioni moja, shilingi bilioni nyingine shilingi bilioni 10 hazijaenda, unategemea nini katika eneo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zetu bado ziko tete haziwezi kujijendesha. Ziko Halmashauri hata kulipa posho ya Madiwani haziwezi kumudu, ningeomba sana uwepo utaratibu wa kuwahisha pesa. Mbona tunazungumza tunakusanya sana, sasa kama tunakusanya pesa inaenda wapi? Kama pesa kila siku tunasema makusanyo yamepanda, eeh, mbona pesa haziendi Halmaashauri? Iko nini? Iko shida gani? Pelekeni hela kule tuone tutakachokwama, bahati nzuri Wabunge wote sisi ni sehemu ya Halmashauri. Bila shaka Mheshimiwa Mpango utakuwa umenipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari? Aah, bado bwana.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa tayari muda wako umemalizika.

MHE. JOHN P. KADUTU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwe na upendeleo kwa machifu.

MWENYEKITI: Ahsante sana, tunaendelea na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, atafuatiwa na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi na baadae Mheshimiwa Zainab Mndolwa ajiandae.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nashukuru sana kupata nafasi ya kuchangia kwenye huu Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango mizuri ni ile mipango ambayo inatekelezwa, tumekuwa tunatengeneza mipango mizuri sana miaka mingi sana na utekelezaji wake unakuwa sio kwenye asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba hii mipango ambayo imeandikwa kwa mwaka 2018/2019 kama utekelezaji wake unakuwa kwa ukamilifu, basi tunaweza tukawa na uchumi ambao utapaa vizuri sana. Mipango mizuri inayotekelezwa inaongeza uchumi na inapunguza mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mipango mingi baadhi ya mipango ya 2017/2018, 2016/2017 imeanza kutekelezwa kwa uzuri kabisa. Tumeona *standard gauge* ya *central line* ikianza, tumeona ndege *bombardier* zikianza kuingia, tumeona umeme kule Rufiji - Ruaha ukianza, kwa kweli inatia matumaini na tumeona bomba la mafuta ambalo linatoka kule Hoima - Uganda mpaka kwetu kule Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitu hivi kwa mfano kama Bomba la Mafuta la Tanga la kutoka Hoima mpaka Tanga inabidi tuongeze thamani yake, *value addition*. Kwamba bomba hili sehemu zote ambazo litapita watafaidika namna gani, kuna mipango gani ambayo ipo ya kusaidia kuona kwamba linaweza kuongeza thamani kwenye maeneo yote ambayo bomba hili linapita na wananchi ambao watafaidika ambao bomba hili linapita wanafaidika kiasi gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye huu mpango sioni *central line*, sioni mpango wowote wa kuanza kutengeneza SGR ya *central line* na nimeangalia kwa makini, lakini sijaona. Naamini kabisa kwamba *Tanga line* pamoja na *central line* zikienda *simultaneously* basi tunaweza tukapata mendeleo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi juzi Rais alikuja Tanga na aliambiwa tatizo hili na akaamuru bandari iongezewe fedha. Nilikuwa naona kwamba tusingoje mpaka Rais aje kwa sababu nchi ni kubwa, lakini ninyi Mawaziri mnapaswa kumsaidia kwenye maeneo yale ambayo ni muhimu. Sikuona namna ambavyo Kiwanja cha Ndege cha Tanga kinaweza kupanuliwa na sijaona namna ambavyo *bombardier* imeelekezwa kutua katika Kiwanja cha Ndege cha Tanga kwa sababu sasa hivi kutakuwa na hekaheka nyingi sana. Naomba Waziri aliangalie hili kwa makini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Tanga *line* nakumbuka kikao kilichopita tulikubaliana kwamba aliyefanya upembuzi yakinifu atalipwa fedha zake na akilipwa fedha zake basi mpango huo utaingia kwenye *PPP*. Wapo wawekezaji kutoka Marekani ambao wameshughulika sana kupata huo mchoro ili waanze kuleta mapendekezo ya kuanza kutengeneza Tanga *line*, lakini mpaka sasa mchoro huo unakuwa ni hadithi. Kwa hiyo, naomba kabisa Waziri a-*take note* kama tuliamua kwamba msanifu alipwe kutokana na Mfuko wa Reli basi alipwe mara moja ili huo mchoro upatikane na tuanze kuuza hiyo biashara kutengeneza Tanga *line* mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza katika bajeti iliyopita, hili suala la *PPP*, suala la *road toll*, duniani kote sio Marekani, Ulaya na baadhi ya nchi hapa Afrika wanatumia *road toll*. Hizo nchi ambazo zimeendelea zinatumia *road toll* sisi kwa nini hatutaki kutumia *road toll*? Naamini kabisa mapato ambayo yatapatikana kwenye barabara...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba mpunguze sauti tumsikilize mchangiaji, zungumzeni taratibu.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mapato ambayo yatapatikana kwenye barabara ni makubwa na mfano upo wa Daraja la Kigamboni ambalo limeingia *PPP* na *NSSF*, mapato ambayo yanapatikana pale Kigamboni yangeweza pia yakapatikana kwenye barabara zetu kama tungeanzisha mpango wa *road toll*. Naamini kabisa kama Mataifa

makubwa wanatumia *road toll* kwa nini hapa tusitumie, tuna tatizo gani? Mheshimiwa Mpango naomba kabisa hili suala aliangalie kwa makini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji tumelizungumza na kila mtu hapa ndani ana tatizo la maji, viwanda na kilimo haviwezi kupatikana bila maji. Kuna mpango upo wa miradi mikubwa 17, kuna mradi wa dola milioni 500 kutoka China lakini sasa hivi imekuwa ni hadithi tu tunaambiwa *financial agreement*, sasa *financial agreement* mpaka lini? Naambiwa *financial agreement* ipo Wizarani kwake Mheshimiwa Mpango. Naomba kabisa atakapokuja ku-*windup* atuambie kwamba hii miradi na hiyo *financial agreement* imefikia wapi, kwa nini haianzi? Mimi ni mdau na Muheza ipo kwenye huo mradi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo, ukiangalia ukurasa wa tisa tumeambiwa kuna ongezeko kutoka asilimia 2.7 mpaka 3.1, hili ni ongezeko dogo sana. Naamini mkazo mkubwa tungeweka kwenye kilimo sasa hivi tungeweza kuwa mbali sana. Mheshimiwa Mpango ningependa sana wataalam wa kilimo watembelee hata hapo Zimbabwe na *South Africa* ili waone mashamba ya kisasa ambayo yapo, waone *system* za umwagiliaji ambazo zinatumika kule *boreholes* na kadhalika, unakwenda kwenye shamba wewe mwenyewe hutaki kutoka kwa raha ambayo unaoina pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakwenda kwenye shamba unakuta kuna viwanda vidogo vidogo kama tumbaku hii ambayo tunasema wanakausha, wana viwanda vidogo vidogo ndani ya mashamba. Tumbaku ikitoka pale inakwenda moja kwa moja *airport* na maua yakitoka shambani yanakwenda moja kwa moja *airport*. Vitu kama hivi ndiyo vya kujifunza, naamini kabisa kwamba tutakapopeleka wataalam na Serikali ikiweka nia kwenye kilimo tutakuwa mbali sana.

Mheshimiwa Spika, hapa juzi nchi moja hapa chini tu walitoa bure mbolea na mbegu wakawapa wakulima na mazao ambayo wamevuna huwezi kuambiwa kwa sababu

yale mavuno yalikuwa ni mengi mwisho ikabidi wawauzie *WHO*. Kwa hiyo, vitu kama hivyo ni muhimu sana kuweza kujua kwamba unawawezesha wakulima, unawapa mikopo ya vifaa vya kisasa, hatuwezi kuendelea kulima na jembe mpaka leo, kuna ma-*harvester* na kila kitu.

Mheshimiwa Spika, hapa kamati yangu ilikwenda Songwe, Mbeya kule, wapo wafungwa wanasema hatuna trekta, hatuna vifaa tulateeni vifaa, Songwe ndiyo ambayo inalisha Mbeya yote ile, tulateeni vifaa tulime na ardhi ipo. Tukaweka kwenye bajeti kwani walipata hata senti tano? Hivi ni vitu vya kuangalia kwa sababu vina umuhimu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna tatizo kubwa sana kwenye zao la chai. Kule Amani sisi tunalima chai sana lakini tatizo ambalo linajitokeza sasa hivi ni kwamba wale walimaji wanatakiwa wa-*export* hiyo chai moja kwa moja au waingie kwenye mnada Mombasa, hawaruhusiwi ku-*blend* wala ku-*pack*, *parking* na *blending* vyote vifanyike nje, sasa hii nini? Wanakwenda Mombasa kwenye mnada, Kenya wananunua chai yetu wana-*pack* Kericho, Kericho wanaleta chai hiyo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hili suala siyo sahihi tunasema tulime na tu-*dd value* sasa hawa hawaruhusiwi, ni suala la kuliangalia. Nimeongea na Waziri wa Kilimo na nime-*set appointment* naye ili tuweze kuona tutafikia wapi lakini ni muhimu suala hilo liangaliwe kwa umakini wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo na pamba, nchi kama Zimbabwe inalima pamba kidogo sana ukilinganisha na sisi, lakini *grade* ya kwake ni kubwa ukilinganisha na *grade* ya kwetu hapa. Ni kwa sababu ya utunzaji na ulimaji wake ambao unafanyika kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo nataka kuongelea ni la kuhamia Dodoma. Wizara zimeshamia Dodoma, Dodoma imeshakuwa makao

makuu lakini sijaona kwenye mpango namna ya kutengeneza huu Mji uonekane kweli ni makao makuu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miji mingi ambayo imehamiwa Serikali inakuwa na mipango, nenda Rwanda na Abuja kaangalie, wanakuwa na mipango kabisa wameshapanga kwamba wanajenga *site* fulani, wana-*prepare certain site*, wanaweka kila kitu nyumba na maofisi *everything*. Sasa hapa sijaona chochote kwenye mpango huu namna gani ambavyo tutaboresha Makao Makuu ya Dodoma iweze kuonekana kweli ni makao makuu kama nchi nyingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Adadi. Tunaendelea na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi na Mheshimiwa Sonia Magogo, Mheshimiwa Almas Maige na Mheshimiwa Edwin Sannda wajandae.

MHE. VEDASTUS M. MANYINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuweza kunipa nafasi na mimi niweze kuwa mchangiaji siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujalia kuwepo katika hii siku njema ya leo, lakini nampongeza sana Mheshimiwa Rais Magufuli kwa kazi yake nzuri anayoifanya. Ni ukweli usiopingika, wote tunayafahamu na hata yale ambayo yalikuwa ni mambo magumu ambayo tulikuwa tunadhani kwamba hayawezekani ameweza kuyatekeleza katika kipindi kifupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mfano suala la kuhamia Dodoma ilikuwa ni hadithi ya toka miaka ya 70 lakini ndani ya kipindi cha mwaka mmoja na huu wa pili tayari wote tumekubali na Serikali nzima imehamia Dodoma.

Vilevile kuna suala la nidhamu ya uwajibikaji, nadhani hilo ni suala ambalo halipingiki kila mmoja anakubali kwamba sasa ile nidhamu imekuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni sisi hawa hawa tulikuwa tunapenda kusema kwamba katika nchi hii wapo wale vigogo hawashughulikiwi wanapokosa lakini leo imedhihirika kwamba nchi hii ni ya kila Mtanzania, uwe mkubwa ama mdogo ukikosea sheria inafuata mkondo wake. Kwa hiyo, hiyo yote ni kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais amelifanya na jukumu letu sisi ni kuendelea kumwomba uzima katika hii kazi nzuri anayoendelea nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa maana ya uwasilishaji wake wa Mpango huu ambao ni wa 2018/2019. Nadhani ukiangalia katika ukurasa wa tano ameweza kusema vizuri kwamba yeye kama Waziri ameweza kutuletea sisi kama Wabunge tuweze kushauri lakini vilevile tuweze kutoa maoni kwa namna bora zaidi ya utekelezaji wa Mpango huu. Kwa hiyo, kumbe sasa ameanza na yale aliyoyaona kwamba yanastahili halafu ametupatia na sisi tuweze kuchangia kwa maana ya kujaziliza. Nikiangalia kuna ile Kamati ya Bajeti imeweza kusema mambo mazuri sana na katika hayo basi kazi yetu ni kuendelea kujaziliza pale penye ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa kwanza, pamoja na kazi kubwa na nzuri ambayo Serikali ya Awamu ya Tano imefanya lakini tuna tatizo moja kubwa kwamba Watanzania hali ya uchumi wetu imeendelea kudorora. Huo ni ukweli usiopingika karibu kila mmoja wetu ukimgusa iwe mkulima wa kawaida hali ya uchumi imekuwa mbaya, lakini hata wafanyabishara, biashara nyingi zimesimama na zimefungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia nini kinachangia haya yote, pamoja na vile viashiria vizuri vinavyoonesha kwamba uchumi wa nchi unakua lakini unapokuja kwenye uchumi wa mtu mmoja mmoja bado hali inaelekea kuwa mbaya. Hii moja, leo Serikali imezuia uuzaji wa mazao ya

chakula hasa mahindi na mchele. Kwa wale wenzetu ambao bahati nzuri wamebahatika kulima na wakavuna, Serikali imeweka mpango mzuri wa kuzuia kile chakula kisiende nje ili kije kitusaidie Watanzania, kumbe Serikali ilikuwa na kila aina ya sababu ya kununua kile chakula iweke kwenye maghala ya Taifa halafu iendelee kusambaza katika yale maeneo ambayo yana upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Spika, kilichofanyika tumemzuia asiuze lakini vilevile hatuko tayari kununua, kwa kweli hali hii tafsiri yake ni kwamba imeendelea kumpa yule mwananchi wa kawaida hali ngumu ya maisha. Kwa hiyo, hilo ni kati ya suala ambalo Serikali inahitaji ilianganalie na ione ni kwa kiasi gani inaweza ikawasaidia hawa wananchi wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumeambiwa na wote tumeendelea kufahamu kwamba mazao kama mbaazi hayana soko, lakini wale wakulima walishalima na wanayo kwenye maghala. Zao kama tumbaku halina soko, wakulima walishalima na tayari yapo kwenye maghala. Tafsiri yake ni kwamba lazima hali ya uchumi, ya kipato iendelee kuwa duni na maisha yao yaendelee kuwa magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika huu Mpango wa leo ambao umeletwa mbele yetu nami nina ushauri ufuatao. Ukiangalia katika nchi yetu zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania ni wakulima lakini pamoja na hayo huu Mpango haujasema unafanya nini katika kipindi kifupi na kirefu kuwasaidia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ushauri wangu leo wa nini kifanyike ni lazima tuwe na mpango na muda mfupi, wa kati na muda mrefu. Katika mpango wa muda mfupi leo ungeniuliza na kama Dkt. Mpango atakubaliana na ushauri huu ili ikiwezekana ndani ya mwaka kesho na mwaka keshokutwa tuanze kuona matokeo tena matokeo makubwa, hebu tutambue mabonde mazuri yanayostahili kilimo katika kila Mkoa.

Mheshimiwa Spika, mfano sisi pale Mara tunalo shamba lisilopungua ekari 20,000 linaitwa shamba la Bugwemu. Maeneo kama hayo yote tukiyatambua, kazi ya Serikali ni kuhakikisha kwamba kwenye hayo maeneo yote inapeleka maji, bahati nzuri tunayo *REA*. Kwa hiyo, tukiweka mkakati wa muda mfupi kwamba yale mabonde yote yatambulike na maji yaweze kwenda pale itasaidia sana na hiyo ni hatua ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya pili, ukiangalia vijana wengi leo wanaomba kwenda kujiunga kwenda JKT wakitegemea wakitoka hapo kwanza watapata mafunzo lakini kuna uwezekano mkubwa wa kuja kupata kazi. Sasa hebu tusiwafundishe zaidi kushika bunduki kule JKT, tuwafundishe zaidi kulima na kazi za mikono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokijua ndani ya kipindi kifupi, wale JKT tukiwawezesha vijana wengi wakaweza kwenda kule wakajifunza kilimo na kile kitakachopatikana na hicho kilimo kikaja kuwa mtaji wao kwa maisha ya baadaye watakapotoka pale waende kuanza maisha. Mimi naamini tatizo kubwa la chakula litakuwa limekwisha lakini hata hili ambalo linatuzuia kupeleka chakula katika nchi jirani kumbe tutakuwa tumezalisha chakula sasa ambacho kina soko kila mahali.

Mheshimiwa Spika, leo ukizungumza suala la mchele, katika nchi zote zinazotuzunguka mchele wa Tanzania una soko kubwa sana, lakini mchele wenyewe ndiyo huo wakitaka kupeleka hawaruhusiwi kwa sababu hautoshelezi. Kwa hiyo, tunadhani kwamba katika mpango wa muda mfupi, hiyo ni namna pekee inayoweza kutuwezesha au kuwawezesha watu wetu wakaweza kupata kipato ambacho kinaweza kikawasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hebu tuone namna ya kuendelea kuisaidia *SIDO*, kuendelea kuiongezea uwezo ili itoe mafunzo kwa watu wengi zaidi. Mnajua kwa bahati mbaya sana yawezekana hili wengi hatulifahamu, bidhaa nyingi kinachotakiwa ni ile *packaging*. Labda nitoe mfano

mdogo, ukienda pale sokoni utakuta kuna ile asali ya Pinda, kwa jinsi ilivyokuwa *packed* ile robo kilo bei yake ni zaidi ya kilo nzima ya asali inayotoka Tabora. Kumbe kilichofanyika pale ni *packaging* na utalam huo *SIDO* wanao, kwa hiyo wanaweza kuwafundisha watu wengi zaidi na wakawafanya watu wengi zaidi wakapata ujuzi na wakawa wanafanya *packaging* ya bidhaa mbalimbali tulizonazo na wakawa wanajipatia kipato kizuri na hata katika masoko ya *export*. Kwa hiyo, tunadhani kwamba *SIDO* yetu tukiendelea kuisaidia basi nayo itatusaidia zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa muda wa kati, kati ya eneo ambalo nadhani tunahitaji kulifanyia kazi ni pamoja na elimu yetu. Leo tumesikia hapa juhudi kubwa tuliyonayo ni kuhakikisha kwamba mikopo inapatikana, vijana wetu wanamaliza vyuo vikuu lakini tumesahau kwamba tuna tatizo kubwa leo la kuwapatia hao vijana ajira. Maana masomo mengi wanayoyasoma baada ya pale uwezo wa kuwaajiri hatuna. Kwa bahati mbaya vijana wengi wa Kitanzania huko nje wanashindwa kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda duniani kote, kila ukikutana na watu weusi watatu wanafanya kazi mahali popote pale duniani, wawili lazima utamkuta ni Mkenya, sanasana utamkuta ni Mganda lakini kwa Watanzania ni wachache sana. Hiyo tafsiri yake ni nini? Ni kwamba inaonekana kumbe ile elimu tunayoitoa haiwapi nafasi kubwa ya ushindani wa ajira katika masoko ya nje. Kwa hiyo, leo watoto tunawasomesha, wanamaliza chuo halafu wanarudi hapa sasa hakuna ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini kifanyike? Hebu tuangalie namna ya kuboresha vyuo hivi vya kati. Wale wanaomaliza kidato cha nne, wanaomaliza kidato cha sita, tuongeze hivi vyuo vya *VETA* na vyuo vya ufundi ili wanafunzi wengi zaidi wapate ujuzi. Tunadhani kwa kufanya hivyo itawafanya sasa hao vijana wajaajiri wao wenyewe. Kwa utaratibu tulionao wanafunzi wengi wanasoma *sociology* na *political science*, maana yake ni kwamba wakimaliza

tunaendelea kukaa nao mitaani. Kwa bahati mbaya sana unakuta kuna baadhi ya wanafunzi wamemaliza chuo kikuu lakini anazidiwa na aliyemaliza kidato cha nne akaenda VETA kwa sababu yeye tayari anao ujuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunang'ang'ana na tunajitahidi kusomesha lakini naamini kwamba baada ya muda tutafika mahali tunatengeneza bomu kubwa na tunayo mifano ya nchi. Ukienda kwenye nchi kama Nigeria, ni kati ya nchi ambazo zina wasomi wengi lakini walioajiriwa huko duniani ni wachache. Sasa inaonekana huo ndiyo mfumo wa elimu tuliona. Kwa hiyo, nina imani kwamba kama hatukuuangalia vizuri basi itatusumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo lingine ambalo tunahitaji kulifanya, ukiangalia kwetu sisi Tanzania ni kati ya nchi ambayo ina madini kushinda nchi nyingi, inashinda Kenya, Uganda, Rwanda, karibu nchi zote zinazotuzunguka. Cha ajabu unakuta katika nchi kama Kenya wana-*export* zaidi madini kutushinda sisi na hizo nchi nyingine zote hizo za Rwanda, lakini haya tunaendelea kuyasema mwisho wa yote yanabaki kama yalivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hatuna udhibiti kamili...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. VEDASTUS M. MANYINYI: Muda umekwisha?

MWENYEKITI: Muda wako umemalizika Mheshimiwa.

MHE. VEDASTUS M. MANYINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono Mpango. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Vedastus Manyinyi. Tunaendelea na Mheshimiwa Sonia Magogo, Mheshimiwa Almas Maige, Mheshimiwa Edwin Sannda na Mheshimiwa Aeshi wajiandae.

MHE. SONIA J. MAGOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kuwa na afya njema mpaka wakati huu na kuweza kusimama mbele yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kukishukuru Chama changu cha Wananchi CUF chini ya uongozi mahiri wa Mwenyekiti wetu, Profesa Ibrahim Haruna Lipumba, akisaidiana na Naibu Katibu Mkuu, Mheshimiwa Magdalena Sakaya. *(Makofi/Vigelele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitakuwa sijafanya busara kama sitalishukuru Bunge lote kwa kutupokea vizuri na kutupa ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeupitia Mpango wa Mheshimiwa Waziri, kwa kweli Mpango uko vizuri. Pamoja na uzuri wa Mpango huo, nami ninayo machache ambayo natamani yaingie au yatiliwe mkazo katika Mpango ambao upo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza kabisa ni suala la lishe. Katika Mpango huo sikuona kama suala la lishe limetiliwa umuhimu sana kama lilivyo katika jamii yetu. Kila mtu anafahamu umuhimu wa lishe na hata sisi tusingekuwa hapa kama tusingekuwa na afya njema na kupata lishe iliyo bora. Hivyo, naishauri Serikali ilianganalie sana suala la lishe. Iziwezeshe taasisi ambazo zinahusika na suala la lishe ili wananchi wapate elimu na kuelewa umuhimu wa lishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tuna utajiri wa vyakula na kama wananchi wangepata elimu ya kutosha, tusingekuwa na watoto wanaozaliwa wakiwa wamedumaa akili. Hivyo, naishauri Serikali itilie mkazo kwenye suala la lishe kwa sababu kuna usemi unasema *prevention is better than cure*. Kwa hiyo, naishauri Serikali i-stick katika kuepusha maradhi kwa kizazi kilichopo na kijacho kuliko kusubiri tumeshapata matatizo tunanunua dawa kwa pesa ambazo zingesaindia kwenye vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa viwanda, kitu cha kwanza napenda tujiulize ni kwa nini vile viwanda vilivyokuwepo vilikufa. Je, zile sababu zilizosababisha vile viwanda vikafa leo hazipo tena? Kama zipo tunafanyaje ili kuhakikisha kwamba viwanda hivyo ambavyo vinakwenda kuanzishwa tena havitakuwa na vitakuwa endelevu? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano suala la malighafi. Naishauri Serikali ijiandae vizuri kwenye suala la malighafi kabla ya kuanzisha viwanda vingi. Tulikuwa na mazao ambayo sasa hivi tunaona yameshuka ama mengine hayapo kabisa, kama mazao ya mkonge, pamba na michikichi. Kwa hiyo, naishauri Serikali, kabla hatujaenda kufungua viwanda vingine zaidi tuangalie uwepo wa malighafi ili viwanda hivyo visije vikaenda na vyenyewe vikafa kama vile ambavyo vilikufa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuangalie *workforce*, je, *workforce* iliyopo inatosha kwa hivyo viwanda ambavyo tunahitaji kuvianzisha? Elimu ikoje kwa wale watu ambao wanakuja kufanya kazi kwenye viwanda hivyo, ujuzi wao ni kiasi gani katika kuendesha viwanda hivyo? Kwa sababu kama tukiwa hatuna *workforce* ya kutosha hivyo viwanda na vyenyewe vitakwenda kufa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni mitaji, nauliza Serikali imejipangaje kwa suala la mitaji ya kuendesha viwanda hivyo. Je, tumeiandaa vipi Benki yetu ya *TIB* katika suala hilo la kuendesha viwanda? Kama tunategemea watu binafsi, je, Serikali imejiandaa katika kukusanya kodi kuhakikisha kwamba kodi zetu hazipotei na zinapatikana kwa wakati muafaka na kuendeleza Taifa letu kama tulivyopanga? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kugusia suala la elimu, natamani kuona Serikali ikiwa imetilia sana mkazo kwenye suala la elimu hasa elimu ya msingi. Watoto wanajazana kwenye madarasa na pale hatutegemei *ma-engineer*, *ma-doctor* wala Wabunge na Mawaziri ambao watakuwa na akili tulivu kama tulivu sisi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wetu tumesoma kwenye shule za kulipia lakini *population* kubwa iko kwenye shule zile ambazo tunaita za kata, lakini ukiangalia wale watoto mazingira wanayosomea ni magumu sana, hata wale Walimu wanaowafundisha hawapati ile motisha ya kutosha kuweza kuwahudumia wale watoto. Hivyo, naishauri Serikali iangalie kwa sababu msingi wa elimu unaanzia chini, hata sisi tusingekuwa na msingi mzuri mimi na wewe leo tusingekuwa hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuangalie elimu zinazotolewa kwenye vyuo vyetu. Wasomi wengi wanatoka vyuoni lakini wanakuwa kama wame-*cram*, ukimpeleka kwenye kufanya kazi ile aliyoisomea, hawezi. Kwa hiyo, tuangalie ile *quality* ya elimu inayotolewa katika vyuo vyetu na inatolewa kwa namna gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tutoe elimu ya ujasiriamali hasa kwa vijana. Vijana wengi wanamaliza vyuo wakiwa na *mentality* ya kwamba nakwenda kuajiriwa Serikalini. Tunaweza kuwajengea uwezo kuanzia chini ya kwamba sio lazima kila mtu aajiriwe, unaweza kujajiri na ukawa na maendeleo zaidi hata ya yule mtu aliyeajiriwa. Hivyo, naiomba Serikali iangalie sana juu ya elimu ya ujasiriamali kwa vijana na vilevile kuwawezesha mitaji pale wanapopata hiyo elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila aliyesimama hapa aligusia suala la maji. Mimi pia naomba nichangie kuhusu maji. Maji imekuwa ni tatizo kubwa katika nchi yetu, kuendesha viwanda kunahitaji maji, shughuli zote maofisini zinahitaji maji, hospitali zinahitaji maji na shule zinahitaji maji. Hivyo, tunaomba sana Mpango huu utilie mkazo suala la maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi vijijini wanateseka sana na suala la maji. Kama mwananchi ananunua ndoo moja ya maji kwa Sh.1,000/= kijijini, je, ana uwezo kweli wa kuhimili maisha yake? Kwa sababu tunajua kipato cha wananchi wa chini, wale wa vijijini, lakini kama anatakiwa

kununua ndoo moja ya maji ya Sh.1,000/= kwa siku maisha yake yanakuaje? Naomba sana na hilo litiliwe mkazo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi kukazia kwenye bomba la mafuta linalopita Tanga. Huu ni mradi mkubwa sana unaopita mkoani kwetu. Naiomba Serikali iwasaidie wananchi wa Tanga kupitia mradi huu waweze kunufaika zaidi kwa kuwapa elimu na vitendea kazi na kuwapa kipaumbele hata katika zile ajira ambazo zinatokea ili kuinua uchumi wa Mkoa wa Tanga. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Sonia kwa mchango wako na kwa kuishauri Serikali. Tunaendelea na Mheshimiwa Almas Maige.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniruhusu na mimi nichangie Mpango huu wa Maendeleo unaopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa vile natoka Mkoa wa Tabora siwezi kuanza vyovyote kwa sababu siasa ya Tabora ni tumbaku. Ndiyo maana kila Mbunge aliyesimama leo hapa ameongelea tumbaku. Kilimo cha tumbaku kimetulea Tabora kwa miaka 50 iliyopita lakini tukio la sasa la tumbaku kutonunuliwa limekuwa tatizo. Wakulima wa tumbaku ambao walitakiwa wauze tumbaku miezi sita iliyopita leo wanayo tumbaku ndani ya maghala na matokeo yake hawana chakula wala mavazi, watoto wa shule wamefaulu, wengine wamepewa ufadhili wa kulipiwa vyuo vikuu, wameshindwa kulipia ile *registration fee* lakini pia hata kuwasafirisha wameshindwa, pia kuna wagonjwa wameshindwa kutibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatusaidia sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuja mara mbili ameongea na wakulima, ameongea na wanunuzi wa tumbaku. Mimi

nimefanya kazi ya kukutana na wanunuzi wote watatu wa tumbaku, *TLTC, Alliance One* na *GTI*. Wote hawakuwa na bajeti ya tumbaku iliyolimwa kwa mwongozo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwepo Morogoro wakati Serikali iliposema wakulima limeni tumbaku, itanunuliwa. Wamelima tumbaku nje ya makubaliano ya makampuni yale ya ununuzi, tumbaku ile ndiyo ilikuwa tegemeo la wakulima ambao wengine walikuwa hawajalima, wanakopeshwa mbolea na vyama vya ushirika vikuu *WETCO*, sasa hawawezi kuuza tumbaku, walikopa mabenki, wanauziwa mali zao, hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, Makampuni haya hayakuwa na bajeti ya tumbaku ya ziada, yamejikunakuna, yamejivuta, mimi sitetei makampuni lakini nasema kama biashara, wametafuta hela za ziada, wako tayari kununua tumbaku kwa dola 1.25, Serikali imewapangia bei ya dola 1.75, hawana hela hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoka kutembea kwenye Jimbo langu lote la Tabora Kaskazini wananchi wako tayari kuuza tumbaku hata kwa dola 1 ambayo ni sawasawa na Sh.2,250 kwa kilo, Serikali imekataa. Sasa wananchi hawataki hata kumwona Waziri wa Kilimo kwa sababu ameleta chuki kubwa sana. Kwa nini Serikali isiruhusu wananchi hawa wauze tumbaku kwa sababu tumbaku sasa baada ya mwezi mmoja itakuwa haina thamani tena. Tumbaku itakuwa imeoza, itakuwa imeharibika na imekuwa nyepesi, haina thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala hili la tumbaku Serikali imeona kila Mbunge wa Tabora akisimama anaongelea tumbaku, sisi sio wajinga, tuna uchungu, tunahurumia wananchi. Mimi nikienda jimboni nafukuzwa, simu yangu imejaa maswali tumbaku inanunuliwa lini na sina majibu. Serikali kama ina huruma kweli kwa wakulima tofauti ya bei ambayo Serikali inataka wanunuzi wanunue dola 1.75 na wanunuzi wako tayari kununua kwa dola 1.25, Serikali itoe ruzuku ya senti 50 kwa tumbaku iliyopo ya kilo milioni

14.7, thamani yake ni shilingi bilioni 15. Basi itoe ruzuku hiyo kwa wakulima ili waweze kuuza tumbaku iliyoopo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumbaku imekuwa tatizo kubwa sana na Serikali ndiyo imekamata kwenye mpini. Wananchi wanasikitika sana, wanailaumu Serikali kwa nini imezuia. Kwanza tumbaku wameilima wao wenyewe, wamekopa mikopo wao wenyewe, wanataka kuuza hata kwa dola moja, makampuni yametoa dola 1.25 kwa nini Serikali inakataa? Maana kuna mwaka wa hasara na faida, tukubali wakulima wa tumbaku safari hii tupate hasara lakini itakuwa hasara zaidi kama mwezi mmoja utapita bila kununua tumbaku hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya tumbaku, lipo suala ambalo tunafikiri ni zuri sana. Serikali imefanya kazi nzuri sana ya kujenga reli ya *standard gauge*, lakini bajeti inayowekwa kwenye *standard gauge* ni ndogo, itachukua muda mrefu sana kuja kufika Tabora. Tuna habari kwamba imefika mpaka Morogoro, inawezekana ikafika mpaka Dodoma lakini kuja kufika Tabora kwa bajeti hii ya kusuasua hatuwezi kumaliza hiyo *standard gauge*. Ni wazo zuri, ni mpango mzuri lakini tufanye mpango wa kumalizia, siyo mpango wa kwenye makaratasi halafu hauishi. Nakumbuka tulipanga mwaka mmoja uliopita na leo reli haipo hata kilometa 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala zuri pia la anga. Tabora tunajengewa kiwanja kipya cha ndege lakini vilevile tunajengewa na jengo la wageni, hii ni hatua nzuri sana. Hata hivyo, lipo tatizo, uendeshaji wa Shirika hili la Ndege mimi sidhani kama tuko kibiashara zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo pia tatizo la ndege zetu kukamatwa huko nje. Mimi nalijua suala hili kwamba Shirika la Ndege halikuweza kununua ndege zake kwa sababu ndege yetu yoyote ambayo ingeruka nje ingekamatwa. Tunapenda kujua, ndege ambayo imekamatwa huko nje inakuja? Serikali iwe wazi iseme ndege inakuja lini ili wananchi tuendeleo kushangilia mafanikio ya anga. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mradi wa bomba la kutoka Uganda kuja Tanzania, ni mradi mzuri ambao Serikali na wananchi wote tunashangilia kwa sababu bomba hili lilikuwa na ushindani na jirani zetu. Kwa hiyo, mafanikio haya tunayapongeza, ni jambo zuri, Serikali imepambana na kupata mradi huu ambao utaleta faida. Kwanza kupitisha mafuta tutapata hela lakini italeta ajira kubwa kwa wananchi ambao watajenga bomba hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la miundombinu, nashukuru sana pia kwamba barabara sasa zitajengwa lakini katika barabara za mikoa ipo barabara ya kutoka Tabora kwenda Mambali inaunganisha Shinyanga, ipo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi lakini sioni utekelezaji wake ukitokea, hata upembuzi wake hakuna. Ilikuwa ni hadithi tu au kweli barabara hii itajengwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ikijengwa itasaidia kuunganisha Mikoa ya Tabora na Shinyanga. Pia ipo kwenye *corridor* ya mazao, kwa hiyo barabara hii kwetu ni muhimu sana kwa watu wa Tabora, Bukene na Shinyanga. Katika Mpango huu siioni barabara hii. Naomba Serikali itakapojibu ituambie barabara hii ya Tabora – Mambali imo au haimo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *REA*, nimeshangaa sana, nimetembea jimbo zima siioni *REA* na *REA III* tumezindua Sikonge kule, kwenye jimbo langu mbona simwoni mkandarasi, yuko wapi, kimetokea nini, kiini macho gani? Wananchi wananiuliza *REA* vipi Mheshimiwa Mbunge wetu, sina jibu. Serikali ituambie hatua kwa hatua utekelezaji wa kuweka umeme vijijini, ni muhimu. Sisi kule tumbaku tunalima halafu tunakausha kwa kukata miti, ili kulikimbia jangwa tukausha tumbaku kwa umeme.

Mheshimiwa Spika, tunaomba *REA* iwe na mpango ambao unaeleweka sasa hatuelewi *REA* inaenea kweli vijijini au ilikuwa hadithi? Mbona imekuwa tofauti sana na ilivyoanza *REA I* na *II*, *REA III* imetokea nini, limetokea jini limemeza umeme, mbona hatuoni maendeleo ya umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la elimu, licha ya kizungumkuti ambacho Mheshimiwa Waziri wa Elimu leo amekielezea hapa kuhusu jinsi ya kuwa-*sponsor* wanafunzi lakini mimi nina wanafunzi baba zao walifariki, nimeandikia Bodi ya Mikopo, mwaka jana wamekosa na mwaka huu pia wamekosa. Vigezo nimesikia hapa anasema moja ni kutokuwa na wazazi au uwe mwenye ulemavu, mimi nina wanafunzi wawili ambao nimechukua jukumu la kuwaandikia barua na kumwandikia Mkurugenzi wa Bodi ya Mfuko wa Elimu lakini wamekosa tena na hawana baba, mama hawana mtu yeyote wataenda wapi na wamefaulu *division one* wote lakini wamekosa, sasa mfumo ukoje?

Mheshimiwa Spika, kama kigezo ni kuwa yatima na hawa ni yatima wamekosa, kama kigezo ni kufaulu vizuri wamefaulu, kama kigezo ni masomo ya sayansi wamechukua sayansi tena mmoja alikuwa Chuo cha Sokoine akaondolewa. Nataka Serikali iniambie nikiwapa majina ya hawa wanafunzi wawili ambao wamefaulu vizuri na mmoja alikuwa anaendelea na masomo watampa mkopo na kwa nini walimpa mara ya kwanza halafu wamemkata na hana baba wala mama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ndiyo inayosomesha wataalam watakaofanya kazi viwandani. Kwa sababu ambayo sijui Waziri aliyepita na bahati mbaya alishafariki aliondoa elimu ya ufundi ambayo ilikuwa na mfumo wa kupata watu wenye *Full Technician Certificate (FTC)*. Kwa mfano, mtu alikuwa anatoka *Ifunda Technical, Dar Technical, Moshi Technical au Tanga Technical* kwenda Chuo cha Ufundi, miaka minne amechagua kozi ya umeme kwa mfano, anakwenda *Technical College* miaka mitatu anapata cheti cha *FTC*, lakini baadaye akirudi miaka mitatu anakuwa na miaka 10 katika *field* ile, kwa hiyo akienda kufanya kazi ni mtaalam aliyefaulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi bahati mbaya sana mfumo huo umevurugika wala hakuna anayejali. Matokeo yake ni nini? Hakuna mafundi viwandani, mafundi sanifu wenye *FTC* hawapo lakini Kanuni za Mainjinia wanasema kila

Mhandisi mmoja katika kiwanda anatakiwa asimamie *technicians* 25 sasa hao *technicians* hawapo na mainjina tunatoa wa *white colour*. Mimi watu wa *Engineering* wa *University* wanapochora maboksi (*Geometrical and Technical Drawing*) niliifanya *form one* na *form two* lakini sasa wanayafanya chuo kikuu wanatoka pale *white colour* hawana wa kuwasimamia, *FTC* tumeifuta.

Mheshimiwa Spika, napenda vyuo vya ufundi virudishwe lakini pia chuo cha ufundi kiendeleze kozi ya *FTC* inayotoa mtaalam wa fundi sanifu. Nashukuru Serikali imenisaidia hela jimboni kwa ajili ya *high school* ya Ndono na shule ya msingi lakini pia naomba kabisa kabisa mjaribu kurudisha mfumo ule wa Ujerumani wa *Technical Engineers na Academic Engineers*, hiyo peke yake ndiyo mkombozi wa watumishi viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora. Nililalamika humu ndani ya Bunge lako kwamba jamani kama Mahakama inaongelea kuweka Mahakama nyingi kila Kata au katika Kila Wilaya kule Upuge kwangu Mahakama imetelekezwa. Mahakama ya mwaka 1954 imefanya kazi mpaka baada ya uhuru na kuendelea lakini sasa imetelekezwa, majengo yake mazuri yako wazi, panya na nyoka wameingia, mwisho wakulima wamevamia wanakaa mle mwenye majengo mazuri.

Mheshimiwa Spika, palepale mbele yake kuna kituo cha afya hakuna Madaktari kwa sababu hakuna nyumba. Nikasema kama kulikuwa na sababu nzuri basi ya kuiacha hiyo Mahakama zile nyumba zitumiwe na Idara nyingine za Serikali na nillikuwa nalenga kituo cha afya.

Mheshimwa Mwenyekiti, kituo cha afya tunajenga vizuri, tumepata shilingi milioni 500 kukiboresha kwa kujenga wodi za wagonjwa lakini sasa Madaktari hakuna, hakuna nyumba na mita 500 kuna majengo ya Mahakama ambayo hayana kazi. Kwa bahati mbaya Mheshimiwa mmoja alijibu humu ndani kwamba Mahakama inafanya kazi jambo ambalo si kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikishaji wa sekta binafsi. Waziri Mpango amesimama juzi hapa akasema sisi tunajua injini ya uchumi ni sekta binafsi, injini gani haina mafuta? Mnasema ndiyo uti wa mgongo, uti wa mgongo hauna mfupa, hamuisaidii, sisi tumekuwa tunalalamika hapa ndani kwamba sheria zilizopo hazitupi *competitiveness* na jirani zetu, tukishindana tunashindwa katika ushindani, *tender* wanapata wenzetu, makampuni ya hapa yaki-*bid* yanashindwa kwa sababu ndani yake kuna kitu kwa mfano kinaitwa *SDL*. Sisi hapa Tanzania tunalipa *SDL* ya 4.5% ndiyo ya *highest* duniani.

Mheshimiwa Spika, muda wote waajiri tumeomba mtupunguzie *highest* ya *SDL* iko Kenya 1.2% lakini kwa ajili ya Idara moja tu ya Utalii kwingine kote hakuna, Uganda, Rwanda na Burundi hakuna, sisi tuki-*bid tender* za *international* maana lazima tuweke *SDL* tunakosa hizo *tender competitiveness* hakuna Tanzania. Sasa mnasema *private sector* ndiyo injini, injini gani bila mafuta?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Serikali haiko tayari kufanya *PPP*, nina mfano mzuri sana. Mimi baada ya kwenda Jimboni kwangu nikagundua kwamba watu hawana elimu kubwa sana kuhusu mambo yanayotokea duniani nikaamua kufungua kituo cha redio na kwa sababu Halmashauri ndiyo nailenga itumie kituo hicho nikaipa 30% kama *PPP*...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maige malizia sentensi yako.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Lakini tangu tumeingia ubia huo Halmashauri imeshindwa kupata kibali cha kuwaruhusu tufanye *PPP*. Kwa sababu lazima tupitie Kamati ya Fedha na Uongozi, Baraza la Wilaya, Baraza la Mkoa, Mkuu wa Mkoa, Waziri wa TAMISEMI, Waziri wa Fedha, Kamishna wa Bajeti ndiyo wapate kibali kwamba ingieni, imeshindikana, mwaka mzima sasa mradi umesimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali inaongelea *PPP*, naomba nimalizie....

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Maige muda wako umemalizika.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Edwin Sannda, baadaye Mheshimiwa Joseph Selasini na Mheshimiwa Agnes Marwa wajiandae.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue fursa hii adhimu kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima na afya leo tumekutana hivi wote katika dhima nzuri kabisa ya kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa 2018/2019. Pia nitoe pongezi kwa Serikali ya Awamu ya Tano ikiwa chini ya Mheshimiwa Dokta John Pombe Magufuli pamoja na timu yake nzima kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kufanya na sisi tukiendelea kuisimamia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika, nitoe pongezi kwa wenzetu walioaminiwa, walioaminiwa wapya lakini na wale ambao wameendelea kuaminiwa na Rais kwa uteuzi wa kushika nafasi za Mawaziri, Naibu wa Mawaziri lakini pia nawapongeza na wale ambao walibaki, tutaendelea kusimamia Serikali huku kwenye ukumbi huu wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, nitoe pongezi kwa Wizara ya Mipango na Fedha kwa Mapendekezo haya mazuri chini ya Mheshimiwa Dokta Mpango kama jina lako lilivyo lakini pamoja na pacha wangu Mheshimiwa Dokta Ashatu na Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara ya Fedha na Mipango. (*Makofi*)

Mheshimwa Mwenyekiti, kimsingi hotuba yenu ya Mapendekezo ya Mpango imekaa vizuri tatizo kubwa ambalo tumekuwa nalo ni kwenye utekelezaji. Kama ambavyo wameainisha kwenye hotuba yao wamechukua maoni kutoka kwenye jamii, taasisi za Kiserikali, Kamati ya

Bunge ya Bajeti ambayo hiyo unaipata kwenye hotuba yake ukurasa wa nne *paragraph* ya saba lakini pia wameileta kwenye Bunge ili waweze kuchukua maoni.

Mheshimiwa Spika, tunawaomba sana kwamba uchukuaji wa maoni haya uwe wa ukweli. Tumeanza juzi tunakwenda kumaliza Jumatatu siku tano nzima Waheshimiwa Wabunge hawa kila mmoja kwa nafasi yake anatoa pale alipoona panafaa. Tukitoka kapa kwa maana ya uchukuaji wa haya maoni, kwa kweli tutakuwa tunapoteza maana nzima ya sisi kukaa na kujadili Mapendekezo haya ili yaje kuboresha mpango na bajeti siku za mbele. Tunawasihi sana wachukue maoni yetu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nataka niseme kwamba pamoja na uzuri wa Mapendekezo na tunatarajia Mpango utakuwa mzuri baada ya kuchukua *input* zetu, ni lazima tuweke mikakati madhubuti na inayotekelezeka ya kuhakikisha utekelezaji wa Mpango huu unakwenda. Tutachukua maoni lakini utekelezaji unakwendaje? Tuna mikakati gani inayotekelezeka ya kuhakikisha Mpango huu wa Maendeleo na Bajeti ya 2018/2019 utakuwa dhahiri, utakuwa *realized* kwa Taifa na utakuwa *realized* kwenye uhalisia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye maoni na ushauri wangu katika kuboresha Mapendekezo haya ambayo mmeyaleta mbele ya Bunge hili. Nia ni nzuri na nia ni kwamba tunakwenda kujenga, kuimarisha na kuendelea kukuza uchumi imara, uchumi endelevu, uchumi ambao tunataka tufike mahali tunasema *sustainable growing economy* na sisi tumepanga mpaka 2025 tuwe katika kiwango cha uchumi wa kati, ni lazima tuone tunakwendaje vizuri ili tufike huko kwenye hazima yetu.

Mheshimiwa Spika, Dhana ambayo tunakwenda nayo ni ya uchumi wa viwanda. Uchumi wa viwanda maana yake tunahitaji kufanya mapinduzi ya viwanda. Tumeyasikia

mapinduzi ya viwanda yamefanyika kwenye Mataifa mengine mbalimbali na hatimaye kweli wamefikia uchumi wa viwanda.

Mheshimwa Mwenyekiti, nia na madhumuni hapa ni kwenda kuongeza uzalishaji. Tumesikia wenzetu wamechangia kwamba mahali ambapo tunategemea sisi kukusanya au kupata mapato ya nchi ni kwenye vyanzo labda vilevile, tunahangaika na *tax base* ambayo kila siku inakuwa ni ileile, unakamua ng'ombe ambaye tayari labda hajaweza kuzalisha zaidi. Sisi dhamira yetu lazima twende kuzalisha zaidi tupate *surplus* ambayo mwisho wa siku tunaweza kuweka akiba na nyingine ikatusaidia kuongeza kipato kwa kuuza huduma na bidhaa ndani na nje ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema na kwenye maandiko haya yote yako vizuri kabisa kwamba tunataka kuweka viwanda ambavyo vitalishwa na rasilimali zinazozalishwa Tanzania. Ni sahihi kabisa, tungeweza kuzungumzia kila eneo na *products* zao wanazozalisha. Mfano kule kwetu Kondoza tunaweza kuweka kiwanda cha *edible oils*, kuna karanga, ufuta, alizeti kwa wingi kabisa na hii inaweza ikawa Kondoza lakini vilevile ikakamata Ukanda mzima wa Kati. Dodoma yote inazalisha alizeti vizuri kabisa, Singida majirani zetu wanazalisha alizeti, karanga, ufuta, tunapiga kiwanda kimoja cha kiwango kikubwa ambacho ni *double refinery*....

MBUNGE FULANI: Pale Singida.

MHE. EDWIN M. SANND: Sio cha Singida. Inaweza kulisha na kuongeza tija katika ukanda wote wa *edible oils*. Lengo kama ambavyo mmeliainisha ikiwa ni kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa kwenye maeneo yetu na kukuza mnyororo wa thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwakumbushe na kuzidi kushauri Wizara katika kuboresha haya Mapendekezo. Mapinduzi ya viwanda yatafanikiwa pale tutakapofanikisha

mapinduzi ya kilimo. Tunazungumzia malighafi zilizoko pale lakini bila ya mapinduzi ya kilimo haya mapinduzi ya viwanda yatakuwa ni hadithi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kuweka jihada katika kuhakikisha tunapata mbegu bora, kuhakikisha tunaweza kupeleka pembejeo kwa wakati, mikakati mingi sana ipo, lakini jambo moja kubwa ambalo nataka kuliwekea uzito leo hapa ni suala la kilimo cha umwagiliaji. Hiki kilimo cha mvua hata upeleke mbegu za namna gani, uwe na pembejeo za namna gani bila ku-engage kwenye *large scale farming* ambayo itakuwa inategemea *irrigation* tutakwama tu kupata mapinduzi ya kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nisisitize sana eneo kubwa ambalo lazima tuliwekee mipango ni hili la *irrigation* ambalo tumekuwa tukilizungumzia mara nyingi. Wizara ya Maji na Umwagiliaji ukiangalia bajeti yake kwenye upande wa *irrigation* ni ndogo sana. Hapa tunahitaji tuwekeze *heavily* kwenye *infrastructure* za *irrigation*, iwe kupitia mabwawa, kupita kwenye utaratibu wa matone (*drip irrigation*) au na mifumo mingine ya mito, mifereji na kadhalika lakini bila *irrigation large scale farming* itashindikana.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia *large scale farming* ndiyo italeta mapinduzi ya kilimo, tunazungumzia wakulima wakubwa lakini pamoja na hawa wadogo, wakitumia kilimo cha umwagiliaji tija yake ni kubwa, una uhakika wa *yield*. Tusipofanya hivyo tutakuwa tunakabiliwa na changamoto ya tabia nchi kila mara na hatimaye uhakika na usalama wa chakula na uzalishaji usiwepo, hata hivyo viwanda ambavyo tunataka malighafi tunazolima wenyewe ziende kulisha kwenye viwanda ikashindikana.

Mheshimiwa Spika, nawaomba sana Mheshimiwa Dokta Mpango na pacha wangu Dkt. Ashatu, na nawasihi sana ushauri huu wa kui-nvest *heavily* kwenye *scheme* na *infrastructure* ya *irrigation* ni jambo ambalo tukiweka hapo mkazo litatuondoa na tutafikia kwenye mapinduzi ya viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kwenye kufanikiwa mapinduzi ya viwanda nimezungumzia mapinduzi ya kilimo lakini vilevile tujiwekeze na tujikite kwenye kuzalisha wataalam wa ufundi. Amezungumza ndugu yangu hapa Mheshimiwa Maige, siku za nyuma nimewahi kuzungumza tulivyokuwa tunajadili Mpango 2016/2017 na 2017/2018 kwenye Bunge hilihili kuhusiana na *polytechnics*, kuzalisha wataalam kwa ajili ya kwenda kuviendesha na kuviendeleza viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumzia uchumi wa viwanda, wako wapi hao wataalam ambao wanakwenda kuwa wabunifu na kuvikuza viwanda hivyo kama kila mmoja anataka afanye kazi ya *white colour*. Vyuvo vilivyokuwepo awali, Chuo cha Ardhi amezungumzia mzee hapa *Dar Technical* vile ambavyo *products* zilizokuwa zikitoka kule zinatoka kwenda kufanya kazi ya ufundi. *Managers* ni wengine, watakuwepo mainjinia watapata *degree* na kadhalika lakini wanaokwenda kuendesha viwanda vile tunawazalisha wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwekeze kwenye *polytechnics*, vyuo vikuu vya ufundi, vya ufundi wa kati ma-*artisan* hawa, *technicians* wa *FTC* lakini pia na vyuo vikuu vya ufundi ambavyo wenzetu maarufu wanaviita *polytechnics* ili viweze kwenda kuzalisha wataalam watakavyovikuza na kuviendeleza viwanda hivyo. Haya ambayo nimeyaongea ya *polytechnics* lakini ya *irrigation* nadhani tukiyazingatia yatatusaidia sana kwenda kuleta tija kwenye Mpango huu ambao tutakuja kuujadili mwakani. Jambo lingine na la mwisho, huko mwanzo nimezungumzia kuongeza uzalishaji mwisho wa siku ina-*ripple effect* kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine na la mwisho nataka kuzungumzia kuhusu na dhana nzima ya uwezesaji wananchi kiuchumi. Sitagusa milioni 50 za kwenye Ilani kwa sababu nadhani huko siko tunakotaka kwenda, lakini basi tujikite kwenye kuwezesha *infrastructure* muhimu,

kutengeneza mazingira mazuri ya *micro-financing* ambapo wale wananchi wa kawaida wataweza kupata angalau nguvu kidogo ya uchumi *liquidity* ikaongezeka kupitia sijiwi SACCOS, kuimarisha mifumo ya VICOBA, *micro-finances* nyingine, kujenga na kuimarisha mazingira haya ili angalau mwananchi wa kawaida aweze kunufaika na mikopo au upatikanaji wa mitaji yenye masharti na gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira ya kawaida, yule mfanyabiashara pale Kondoza kijijini au mjini au mkulima ni ngumu sana ku-*access financing* kupitia *financial institutions* tulizonazo. Ni lazima tutengeneze miundombinu mizuri kabisa, tujenge mazingira ya kuwafikia hawa watu wa chini wakope kidogo kidogo ili waweze kujiinua kiuchumi wao wenyewe mmoja mmoja na hatimaye jamii nzima ya maeneo halisia na hatimaye Taifa kwa ujumla. Tutakuwa tumepiga uchumi jumla na tumepiga *micro-economy*, mwisho wa siku Taifa linakwenda mbele na kwa kazi kubwa zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Edwin Sannda. Tunaendelea na Mheshimiwa Aeshi na baadaye Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Agnes Marwa na Mheshimiwa Stanslaus Mabula wajiandae.

MHE. KHALFAN H. AESHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Mpango wa Mheshimiwa Dkt. Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza awali ya yote nataka niliweke Bunge sawa. Wabunge tulioko humu ndani tunatoka maeneo tofauti tofauti. Wako ambao wanatoka maeneo ambapo wanachi wanalima mahindi, karafuu, pamba au korosho. Ni wajibu wa kila Mbunge kuhakikisha anatetea maeneo anakotoka, lakini vilevile kuhakikisha anaitetea Tanzania nzima kwa ujumla kwa jambo analoliona haliko sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilisikia hotuba ya Mbunge mmoja akiponda Wabunge wengine wanaotetea maslahi ya wananchi wao. Imetokea na desturi mbaya sana ndani ya Bunge hili, wako watu wanaojifanya wao ni wema sana kuliko wengine, wako watu wanaojifanya wao wako karibu sana na viongozi wa juu kuliko watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya jana ya Mheshimiwa Musukuma kutupinga sisi Wabunge tunaotetea suala la wakulima wa mahindi lilitukera sana sana. Ukilala na mgonjwa utajua matatizo ya mgonjwa, inawezekana Mheshimiwa Musukuma anakotoka hakuna wakulima. Sisi tuna wakulima ambao tunatakiwa tuwatetee kwa nguvu zote, hili limetukera sana. Niwaombe tu Wabunge kama unachangia, changia yale unayoweza wewe kuyasema ndani ya Bunge usiwakere wenzako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye hoja sasa, nimepitia taarifa ya Mheshimiwa Mpango. Katika kurasa zake zote hakuna sehemu aliyomkumbuka mkulima na wenzangu wote wamechangia kuhusiana na kilimo lakini hawa wote waliotoka hapa, wale wote waliochangia suala kubwa linahusiana na kilimo na kilimo ndiyo uti wa mgongo. Asilimia 80 ya wananchi wa Tanzania ni wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo yanakera sana, Serikali haieleweki nini inafanya. Hili nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu alisimamie. Serikali inapiga marufuku mazao yetu tusiende kuuza nje lakini haina uwezo wa kuyanunua mahindi yale. Sasa ifike wakati mkulima huyo ambaye anatupa kura nyingi sana sisi, mkulima huyo ambaye anahangaika sana kuhakikisha Taifa hili halipati njaa, basi tumkumbuke na kuhakikisha kama tunazuia mazao yasiende nje, basi tuyanunue, lakini kununua hatununui, kuwaruhusu kuuza nje hatuwaruhusu, matokeo yake tunataka kuzuia mfumuko wa bei kwa kumuumba mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko wa kilo tano za mbegu ni Sh.12,500/= lakini leo gunia la mahindi ni Sh.25,000/

= mpaka Sh.30,000/= na mbolea ni Sh.65,000 mpaka Sh.70,000/=. Mkulima ili apate mbegu na mbolea ya heka moja anahitaji auze gunia zaidi ya 10, tunamwonea sana mkulima. Leo hii Mbunge mwenzangu alikuja na hoja akaomba mwongozo lakini kwa bahati mbaya alikosea Kanuni, kesho tutajipanga tena upya ili tuliamshe dude humu ndani, Wabunge tusimame kwa umoja kuhakikisha tunawatetea wakulima na Serikali ije na kauli kwamba kama imeshindwa kununua, basi iwaruhusu kuuza yale mazao yao. Kama tunaongelea Mpango wa Maendeleo na uchumi wa nchi ni lazima tuhakikishe tunamtetea na kumsaidia mkulima ili kilimo kile kiwe na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuja na kauli mbiu ya Kilimo Kwanza, wananchi wakafurahi sana, wakaunga mkono kauli mbiu hiyo, lakini leo tumekuja na kauli mbiu nyingine mpya ya viwanda. Hata hivyo, bila kilimo viwanda havipo, sasa sijui tunakwenda wapi. Kila nikipitia hii hotuba yote ya Mheshimiwa Mpango inahusiana na kodi tu, tunakusanya kodi, tutakusanya kodi, hao tunaowatoza kodi kila siku wamechoka sasa hivi hawana kiasi chochote cha kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri atusaidie, wako baadhi ya watu wanaoidai Serikali, wako wakandarasi wanaoidai Serikali lakini na Serikali inawadai kodi. Kuna tabia imejitokeza, huyo mfanyabiashara anayedaiwa kodi anazuliwa biashara zake, anauziwa vitu vyake wakati na yeye upande wa pili anaidai Serikali kwa nini wasikae chini wakapiga hesabu zao na mwisho wa siku kama anaidai Serikali imkate deni moja kwa moja kuliko kumfungia biashara yake na mwisho wa siku anapoteza dira. Sasa kama tunataka uchumi mzuri, basi tuhakikishe na hawa wanaotudai tunawalipa ili waweze kuendelea na biashara zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea uvuvi, katika mtu anayeteseka ni pamoja na mvuvi wa *Lake Tanganyika*. Mvuvi mmoja ana leseni zaidi ya 10 au 20, mvuvi huyo huyo akitoka Kirando akihamia wilaya nyingine anatakiwa akate

leseni mpya, boti hilo hilo moja la uvuvi lina wavuvi 12 kila mvuvi ana leseni na kila mvuvi anailipia. Sasa wavuvi wanahama wanatoka Wilaya ya Nkasi wataenda Wilaya ya Tanganyika, wakitoka Wilaya ya Tanganyika watakwenda Lagosi, kote kule mvuvi analipia leseni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unaweza ukamkuta mvuvi ana leseni zaidi ya 100, hivi tunakwenda wapi? Kwa nini tusiweke utaratibu wa mvuvi mmoja kuwa na leseni moja kwa sababu ziwa lile ni letu wote, ziwa ni moja hakuna maziwa mengine pale *Lake Tanganyika* lakini huyu mvuvi tunamwonea siku hadi siku. Ifike wakati kama tunataka kuinua uchumi wa nchi hii basi na huyu mvuvi aangaliwe kwa jicho lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimuulize tu Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hivi Mheshimiwa Waziri amesomeshwa na mtu gani? Ni mvuvi, mkulima, mfanyabiashara au mtoza kodi? Nataka akija hapa aje anijibu kama alisomeshwa na mkulima lazima awe na uchungu na wakulima, kama alisomeshwa na wavuvi atakuwa na uchungu na uvuvi na hatimaye kwenye Mpango wake humu angewaweka watu hawa akawapa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina wasiwasi inawezekana labda alisomeshwa na mtoza kodi maana humu ndani ni kodi, kodi; atakamua ng'ombe maziwa na hatimaye atakamua damu. Naomba sana akija kujibu hapa atusaidie, kwanza atuambie kama Serikali haina uwezo wa kununua mahindi iruhusu twende tukauze kokote tunakotaka. Huyu mkulima wanamwonea mno kila wakiamka wao ni kumbana tu lakini siyo wajibu wa mkulima kuhakikisha mwananchi hafi na njaa, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha wananchi wake hawafi na njaa, sasa sisi leo ni kumbana tu ooh bwana chakula kimepungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tumeshindwa na Zambia, mahindi yanatoka Zambia yanakwenda Kenya *on transit* hapa, sisi tumebaki tunatazama tu tunasema kuna

njaa, kuna njaa, kuna njaa. Naomba Waziri akija atuambie kama ana uwezo wa kununua mahindi atuambie atanunua mahindi, kama uwezo wa fedha hatuna turuhusu mahindi yaende yakauzwe nje kwa sababu nakumbuka kauli ya Mheshimiwa Rais ambaye sisi wote tunampenda na tunampigania alisema kwamba, mkulima auze mahindi kwa bei yoyote anayotaka, akiuza Sh.100,000/= au Sh.200,000/= sawa ni kama vile mvuvi au mfugaji ambaye hatumuingilii chochote kile kwenye mifugo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina uchungu sana na mkulima. Juzi Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alitudanganya hapa, Waziri huyu ni jeuri sana kwa sababu amesema ameanza kununua mahindi na sasa hivi wametenga shilingi bilioni 40 kuhakikisha mahindi yananunuliwa. Jamani mbona wanasema uongo kila siku? Hakuna hata chembe ya gunia moja lililonunuliwa kutoka Rukwa, Katavi na Mbeya halafu wanakuja kutuambia wametoa fedha za kununua mahindi, hivi kuna Mbunge asiyejua kinachoendelea ndani ya Jimbo lake? Nani? Kila kukicha ukiamka asubuhi meseji unazo kwa hiyo unajua kila kitu kinachoendelea ndani ya Jimbo lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini leo Waziri wa Kilimo anadanganya kwamba ametoa fedha za kwenda kununua mazao, hakuna fedha yoyote iliyotoka kwenda kununua mazao isipokuwa wamekopa shilingi bilioni mbili kutoka CRDB na hatimaye wamezipeleka Njombe na Songea, sasa kule Sumbawanga ni Tanzania au ni Tanganyika? Kule Katavi ni Tanzania au Zambia? Kwa nini wanakuwa na ubaguzi wa hali ya juu *at least* wangepewa kidogo kidogo lakini hatimaye mahindi hawanunui, wanawadanganya wananchi, wanakaa wanawabeza wakulima.

Mheshimiwa Spika, kama kungekuwa na uwezo wa kutoka na shilingi hapa ningetoka nayo, lakini kwa Mpango huu kesho tutakuja na ajenda nyingine hapa, tutakuja na Kanuni nyingine mpya ili kuhakikisha kesho Bunge linasimama pamoja kuhakikisha Serikali inatoa kauli ya kununua mazao yale au kuyarusu yaweze kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, naomba nisubiri majibu ya Mheshimiwa Waziri na baadaye naweza nikaunga mkono hoja au nisiunge mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Aeshi. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Selasini na Mheshimiwa Agnes Marwa, Mheshimiwa Stanlaus Mabula na Mheshimiwa Omary Mgumba wajandae.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie katika hoja hii iliyo mezani kwetu. Hata hivyo, kabla sijachangia, nataka nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na daima nitaendelea kumshukuru kwa uponyaji ambao amefanya kwa Mheshimiwa Tundu Lissu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu wale waliobahatika kumwona Mheshimiwa Tundu Lissu siku ambayo watu wasiojulikana walikuwa wamedhamiria kudhulumu maisha yake, wataamini kabisa kwamba uponyaji wake ni mpango wa Mungu. Ndiyo maana kwa kweli binafsi nikisikia tukio la kuumizwa Tundu Lissu likiongelewa kwa dhuhaka, kejeli, dharau kwa kweli linanikasirisha kupindukia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi baada ya Waziri Mkuu kujibu vizuri swali la Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Mlinga alikuja na mwongozo na uliojaa kejeli. Mwongozo ule ulimhusisha Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni na mauaji ya *albino*, jambo hili halikubaliki. Ombi au pendekezo la Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa Serikali kuhusisha Wachunguzi wa Kimataifa ni pamoja na baadhi ya matendo ambayo yamekuwa yakitokea katika nchi hii na kufumbiwa macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanakumbuka na sisi tunakumbuka kwamba, Mheshimiwa Goodluck Mlinga alihusishwa na kumuua mpenzi wa mpenzi wake. *(Makofi)*

T A A R I F A

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana Mheshimiwa Selasini. Tangu nizaliwe sijawahi kuhusishwa na kifo cha mpenzi wa rafiki yangu. Namwomba alete ushahidi katika Bunge hili ni nani alinihusisha.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini taarifa hiyo.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia na huo ni mkuki kwa nguruwe kwa binadamu mchungu. Gazeti la Dira liliandika vizuri sana kwamba mpenzi wako alikusaliti, wewe na kundi la vijana wenzako mkaenda kumuua, limeripotiwa Polisi, limeripotiwa kwenye magazeti na hujakanusha hadi hivi leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeiomba Serikali katika uchunguzi wa nani walihusika kutaka kudhulumu maisha ya Mheshimiwa Tundu Lissu, huyu ambaye alikwishatajwa kwamba alihusishwa na mauaji uchunguzi uanzie kwake. *(Makofi)*

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: *(Makofi)*

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Makofi yako inaonekana kwamba unakubali uchunguzi uendele. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini naomba urudi kwenye hoja tafadhali.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwenda kwenye hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo napenda kulizungumza ni kushauri Kiti chako. Jana kuna mwenzetu mmoja katika mchango wake alihusisha Bunge

hili na ubaguzi. Namshukuru sana *senator* Ndassa kwa jinsi alivyojenga hoja yake asubuhi na kututahadharisha kwamba tusije tukaigawa nchi kwa sababu ya hisia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hili kwa sababu nakuomba kama ikikupendeza *Hansard* ya jana ya hotuba ya Mheshimiwa Musukuma iangaliwe kwa sababu...

TAARIFA

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili lina uhuru wa kuongea chochote ambacho hakijavunja sheria na kwa kuwa Mheshimiwa Selasini amezungumza, baada ya jana kumaliza kuchangia hapa yeye na wenzie anawafahamu, mimi siyo mtu wa kuongea na nilikwambia jana, walinifuata kunitishia kwenye *parking*, sasa unayarudisha humu ndani, mimi siyo mtu wa kutishiwa na wala siogopi kusema humu Bungeni na nilikuwa sijasema na leo umeendeleza haya wakati hata asubuhi yametolewa mwongozo na Spika, sasa unayaendeleza maana yake yale uliyonifuata kwenye *parking* unayo, karibu. (*Makofi*)

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini, naomba uendelee.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi sijapewa taarifa na kwa sababu hiyo naomba niendelee kukushauri. Nashauri ile hotuba yake iangaliwe kwa sababu ndani ya ile hotuba kuna maneno haya ambayo ni maneno mabaya kama yataachwa kwenye ile hotuba kwamba, wakati mnakula vizuri sisi tulikuwa kimya sasa zamu yetu mnapiga kelele. Naomba kama haya maneno yako kwenye *Hansard* yaondolewe kwa faida ya vizazi vijavyo. Haya maneno siyo mzuri, haya maneno ni mabaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa niingie kwenye Mpango. Mimi simlaumu Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa hoja yake aliyoileta Mezani kwa sababu

wajibu wetu ni kumshauri ili baadaye atulettee Mpango. Namshukuru pia Spika kwa jinsi alivyotuweka sawa asubuhi. Mheshimiwa Mpango yuko hapa kutusikiliza ili tumsaidie aweze kuchukua hoja zetu, baadaye azifanyie kazi ili tuweze kuwa sasa na Mpango wenyewe. Mimi ninachoelewa kilicho mbele yetu ni Mapendekezo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuzungumza kuhusu gesi ambayo nchi hii inayo. Kamati ya Bajeti ilipata bahati ya kwenda Mnazi Bay na Msimbati. Gesi tuliyonayo ni nyingi kwelkweli, ni nyingi sana lakini hatuna uwezo wa kutumia robo tatu ya gesi tunayozalisha. Kinachotokea ni ukiritimba wa *TPDC* kwa sababu *M&P* ambao wanazalisha hii gesi wanaiuza kwa *TPDC* na wanaiuza kwa *TANESCO* Mtwara na ukiritimba huo unafanya sasa ile gesi isilete faida yoyote katika nchi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba kama mikataba ambayo Serikali iliingia na *M&P* ikirejewa vizuri ile gesi inaweza ikauzwa kwa makampuni mengine, inaweza ikauzwa kwa watu binafsi. Kwa kufanya hivyo uko uwezekano hata wa kupunguza mafuta ya mitambo ambayo tunaagiza kutoka nje, mafuta ya magari tunayoagiza kutoka nje na kuokoa pesa nyingi sana za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mataifa mengi sasa hivi yenye gesi magari yake yanatumia gesi. Gesi inatumika majumbani, hakuna sababu yoyote ya kutojengwa kwa vituo vya kuuzia gesi kama vile vituo vya *petrol*/na *diesel*/na kufanya magari yetu yakatumia gesi. Ni kitu kidogo sana tu kwa sababu katika gari utahitaji kuwa na mtungi tu kwa ajili ya gesi na kwa sababu hiyo tutaokoa pesa nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali ifanye kila linalowezekana ili gesi ambayo inazalishwa kwa wingi itumike katika uendeshaji wa magari na maeneo mengine na ikiwezekana *TPDC* sasa iweze kutoa *master plan* ya namna ambavyo gesi hiyo itafika katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa, Mikoa ya Kaskazini, Mikoa ya Nyanda za Juu hata na Mikoa

ya Kusini ili tuweze kuokoa uharibifu wa mazingira na vilevile tuweze kuokoa pesa nyingi sana za kigeni ambazo zinatumika kwa ajili ya kuagiza mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuzungumza ni kuhusu kilimo chetu. Zamani kahawa, pamba, mkonge, pareto na kadhalika ni mazao ambayo yalikuwa yanatuingizia fedha nyingi sana za kigeni lakini sasa hivi maeneo ambayo yalikuwa yanalima pamba zamani pamba hailimwi tena kwa sababu wakulima wanakata tamaa, maeneo yaliyokuwa yanalima kahawa hivyo hivyo na kadhalika na kadhalika. Sasa tunazungumza habari ya Tanzania ya viwanda lakini Tanzania ya viwanda itapatikana namna gani kama hatuwezi kuwahamasisha wakulima wetu tukapata malighafi. Naomba mpango utakapokuja uje na mkakati mahsusi kabisa wa namna ambavyo tutabadilisha kilimo chetu kiwe cha kisasa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kulikuwa na ule mpango wa *SAGCOT* ambao ulikuwa ni mradi mkubwa kabisa. Niseme wazi kabisa kwamba sipingani na mradi wa Stiegler's Gorge wala siko kwenye hoja ya *UNESCO* na mambo mengine, lakini nataka kusema wataalam wametafakari namna gani mradi wa Stiegler's Gorge na mwingiliano wa ule mkakati wa *SAGCOT* labda pengine ule mkakati umefutwa au namna gani. Kwa sababu yako mazao madogo madogo ukiacha haya mazao makubwa ya biashara ambayo yanaweza yakaibadilisha nchi hii. Tunaweza tukauza nje mananasi, maembe, nyanya na kadhalika na matokeo yake hivi ndiyo vitu vidogo ambavyo vinaweza vikafanya watu wa kawaida kuonekana kwamba Serikali inawajali na kipato chao kinaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kuhusu ujenzi wa reli yetu, hili ni wazo ambalo hakuna mtu hata mmoja ambaye anaweza akalipinga, tunahitaji reli kutoka Dar es Salaam kwenda Isaka, Kigoma, Karema, Tanga na Moshi. Hoja ni hii tutaweza kwa pesa zetu? Naomba Serikali iseme fedha za kujenga reli hii tunazipataje? Hizi fedha shilingi trilioni

16 kwa ajili ya ujenzi wa reli kuzibeba peke yetu kama nchi maana yake ni kuacha shughuli nyingine za huduma kwa jamii, ni lazima zitaathirika.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo nasema kama walivyosema wenzangu tusione aibu hata siku moja kushirikisha *private sector*. Wako watu duniani kama Serikali ikidhamiria miradi hii mikubwa tunaweza tukaingia nao ubia ikafanywa vizuri kabisa. Kwa sababu hii reli lazima iwe ya kibiashara kama sisi tutaamua kukopa reli ifike mpaka hapa Dodoma halafu tushindwe kuiendeleza lazima kama nchi tutafakari hizi fedha tutazirejesha namna gani kwa sababu ikifika Dodoma itakuwa ni ya huduma tu haitaweza kuwa ya biashara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima Mpango utakapokuja Waziri Dkt. Mpango atuambie ni maeneo gani ambayo yanaweza yakanyanyua uchumi ambayo tunaweza tukashirikiana na *private sector*. Eneo kwa mfano la ujenzi wa barabara, wamesema wenzangu wengine Mheshimiwa Adadi amesema kuna barabara nyingine ambazo Serikali haihitajiki kujenga sasa, kuna watu binafsi wanaweza wakajenga halafu wakaingiza *road toll*. Kwa hiyo, hii sheria ya *PPP* tusiiweke tu kwenye vitabu, tuangalie namna ambavyo itafanya kazi kwa manufaa ya nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulisema kuhusiana na hilo, tusiwanyanyapae wafanyabiashara. Wafanyabiashara wanalalamika na wanalalamika kwa sababu inaonekana kana kwamba Serikali inataka kurudi katika ukiritimba wa Serikali yenyewe kufanya biashara. Miradi ya ujenzi sasa inakwenda *JKT*inarudi Serikalini.

MWENYEKITI: Malizia sentensi yako Mheshimiwa.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuhakikishe kwamba tunai-boost *private sector* kwa sababu Serikali ndiyo yenye pesa ifanye ubia na *private sector*

ili wananchi waweze kunufaika kwa sababu *private sector* kwa kiwango kikubwa ndiyo inayotoa ajira kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Selasini. Tunaendelea na Mheshimiwa Agness Marwa.

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Mapendekezo ya Mpango. Kwanza kabisa, namshukuru sana Mheshimiwa Rais wangu kwa kutuhudumia Watanzania kwa upendo, kwa kweli ni chaguo la Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nirudi sasa kwenye Mpango nimeona wameongelea suala la afya. Kwenye suala la afya niishauri Serikali yangu, Serikali ya Chama cha Mapinduzi iangalie sana hospitali nyingi na hasa hospitali za rufaa ambazo hazijakwisha huko vijijini kwetu, wilayani na kwenye mikoa mingine kwa ujumla ili kuboresha huduma ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Hospitali ya Rufaa ya Kwangwa ya Mkoa wa Mara imekuwa ikisuasua kwa muda mrefu sana. Hospitali ya Kwangwa imekuwa ikijengwa tangu sijazaliwa mpaka leo inaendelea kujengwa, pesa yake inakuja kwa matone matone kama ya mvua. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali yangu iangalie sana suala la afya na kuangalia pia jinsi ya kuboresha zile hospitali zetu ndogondogo za wilaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika Mpango nimeona wameongelea kuhusiana na suala la maji, niiombe sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi iangalie sana hili suala la maji. Kama tulivyoomba Wabunge wengi na hasa Wabunge wanawake suala la kumtua mwanamke ndoo kichwani basi Serikali yetu katika Mpango huu ujao iangalie sana suala la maji kwa upana wake ili kusudi kumtua ndoo mwanamke kichwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika Mpango wameongelea mambo ya Serikali kwa ujumla kwa mfano kuna Mahakama, magereza na vitu vingine. Sijui kwa mkoa mingine kwa Mkoa wangu wa Mara kuhusiana na suala la Mahakama kwa kweli kumekuwa kuna shida sana na hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Wilaya ya Rorya kuna pesa ilishatolewa kwa ajili ya Mahakama lakini hadi sasa Mahakama haijajengwa hivyo kumekuwa na msongamano mkubwa katika Mahakama iliyopo Wilaya ya Tarime na kusababisha usumbufu na pia kuwasababisha wananchi wengi kushindwa kuhudhuria kutokana na umbali na kipato cha kwenda kule au nauli inakuwa ni ngumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala pia la magereza, magereza zimejengwa muda mrefu sana toka kipindi cha Mwalimu Nyerere. Hivyo tuangalie suala la magereza katika Mpango huu kwa nchi nzima kutokana na ongezeko la watu. Kwa mfano, Wilaya ya Tarime watu kipindi hicho walikuwa wachache sana lakini siku hizi kwa kweli watu ni wengi sana na tunazaliana kwa *speed* ya hatari, kwa hiyo magereza ya Wilaya ya Tarime kwa kweli hayatoshi kabisa watu wanabanana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niongelee suala la madini. Humu kwenye Mpango wameongelea suala la madini na sheria zake na mambo mengine. Katika madini tunaiomba Serikali au mimi Mbunge wa Mkoa wa Mara naishauri Serikali iangalie sana suala la kulipa fidia kwa wananchi ambao wanakuwa wamechukuliwa maeneo yao na wawekezaji waliowekeza katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, Kwa mfano, Mgodu wetu wa *North* Mara umechukua maeneo ya wananchi kwa muda mrefu sana kwa kweli, watu walikufa, wengine hawana pa kuishi mpaka sasa, wengine ni wazazi wetu, wengine ndugu zetu lakini hawana pa kuishi. Hivyo, niombe Serikali yangu ya

Chama cha Mapinduzi ifuatilie suala hili ili kuweka kwenye Mpango kuwalipa wananchi hao wa mgodini malipo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea haya kwa sababu nimemuona Mbunge wangu wa Tarime ambako ndiyo huko Nyamongo, Mheshimiwa Heche, yeye anawashwawashwa na uwanja wa ndege ulioko kwa Mheshimiwa Rais, anashindwa kuwaomba wananchi wetu walipwe fidia zao. Sasa yeye anatakiwa ajue kwamba wale wananchi wanahitaji yeye awatete siyo awashwewashwe na mikoa mingine kitendo ambacho kwa kweli siyo kizuri sana na ni kitendo ambacho hakikubaliki hata kidogo kwa sababu yeye alitaka uwanja wa ndege uende nyumbani kwake? Au ni kosa Mheshimiwa wetu Rais kuzaliwa eneo ambalo uwanja wa ndege umepelekwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwanza kutokana na Mpango hili suala nina imani kabisa limeangaliwa kwa undani zaidi, kwanza kurekebisha au kubana matumizi. Kubana vipi matumizi basi na wananchi wetu wanapaswa walisike hili. Ule uwanja ungepelekwa Shinyanga inamaanisha kwamba wananchi wangebomolewa nyumba, kwa hiyo ili kubana bajeti kule kulikuwa na maeneo ya wazi ni kwa nini uwanja usijengwe?

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mambo mengine tunapaswa na sisi kupeleka siasa mitaani siyo tulate siasa Bungeni. Kwa hiyo, niwaombe sana Wabunge wenzangu mambo mengine yanapokuwa ya heri tufurahie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nishukuru sana, sina zaidi ila nasema Mbunge wangu Heche asiwashwewashwe, awatete wananchi wa Nyamongo. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Agnes. Tunaendelea na Mheshimiwa Stanslaus Mabula na Mheshimiwa Omary Mgumba na Mheshimiwa Amina Mollel wajiandae.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili angalau niweze kusema kidogo juu ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa ili haya ambayo tunakwenda kuyachangia utakapokuja Mpango kamili tuweze kuona mabadiliko lakini tuweze kuona hiki tunachokizungumza kinakwenda kufanyika kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu tuko hapa ndani kwa sababu ya kuzungumza lakini kwa sababu ya kuleta hoja ambazo zitawasaidia Watanzania. Naomba nianze tofauti kidogo na kuanza kwangu nataka kuzungumza juu ya suala zima la uboreshaji wa miji, majiji lakini namna ambavyo tunaweza kushughulika na mambo ambayo yanaweza yakatusaidia sana kwenye sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimefurahi moja ya kati ya mapendekezo yaliyoko kwenye Mpango huu katika sekta ya ardhi inatambua na wajibu wake mkubwa ni kupanga, kupima na kumilikisha lakini tukifanikiwa kupanga, kupima na kumilikisha sisi wenyewe tunasema itakuwa ni sehemu nyingine ya mfumo wa uboreshaji na upatikanaji wa mapato mengi zaidi. Kwa nini nasema haya? Natambua Serikali inao mpango thabiti wa kuhakikisha maeneo ya Miji, Majiji, Manispaa na Miji inapimwa kwa kiwango ambacho kinastahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa upo mpango ambao unaendelea, mpango wa upimaji shirikishi ambao unamfanya mwananchi achange mwenyewe ili kuweza kupimiwa kwa sababu tu ya msingi kwamba maeneo mengi sana Serikali inatambua hayajapimwa. Liko tatizo moja hapa ambalo nilitamani sana kuliona kwenye Mpango humu ndani linawekewa mkakati thabiti.

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni kuhakikisha hii *premier* ambayo inatokana na ada zinazoongezeka katika kulipia hati inaondolewa ili mwananchi huyu aweze kupata nafuu anapokwenda sasa kuchukua hati yake kimsingi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kubwa sote tunafahamu mpango huu ukifanyika vizuri miji yetu mingi ambayo kiukweli ziko *squatters* za kutosha ikapimwa ikapangika na watu wote hawa wenye *squatters* wakishamaliza kupimiwa hizi ni fedha zingine ambazo Serikali inaweza kuzipata na zikatusaidia sana kwenye mapato. Kwa sababu ni ukweli usiofichika sasa hivi ziko fedha nyingi sana zinapotea kwenye kodi ya majengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale ambao wanasafiri na ndege ukipita kwenye Miji ya Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma, Arusha na miji mingine yote mikubwa unaweza kuona ni namna gani nyumba zilivyo nyingi lakini 70% ya nyumba hizi unaweza kukuta miji haijapangwa, nyumba hazitambuliki na badala yake hazilipi kodi.

Mheshimiwa Spika, sasa zoezi hili likifanyika vizuri sina shaka mwananchi mwenyewe atakuwa na uhakika na kile ambacho anakifanya lakini atakuwa na uhakika na makazi yake, lakini kubwa zaidi muda ambao kwa sasa Serikali imetoa na ndiyo mpango, kwenye Mpango ije ituambie huu muda utakuwa unakwenda kwa ukomo wa muda gani ili kuweza kusaidia wananchi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu sote tunafahamu hata Mpango tunaokwenda nao upatikanaji wa fedha wenyewe haukidhi mahitaji na muda uliowekwa na Serikali. Sasa kule tunakokwenda lazima tuseme kwenye Mpango tunatazamia tuwe na muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, yako maeneo ambayo yana milima, mimi natoka Mwanza, Jimbo la Nyamagana, watu wengi sana wamejenga kwenye milima na hawa hatuwezi kuwaondoa kwa namna yoyote ile lakini tukijitahidi tukawapimia, tukarasimisha maeneo yao waliyopo yana uwezo wa kutengenezwa vizuri na eneo hilo tukawa tumesaidia Serikali ikakusanya kodi wananchi wakaishi kwa amani na wakaendelea kushughulika na maisha yao ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, nilikuwa najaribu kupitia mpango huu sijaona popote, tulizungumza hapa juu ya urasimishaji wa biashara na wafanyabisahara ndogondogo, tunawazungumzia machinga, mama lishe, baba lishe na wengine wauza mbogamboga na matunda. Sasa kwenye mpango huu tunaoupendekeza sasa hivi hatuoni umuhimu wa kuweka wafanyabiashara hawa watengenezewe mkakati endelevu kuliko hivi walivyo sasa tutawaacha tu, tumesema wapewe vitambulisho, halafu miaka mingine inakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima tuhakikishe kwenye Mpango huu tunaoutafakari tuwatambue watu hawa vizuri, wawekewe misingi ambayo itawasaidia maisha ya mbele zaidi watoke hatua moja na kwenda hatua nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwenye miji yote mikubwa hii, kama ambavyo kwenye kitabu chenu mmesema, ukitoka miaka ya 1967 mpaka leo kuna zaidi ya ongezeko la watu zaidi ya milioni 13 tafsiri yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hili linapatikana kubwa sana kwenye miji. Kama hatualitengenezea mkakati endelevu wa kudumu tutakuwa tunacheza *mark time* na hatuwezi kuwasaidia wananchi hawa. Kwa hiyo, ningependa sana tuone mkakati wa wafanyabiashara ndogondogo kwenye nchi hii inakuwa ni endelevu na mazingira yao tunatafakari namna ya kuwasaidia ili waweze kuendelea kufanya biashara zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni mpango wa kuzifanya Halmashauri ziwe na uwezo wa kukusanya mapato. Sote tunafahamu kwenye mpango hapa tumeshaanzisha sheria ambazo zipo, zilikuwepo na nyingine tumezihuishia sasa hivi, namna ya ukusanyaji wa mapato mengi na makubwa yaende kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Hili sio jambo jipya toka mwaka 2005/2006 lilifikiriwa, lakini halikufanyiwa kazi, mkakati wa upangaji wa matumizi asilimia 30 na 40 tunayoizungumza sasa hivi tunafahamu, ziko

kodi zinaondoka kwenye Halmashauri zinakwenda kwenye Mfuko wa Serikali Kuu ikiwemo kodi ya majengo, ikiwemo kodi ya mabango na kodi nyingine kama tunavyoendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni lazima tutengeneze mkakati kwenye mpango tunaoutazamia kuziwezesha Halmashauri zote nchini ziwe na uwezo wa kuanzisha vyanzo vingine vipya vya mapato. Kwa mfano, watu wanafikiria kujenga *stand* za mabasi, watu wanafikiria kuwa na miradi ya masoko ambayo inaweza ikaleta fedha nyingi kama kodi, lakini wapi wanapewa fursa ya kufanya hivyo? Hii PPP tunayoizungumza inaanza kufanya kufanya kazi kwa wakati gani na msingi wake ni upi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tujenge msingi ambao utasaidia kuhakikisha kwamba, suala hili Halmashauri zinakuwa na uwezo. Mbali ya fedha hizi zilizoondoka, lakini nzina uwezo wa kujiendesha, zitapata fedha ambazo Madiwani watafanya vikao, Wenyeviti watalipwa na mambo mengine kadha wa kadha yataendelea, lakini Mheshimiwa Waziri wa Mipango hujalizungumza humu ndani. Ninaomba ulichukue na utakapoleta mpango kamili tuone namna ambavyo Halmashauri zimewekewa mkakati, ili ziweze kusimama na kujitegemea zenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nne naomba niizungumzie sekta ya afya. Sote tunafahamu kwenye sekta ya afya mipango tuliyopita nayo, kwenye mwaka 2015/2016, 2016/2017 na 2017/2018 tuliweka mkakati wa kuhakikisha kila Wilaya kwenye kila Kata na Kijiji tunakuwa na zahanati na vituo vya afya. Kwenye Mpango huu nimejaribu kuangalia naona tumejikita kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Rufaa za Kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo na hili, lakini lazima tufahamu kama tunashindwa kujenga vituo vya afya na zahanati za kutosha, kesi tunayoizungumza ya kuokoa maisha ya mama na mtoto hatutafanikikiwa kama tuta-*base* kwenye hospitali za Kanda peke yake. Sasa ni lazima

tukubaliane tunapozungumza namna ya kumsaidia mama na mtoto wasiendelee kupoteza maisha, tumeongeza dawa kwa kiwango kikubwa lakini lazima iendane na ujenzi wa zahanati na vituo vya afya kwenye kata na vijiji vyetu, ili tuweze kuwa na msingi imara. Tunapozungumza kumuokoa mama na mtoto tuwe tunamaanisha kutokana na haya ambayo tunayafanya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia hospitali za rufaa. Hospitali za Rufaa tumeona ujenzi unaendelea, lakini mikakati ya kuboresha, humu imetajwa Benjamin Mkapa, imetajwa Hospitali ya *Ocean Road*, zimetajwa hospitali nyingine ikiwemo na Muhimbili. Pia, nishukuru kwamba mmesema jengo la wodi ya mionzi kwa ajili ya ugonjwa wa kansa pale Hospitali ya Bugando limeshakamilika na ni kweli, lina mashine kubwa za kisasa zinafanya kazi na gharama yake ni kubwa. Mpango mkakati wa kujenga jengo la wodi ya wagonjwa ni upi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwepo bajeti miaka mitano iliyopita. Kila mwaka unawekwa mpango haukamiliki, unawekwa mpango haukamiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninakuomba ukienda pale *Ocean Road* kwenye asilimia 100 ya wagonjwa asilimia 60 ya wagonjwa wa saratani wanatoka Kanda ya Ziwa. Sasa ni lazima tufikiri namna ya kuiwezesha hospitali yetu ya Bugando ili iwe na uwezo wa kujisimamia tukihakikisha kwamba tunapeleka fedha kwa ajili ya kutengeneza na kufanya ukarabati wa vifaa hivi, lakini bila kusahau ujenzi wa jengo la wodi ambalo litatusaidia kuepukana na matatizo haya ambayo tunadhani tukifanya vizuri yanaweza yakatusaidia sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze juu ya habari ya miundombinu. Umezungumza juu ya habari ya miundombinu na *focus* yetu kubwa ni kwenye *TANROADS*. Lakini nikushukuru kwenye kitabu chako umesema, japo kwa uchache sana umeitaja *TARURA* kama chombo mbadala kinachokwenda kutatua tatizo la ardhi mijini na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa najaribu tu kuangalia harakaharaka...

MBUNGE FULANI: Barabara siyo ardhi.

MHE. STANLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kutatua tatizo la barabara Mijini na Vijijini. Kazi wanayokwenda kufanya sasa hivi hawa *TARURA* moja ya kazi wanayokwenda kufanya sasahivi kubwa, uko mradi wa *TSCP*, uboreshaji wa Miji na Majiji kwenye Manispaa miji karibu Nane nchi nzima. Wana fedha nyingi zaidi ya shilingi bilioni 183 kujenga barabara kilometa nne, kumi, kulingana na mji wenyewe jinsi ambavyo ulivyo, lakini mkakati wa kuifanya *TARURA* kiwe chombo chenye nguvu, kiwe chombo ambacho leo hata Mbunge anayehudhuria kwenye Baraza la Madiwani kinapokwenda kutoa taarifa na yeye ajue, leo katika wigo wa Halmashauri hakuna sehemu yoyote Halmashauri inatoa taarifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa lazima tuzungumze pamoja. Kwenye mkakati tulionao *TARURA* kama ni chombo kitakachotusaidia, mkakati wetu ni nini wa kukifanya chombo hiki kiwe na uwezo, kiwe na fedha, lakini sisi ambao tunahangaika na barabara za wananchi tupate nafasi ya kuhoji na kujua ni nini kinachofanywa na kazi yake inafanyika wakati gani, ili tuweze kushauri, tuweze kusaidia na tujue umuhimu wa chombo hiki. (*Makofi*)

Mwisho tuliongelea bajeti iliyopita iko Mikoa iliyotajwa maskini, ukiwemo Mkoa wa Mwanza, Kagera, Mara, Singida na mingine. Moja ya kitu ambacho kimenishangaza sijaona mkakati wowote kwenye kitabu hiki unaozungumzia namna ya kukuza na kuondoa umaskini kwenye Mikoa hii.

Sasa utakapokuja na taarifa kamili kwamba, huu ndiyo mpango, Mheshimiwa Mpango naomba tuone ni namna gani tumejipanga kupunguza matatizo na kuondoa umaskini kwenye hii Mikoa mitano ambayo zaidi ya Mikoa minne iko Kanda ya Ziwa, tunafanya nini kuhakikisha kwamba, tatizo hili linaondoka? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini sio mwisho kwa umuhimu kama muda utakuwa unaniruhusu ni suala la viwanda. Serikali tunaipongeza sana kwa kuamua kuchukua Shirika la *National Milling* ambalo lina vipuri vyake karibia nchi nzima maeneo mbalimbali. Sasa ni lazima tujue mkakati wa Serikali kwenye hizi *National Milling*, pamoja na kazi kubwa itakayofanya kununua mahindi na mpunga kuyaongeza thamani kwa kuyasaga, na mimi nimshukuru sana Mheshimiwa Jenista hapa, kwa namna ya kipekee kabisa walivyofikiria hii mifuko ya jamii kuwekeza fedha huku ambako zinakwenda kuonesha tija kwenye hawa watu ambao wanashughulika na haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini tukisimamia vizuri ajira kwa vijana zitapatikana, lakini wakulima wanaolia leo watakuwa na sehemu ya kupeleka mazao yao. Wakiyauza yanasagwa yanatengenezwa yanaongeza thamani na tunaona umuhimu wa Serikali hii kuwahudumia Watanzania hawa wakulima na wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze Serikali kwa namna ya kipekee kuanzisha mpango wa kurasimisha ajira zisizo rasmi kwa vijana, ikiwemo kuwaongezea uwezo, kuwawekea ujuzi na stadi za kazi, ni idadi kubwa sana ya vijana, zaidi ya vijana 3,400 wako kwenye vyuo mbalimbali ikiwemo Don Bosco na T/A. Tunaamini vijana hawa wakikamilika na mpango wa vijana milioni nne kufikia mwaka 2021, tunaweza kuwa tumefanya jambo la maana kama mipango yetu inavyozungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na mwisho tu niseme jambo moja kwamba, tuko hapa kwa ajili ya kujenga nchi yetu, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kambi ya Upinzani, leo amezungumza vizuri na hivi ndivyo tunavyotakiwa tuseme, kwa sababu lengo letu ni kujenga nchi moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na Mungu akubariki. Ahsante sana. *(Makofi)*

KUHUSU UTARATIBU

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa Kanuni ya 68(1) na ikisomwa pamoja na Kanuni ya 64(1)(f).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mchangiaji mmoja baada ya huyu aliyemaliza alikuwa anazungumza, kule kwetu Musoma anafahamika kwa jina maarufu la vocha, kila mtu mwenye simu anaweza kununua vocha. Alikuwa anazungumza hapa...

MWENYEKITI: Aah, naomba uifute hiyo kauli.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo hivyo.

MWENYEKITI: Naomba umtaje kwa jina, usitaje kwa jina la utani.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema nawashwa washwa hakuna aliyem-*interrupt*, asimame kwa Kanuni.

MWENYEKITI: Sasa unatoa Kuhusu Utaratibu, naomba uzungumzie Kuhusu Utaratibu usitaje jina la utani.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, asimame kwa Kanuni ajibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeele tafadhali. Kwa hiyo, wakati mchangiaji huyo alikuwa anazungumza amenishambulia sana na anasema mimi nawashwa-washwa. Sasa ukisoma Kanuni ya 64(1)(f) hairuhusu lugha hizo hapa Bungeni na sisi pia, tunaweza kusema hivyo hivyo kwa lugha za ukali, lakini tunakuwa na staha, mimi ni Mbunge wa Jimbo Serikali yenu hii ndiyo inashindwa kuwafanya *Barrick* iwalipe wananchi, mimi nafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vema akafuta kauli yake hiyo anayosema mimi nawashwa washwa, mimi siwashwi. Mimi ndiyo nawasha watu, mimi siwashwi. *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Heche, ninafikiri hiyo lugha ya kuwashwa washwa ni neno la kiswahili la kawaida, labda kama umeitafsiri wewe vibaya, lakini siyo vizuri pia kulitaja humu Bungeni kwa namna yoyote kwa sababu tafsiri zinaweza zikatoka vibaya. Kwa hiyo, naomba yule ambaye amezungumza asirudie tena na mtu yeyote asizungumze neno hilo kwa tafsiri mbaya.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Omary Mgumba.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie Mpango wa Serikali uliokuwa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nichukue nafasi hii nimpogeeze Mheshimiwa Mpango, Naibu Waziri wake na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Doto kwa kuandaa Mpango huu na kuletwa hapa Bungeni ili sisi Wabunge tuweze kutoa mchango wetu na pale kwenye mapungufu tuweze kuongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipogeeze sana Serikali kwa kuanzisha Wakala wa Barabara Vijijini *(TARURA)*. Ni wakala ambaye anaenda kutatua changamoto za miundombinu, hususan kule vijini kwetu tunakotoka. Hii maana yake nini kwamba, mawasiliano kati ya wakulima kutoka sehemu moja mpaka sehemu nyingine yanakuwa ni rahisi zaidi, lakini pia wakulima tunapata nafasi nzuri ya kupeleka mazao yetu sokoni na kupunguza gharama na kuongeza vipato kwa wakulima wetu. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipogeeze Serikali kwa kuanzisha na kuihamasisha Mifuko ya Jamii kuingia kwenye

kuwekeza katika viwanda, hususan kiwanda cha kielelezo, Kiwanda cha Mkulazi. Nawapongeza sana, kwa sababu kinaenda kujibu tatizo la nchi la upungufu wa sukari. Baada ya kiwanda hiki kuisha matatizo ya sukari yatapungua sana nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo nianze kuchangia kwenye Mpango, na mi mi kwa sababu natoka kijijini, ninatoka Wilaya ya Morogoro Vijijini lazima nitajikita zaidi kwenye suala la kilimo kwa sababu ndiyo suala linalogusa wananchi walio wengi katika maeneo yangu ni suala linalogusa Watanzania wengi. Kwa sababu zaidi ya Watanzania asilimia 70 wako vijijini na wanategemea kilimo kwa chakula pamoja na shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Mawenyekiti, nataka tu ni-*quote* vitu kidogo kwenye Azimio la Arusha, kule mwanzo kabisa. Azimio la Arusha lilizungumza kabisa maendeleo ya nchi yataletwa na watu, hayaletwi na fedha. Fedha ni matokeo sio msingi wa maendeleo. Ili tuendeleo tunahitaji vitu vinne, watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Watu tunao zaidi ya milioni 55, ardhi tunayo tena yenye rutuba na mito inayotiririka, siasa safi tunayo ambayo ni siasa ya ujamaa na kujitegemea, uongozi bora tunao, uongozi wenye sera nzuri za Chama cha Mapinduzi. Tatizo ni nini tunakwenda kwa taratibu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni kwamba tumewaacha watu wengi katika ushiriki wa kiuchumi katika Taifa letu. Watu hao ni nani? Ni wakulima wa nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najikita kwa wakulima kwa sababu kama nilivyosema ndiko ninakotoka huko, huwezi kusema nchi hii tutaendelea kama hatujaweza kuongeza kipato cha watu walio wengi wa Tanzania ambao ni wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa sababu kilimo chenyewe kinakua taratibu sana, lakini pia hata uwekezaji wa kilimo kwa Serikali bado uko chini sana kwa

hiyo, maana yake ni nini, tunawa-*sideline* watu wengi Watanzania wako nyuma. Kama kilimo kinakuwa taratibu maana yake kipato cha Watanzania wengi nacho kitakua taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Azimio la Arusha liliwahi kuzungumza kwamba tusipotahadhari kwa sababu watu wanasema ukizungumza unyonyaji watu wengi wanafikiria ubepari, lakini Azimio la Arusha lilizungumza kwamba, kuna unyonyaji mwingine kama hatukuchukua tahadhari na Serikali isipochukua tahadhari tunaweza kuzalisha unyonyaji mwingine ndani ya nchi kati ya wafanyakazi tunaishi mjini na wafanyabiashara tunaishi mjini na wakulima wengi wanaoishi vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu wakulima hawa ndio tunawategemea kwa ajili ya uzalishaji wa chakula. Wakulima hawa ndio tunawategemea kwa ajili ya uzalishaji wa malighafi za viwanda vyetu, lakini tutapata dhambi kama hatuwaangalii, hatuwatengenezei mazingira mazuri ya mazao yao kupata bei nzuri zaidi ili waweze kuwainua kimapato kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mmoja, mimi natoka Morogoro ni wakulima wazuri sana wa mpunga, mahindi na mbaazi, lakini leo hii wakati wa msimu wakulima ukianza kule Mikese, Tomondo, Kikundi na sehemu zingine tulikuwa tunauza mahindi debe moja zaidi ya shilingi 10,000, kilo zaidi ya shilingi 600, lakini leo hii mahindi ni shilingi 450. Wakati ule tunavuna ambapo kila sehemu Tanzania watu wanavuna sisi mahindi yalikuwa ni shilingi 600 leo hii hakuna msimu mahindi shilingi 450. Ndiyo maana ninaishauri Serikali kwamba tusipokuwa waangalifu tunazalisha unyonjaji, watu wa mjini kuwanyonya watu wa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao ya wakulima yanayozalishwa mahindi tunawalazimisha wauze bei ya chini ili watu wa mjini na wafanyabisahara tupate chakula kwa bei nafuu, lakini wenyewe wakulima bidhaa zinazozalishwa mjini kwenda vijijini bei zake ziko palepale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumzia sukari bei iko palepale, tukizungumza sabuni bei iko palepale, tukizungumza nguo bei ziko palepale, tukizungumza mafuta bei iko palepale, tukizungumza *tiles* bei ziko palepale. Mkulima anachotoka kununua bei zinapanda, mkulima kitu kinachomuingizia kipato bei zinashuka, bora zingeshuka kwa nguvu za soko kuliko kushuka kwa kutengeneza mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima hawa hawakulima mahindi haya kwa bahati mbaya, walilima kutokana na bei nzuri ya mwaka jana ambayo mahindi yalifika zaidi ya shilingi 2,000 ndiyo maana watu walihamasika mpaka wengine walichukua mikopo kwenda kununua, lakini leo kuna watu wanasema kuna wafanyabiashara wamenunua mahindi ndio wanaolalamika wanataka kufaidika, hili sio kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali ina dhana kwamba, wamepiga marufuku kwa sababu wafanyabishara wamenunua mahindi wameyahifadhi watafaidika sio sahihi, kwa sababu mkulima huyu anayelima kama nilivyosema mwanzoni anategemea kilimo kwa sababu ya chakula, anategemea kilimo kwa sababu ya kipato chake, anachokihifadhi ni chakula tu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ukikataza kwamba mahindi yasiwe na bei nzuri unatumia mkulima auze bei ndogo kwa wafanyabiashara na watu wengine. Hamna namna yoyote ataacha kuuza kwa sababu ndio kipato chake, lakini pia hana mahali pa kuhifadhi. Mtu amelima amepata gunia 200 ama 300 kuna mkulima gani wa kijijini ana uwezo wa kuhifadhi gunia 200? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama Serikali inaona kwamba kumsaidia mkulima ni kuzuia mahindi yasiende nje ya nchi, basi ni kuumiza kwa sababu wakulima ni lazima wauze. Ni kweli mahindi mengi yapo kwa wafanyabiashara na mahindi machache yako kwa wakulima, tangu lini imekuwa dhambi kufanya biashara kwenye nchi hii, tangu lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ajira hamna tunawahamasisha watu wakafanye biashara, wamechukua mikopo, wamechukua hela zao wamekwenda kununua, kwa mkulima anamuona ndio mwokozi wakati wa msimu ili kutatua changamoto zake, amemuuzia mahindi, ameyahifadhi, ana mkopo, leo unamwambia asiuze. Ndio maana Mheshimiwa Dkt. Mpango leo unaona mikopo chechefu inaongezeka kwenye mabenki. Inaongezeka kwa sababu miongoni mwa watu waliokopa benki ni hao wafanyabiashara wa mahindi na hao wafanyabiashara wa mazao tuliyopiga marufuku yasiweze kuuzwa nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kwa Serikali, na ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba, tutumie fursa ya mahitaji makubwa ya mahindi yetu Kenya, fursa ya mahindi yetu Sudan Kusini, fursa ya mahindi yetu kuhitajika Uganda, tuziangalie kama fursa tusiziangalie kama changamoto. Tutanue soko letu la mahindi tupeleke zaidi ili tuongeze uzalishaji zaidi miaka ijayo na mwakani, kwa sababu vuli hizi tukifika mwezi wa pili/tatu mahindi watu wakianza kuvuna vuli, mahindi yatakuwa zaidi ya shilingi 300, sijui kama tumemsaidia mkulima, hatujamsaidia mfanyabiashara zaidi ni kuwarudisha watu kimapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu Serikali fanyeni tafiti. Waruhusuni wakulima wakubwa na wafanyabiashara wauze mahindi haya ili waweze kulipa mikopo waliyokopa na kurudisha tija kwa uwekezaji wao kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ninalotaka kuzungumzia kwenye suala la mbaazi kwa sababu linatugusa, hapa ndiyo hii dhana ambayo ilikuwepo. Sasa hivi kuna baadhi ya watu wanafikiria kufanya biashara ni dhambi, akiambiwa kuna dalali ni mwizi, akiambiwa kuna wakala ni mwizi, akiambiwa kuna mfanyabiashara ni mwizi! Hatuwezi kujenga, hata hiyo kauli tunayosema kwamba tunataka tushirikiane na wafanyabiashara binafsi maana yake wafanyabiashara binafsi ni wafanyabiashara, sasa ukiwaweka kwenye kundi la wezi hatuwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna dhana ilijengeka kwamba ukiongea na mnunuzi wa mwisho basi utapata bei nzuri, hili ni kosa kubwa ambalo tullilifanya kwenye mbaazi mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuja hapa Waziri Mkuu wa India ambaye ndiye mnunuzi mkubwa na mwenye bei nzuri wa mbaazi. Serikali tukaongea naye, tukamwambia kwamba sisi ndiyo wazalishaji wakubwa wa mbaazi, tunazo mbaazi za kutosha ila walanguzi tu ndiyo wanakuja kutununulia hapa, njooni ninyi wenyewe. Kwa taarifa baada ya pale aliwaita wanunuzi wote 16 hapa nchini wa kununua mbaazi akawaambia naomba muanzishe wakala wenu, umoja wenu wa kununua mbaazi Tanzania na sitaki mtu yeyote anunue mpaka aje kwanza kupata kibali. Tumekiona mwaka huu, mbaazi kutoka shilingi 2,000 mpaka shilingi 150.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali mjue kwamba biashara ni taarifa, kama mimi nina taarifa wewe huna ndiyo mimi nitafanya biashara na kupata faida. Kama mnunuzi wa mwisho amejua kwamba kumbe mbaazi inapatikana Tanzania ana haraka gani ya kuongeza bei? Kwa hiyo, alichokifanya amefanya *syndicate* kwa wafanyabiashara wote wakubwa akawaambia huwezi kununua, kwa sababu mwanzoni bei zilikuwa zinapanda kutokana na uzoefu, weledi wa hao wafanyabiashara kwa sababu wamewekeza, wamechukua mikopo, wana wafanyakazi lazima wanunue. Wao wanafanya tafiti, wanajua mbaazi hizi zinahitajika lini, nani anahitaji na kwa kiasi gani. Kwa hiyo, wanajua kucheza na yule mnunuzi wa mwisho. Wana uwezo wa kununua bei kubwa kuliko iliyoko katika soko la dunia lakini wanajua nae anahitaji lini, wanazi-*hold* wanamwambia hatuna mbaazi kama hutaki bei yetu hatuuzi, ndiyo maana bei inapanda. Lakini wafanyabishara wale kwa sababu wanajua wanamdanganya kumbe wakati mwingine mbaazi ni nyingi lakini wanamwambia sharti kwa ajili ya kufanya biashara, hakuna!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri katika hilo. Baada ya hapo Dkt. Mpango na Waziri wa

Viwanda, kaeni na wadau/wafanyabiashara wa mazao mbalimbali mjue mahitaji ni nini, ubora gani unaohitajika, wakati gani. Kwa sababu wao wana uzoefu wa kutosha, wana mitaji hawategemewi Watanzania peke yake, wanategemewa dunia nzima wanunuzi ndiyo hao hao ukizunguka.

Kwa hiyo, wao wanaweza kujua kwamba kwa nini mbaazi zimeshuka na kwa nini mazao mengine yamepanda. Watu wengi wanataka kupotosha kusema kwamba biashara ya mbaazi imeshuka kwa sababu ya soko holela na biashara ya korosho bei inapanda kwa sababu ya udhibiti wa soko, siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya mbaazi inashuka kwa sababu ni zao la muda mfupi, zao la muda mfupi mwaka huu ukipata hela na nchi nyingine zitalima kwa sababu ni zao la miezi mitatu, miezi sita. Kwa hiyo, baadae *supply* inakuwa ni kubwa kuliko *demand*. Korosho, hata akikuta 4,000 huwezi kupanda leo ukavuna, tsubiri baada ya miaka mitano au kumi, hizi bei zilizoenda utakuja kuona hali itakuwaje. Ndiyo maana ushahidi unauona, Serikali ya India ndiyo wabanguaji wakubwa wa korosho baada ya Vietnam zaidi ya tani milioni moja lakini uzalishaji wao kila siku unashuka wanazidi ku-*import*...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mgumba.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Amina Mollel.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema, lakini kipekee kabisa niwapongeze wenzetu waliopata nafasi za uteuzi. Kipekee kabisa nimpongeze pacha wangu Mheshimiwa Ikupa Stella Alex kwa nafasi uliyoipata, nina imani na wewe na nina amini kabisa utasaidia kuishauri Serikali hasa katika masuala ya watu wenye ulemavu. Waswahili wanasema; kitanda unachokilalia ndio hapo utakapojua kunguni wake. Kwa hiyo wewe unajua, unajua adha na shida mbalimbali zinazowakabili watu wenye ulemavu. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze pia Serikali kwa sababu hata wale wanaochangia ni wanachangia kwa nia njema kuona kwamba ni kwa namna gani mpango huu utakwenda kunufaisha Taifa la Tanzania na kufanya uchumi wetu uendelee kukua. Kwa mujibu wa Benki ya Dunia ni kweli kwamba katika Bara la Afrika uchumi wa nchi ya Ethiopia unakua kwa kasi sana lakini pia Tanzania tunakua kwa uchumi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Tanzania kuwepo katika ukuaji wa uchumi, bado pato la wananchi wa kawaida ni dogo sana kwa maana kwamba maisha ya wananchi wa kipato cha chini hali zao bado ni duni sana. Kwa hiyo, katika mpango huu tulitarajia kuona kwamba mikakati madhubuti ambayo itakwenda kusaidia mbali ya kukua kwa Pato la Taifa, lakini tuone ni kwa kiasi gani kwamba mpango huu unasaidia kukuza pato la mwananchi wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona pia imezungumzia mfumuko wa bei, lakini katika mfumuko wa bei huu pamoja na kwamba wanasema umeshuka, lakini je, kwa kipato cha mwananchi wa kawaida pato hili limeshuka kwa kiasi gani. Tunaona kwamba bado hali iko pale pale. Kwa hiyo tuone kwamba ni kwa jinsi gani tunaboresha maisha ya wananchi wetu, kwa mfano kwa kuangalia ni vitu gani ambavyo ni muhimu kwa mwananchi wa kawaida. Bei ya mafuta inapokuwa juu ni dhahiri kabisa kwamba inaumiza watu wengi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeona kwamba katika muda wa mwaka mmoja, bei ya sukari imekuwa ni tatizo kubwa sana ambapo bei yake pia imekwenda mpaka wakati mwingine imefika shilingi 3,500 mpaka shilingi 4,000. Sukari inategemewa na kila mwananchi wa kawaida, kwa hiyo tunapozungumzia kwamba mfumuko wa bei umeshuka, tuangalie kwa huyu mwananchi wa kawaida umeshuka kwa kiasi gani, tunawasaidiaje wananchi wa kawaida ili uchumi wao na wao pia uweze kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite katika suala zima la watu wenye ulemavu. Hapa katika ukurasa wa 53 ambapo wameweka vijana, ajira na wenye ulemavu nilitarajia kuona mambo mengi ambayo yangekuwa na manufaa, mpango huu ungeeleza ni kwa jinsi gani unakwenda kujikita kusaidia kundi zima la watu wenye ulemavu. Kwa mfano, hatuna idadi kamili ya watu wenye ulemavu na ili upange mpango wako uweze kukamilika kwamba utafanya nini kwa kundi fulani au kwa vijana ni vema basi tujue kwamba je, tuna watu wangapi mfano walemavu wasioona, kwa mfano tuna walemavu wa viungo, viziwi na wengine wengi. Kwa kujua idadi yake tunapanga mipango kulingana na idadi ya watu ambao tunakwenda kuwasaidia kukwamua kipato chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu tunapozungumzia pato la chini na hasa kwa kundi la watu wenye ulemavu ni watu ambao maisha yao ni ya duni sana. Hasa unapokwenda vijijini, hali zao bado ni duni. Katika mpango huu nilitarajia tuone kwamba kulingana na idadi hii ni mikakati gani Serikali mpango huu unakwenda kuwasaidia vipi watu wenye ulemavu.

Kwa hiyo, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuona kwamba ni kwa jinsi gani mnapokwenda kuongezea zile nyama ambazo zimechangiwa na Wabunge tuone kwamba basi mpango huu unakwenda kuwasaidiaje watu wenye ulemavu badala ya jinsi mlivyoweka hapa kwamba vijana, ajira na wenye ulemavu. Wenye ulemavu wana mahitaji yao muhimu tofauti ni vijana, lakini wana

mahitaji yao muhimu tofauti na wengine. Huwezi kulinganisha na kijana wa kawaida. Tunawawekea mipango gani, mikakati gani ya kuwasaidia watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali kwa sababu suala la chakula limezungumziwa sana, naomba nizungumzie kwangu mimi hasa katika suala la kuboresha kilimo. Kilimo ndiyo uti wa mgongo. Wengi wetu hapa tumesomeshwa na kilimo, pia na mifugo tumetoka huko. Sasa tunapoelezea katika mpango huu tungeona kwamba katika kilimo tunaboresha vipi kilimo chetu. Ni kweli wananchi wanalima, lakini kilimo chenyewe bado ni kilimo duni. Kutokana na mabadiliko ya tabianchi hali ya hewa hivi sasa baadhi ya maeneo mvua zimekuwa shida. Je, tunawashauri vipi wananchi wetu ili walime kulingana na hali halisi ya mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunaangalia suala la pembejeo ambalo kwa wakati mwingine limekuwa likifika kwa muda ambao sio sahihi, je tunajipangaje? Miundombinu ni suala muhimu sana kwa sababu hata wanapozalisha kama miundombinu sio rafiki, sio mizuri mfano barabara. Kule kwetu ukienda kuna baadhi ya maeneo vijana wanalima nyanya sana, lakini kwa sababu barabara ni mbaya na wachuuzi wanaokwenda kuchukua katika maeneo yale wananunua kwa bei wanayotaka, kwa hiyo, bado hatujawasaidia vijana wetu kuwakomboa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo katika mpango huu, tuone kwamba kutakuwa na mikakati ya elimu kwamba katika eneo fulani kwa mfano yanajulikana maeneo ambayo ukienda Mkoa wa Rukwa, Katavi, ukienda Ruvuma ni baadhi ya maeneo ambayo wanapata mvua nyingi. Je, maeneo yale ambayo hawapati mvua tunawaandaaje wananchi wetu ambao tunajua kabisa kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo, tunawaandaaje ili wao waweze kulima mazao kulingana na mvua. Waweze kulima mazao ambayo yataendana na eneo husika, katika mpango huu sijaona kwamba ni kwa namna gani tunaweka hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mitaji ni muhimu, siku hizi kila kitu kinahitaji mitaji, je, tunaandaaje kuhakikisha kwamba tunawawezesha. Mfano, kama ni vijana ambao ndiyo nguvu kazi tunawaandaaje kwa mitaji ili vijana hawa tunataka kwamba wajajiri wao wenyewe na kwa sababu tunakwenda katika sera ya viwanda, tunawaandaaje kwamba ili hizo malighafi hao vijana wanaokwenda kujajiri wenyewe, je, mitaji wanapata wapi. Katika mpango, mpango haujajeleza wazi kwamba vijana hawa tunawaandaaje katika suala la kilimo na kwa sababu kilimo ndiyo ajira pekee ambayo inaweza kuwaajiri vijana wengi wakajajiri wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji pia kwa sababu hata hawa wakulima wadogo wadogo bado wanahitaji wawekezaji wakubwa ili kwa namna moja kila mmoja anamuhitaji mwenzake. Mipango gani inawekwa ili kuvutia hawa wawekezaji ambao na wao pia waweze kuwasaidia hawa wakulima wadogo wadogo. Vyote hivyo ni vitu ambavyo Mpango ungeweza kueleza kwa uwazi ili basi yeyote yule anayekamata Mpango huu na yeye anasoma anajua kabisa kwamba nchi imeandaa kitu fulani, kwa hiyo vijana au wananchi tujiandae kwa jambo hili kutokana na Mpango jinsi ulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuboresha ufugaji na kwa mfano, tuliona hivi karibuni bilionea mmoja Bill Gates ambaye anaamini kabisa kukuza uchumi wa wananchi ukiwawezesha katika suala zima la ufugaji kwa mfano kuku. Kuku hivi sasa ni mali, kuku ni pesa. Tunawaandaaje wananchi wetu ili kuhakikisha kwamba na wao wanajilingiza huko kwa kuamini kabisa kwamba ukiwa na kuku hata watatu, nakumbuka siku moja Mheshimiwa Waziri Mkuu alipofika kijijini kwetu alisema kwamba wananchi ili kulipia umeme wa REA ukifuga kuku watatu tu tayari umeshalipia gharama ya kupata umeme wa REA. Je, sasa katika mpango ambao ndiyo tunategemea huku tunawaandaaje wananchi ili hawa wananchi waweze kujikita zaidi katika suala zima la ufugaji kwa sababu ufugaji kama nilivyosema kuku ni pesa. *(Makofi)*

Vilevile katika suala zima la uvuvi kuna ufugaji wa samaki hivi sasa. Ufugaji wa kisasa ambao ili kukuza mitaji yao na kipato cha wananchi pia nilitarajia kwamba Serikali yenyewe imejiandaa vipi. Kwa hiyo, katika Mpango huu tungeweza kuona kwamba wananchi watasaidiwa katika ufugaji wa samaki ili kuhakikisha kwamba tunapunguza makali ya maisha jinsi yalivyo kwa hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeona kuna uvuvi katika Bahari Kuu. Mfano, zipo meli nyingi zinakuja hapa nchini na zinakwenda katika bahari kuu kuvua. Je, zile leseni ambazo wanapewa je leseni hizo zinatolewa kulingana na ukubwa wa meli jinsi ulivyo au watu wanapewa tu wanakwenda kuvua kadri yeye anavyoweza na ukubwa wa meli yenyewe. Kwa hiyo, kama tunataka kukuza uchumi wetu katika suala la uvuvi, kwenye Bahari Kuu basi tuone kwamba hizo leseni ziendane kulingana na ukubwa wa meli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa sababu Serikali yetu hivi sasa imeweza kununua ndege, basi tuone ni wakati sasa wa kufikiria mbali zaidi kuwa na meli ya kwetu wenyewe ya uvuvi ili tuweze kuvua wenyewe kwa sababu mahitaji ya samaki hivi sasa watu wengi wanaondoka katika ulaji wa nyama za ng'ombe na ulaji wa nyama nyingine, kwa hiyo wanakimbilia zaidi kwenye samaki na kuku. Kwa hiyo, hili Mheshimiwa Waziri wa fedha jambo ambalo ningetarajia kuliona katika Mpango pia kwamba Serikali katika miaka miwili/mitatu ijayo pengine tumejikita katika kununua meli yetu wenyewe ili basi nasi katika uvuvi wa Bahari Kuu tuweze kwenda kuvua wenyewe na sio kila siku wavue tu wageni wanaokuja hapa nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ile Sera ya Huduma za Fedha kwa ajili ya wananchi. Tuone kwamba hivi sasa inafanyiwa kazi ili basi wananchi waweze kufaidika na hilo. Kwa mfano hili tuangalie kwenye Halmashauri zetu kwa sababu tayari tunawaandaa wananchi ili wananchi waweze kuzalisha kwa wingi. Mfano, katika viwanda, tunapokwenda kwenye viwanda, je, tumewaandaaje katika suala zima mfano kwenye jamii tumeandaaje katika wataalam wa afya

maji vijijini ili wananchi basi wawe na afya njema. Vyote hivi ni vitu ambavyo vinahitaji kuzingatiwa kwa umakini kwa sababu wakati mwingine watu wetu wanaangamia kwa kukosa maarifa. Kwa hiyo, kukiwepo na mipango thabiti na katika Halmashauri zetu, kwa mfano Maafisa Biashara hawa wakawezesha kuandaa vikundi kwa ajili ya watu wenye ulemavu na kwa sababu sasa hivi kuna ile asilima nne kwa wanawake, asilimia nne kwa vijana na asilimia mbili kwa watu wenye ulemavu.

Kwa hiyo, Maafisa Maendeleo Jamii na wao wahakikishe kwamba wanaandaa na kutoa mafunzo kwa makundi yote hayo ili kuhakikisha kwamba kila mmoja anajitegemea na kuongeza pato yeye mwenyewe lakini pia katika kukuza uchumi wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la mikopo kwenye mabenki ni kweli kwamba tumeona Benki Kuu kwa mfano imepunguza riba kuanzia asilimia 16 lakini vilevile ikashuka mpaka asilimia 12 na sasa asilimia tisa, lakini bado mabenki yanatoza riba kubwa mfano, mpaka asilimia 20, 22. Sasa tunawaandaa hawa wananchi kama kweli Benki Kuu imepunguza kutoka asilimia 16 imekwenda asilimia 12, imekwenda asilimia 9 kwanini mabenki yaendeleo kutoza riba ya asilimia 20 mpaka 22 huku sio kumsaidia mwananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili naishauri sana Serikali yangu kwa upendo kabisa kuhakikisha kwamba kama kweli na hili pia ndiyo maana tumeona kwamba kutokana na jinsi uhaba hivi sasa biashara nyingi ambazo hazijaenda vizuri lakini pia wananchi wengi hawana fedha. Tumeona jinsi ambavyo watu wanauziwa nyumba. Kwa hiyo, kama Serikali katika Mpango tuweke kwamba ndiyo muda umefika muda fulani mtu aongezewe kulipa ili basi kuepusha watu kuwatia katika umaskini. Tukifanya hivi tutawasaidia sana wananchi wetu.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Amina, muda umeisha.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Kengele imegonga? Namalizia *point* moja ya mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la ufugaji, ninaiomba Serikali na hasa katika mpango huu kwa sababu wakati mwingine tunawatia wananchi umaskini.

Mimi ni mtoto ambae nimekulia kwenye familia ya ufugaji. Tumeona juzi huko Rukwa wakati mwingine wafanyakazi au hawa Watumishi wa Serikali wawe na moyo wa huruma. Tumeona wanawafungia ng'ombe kwenye mazizi kweli? Wanawafungia ng'ombe miezi sita, mwaka ng'ombe wanakufa na wengine bado wanaendelea kuwepo pale wazima jamani! Hivi ni kwa sheria zipi? Je, hawa watu tunawafikiria vipi? Kuna mambo mengine ambayo kwa kweli tunaomba wakati mwingine tutanguliwe na huruma zaidi katika kuwasaidia wananchi wetu. Hali ni ngumu, unaenda tena kummaliza huyu mtu. Tuwe na huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe pia na nakupongeza sana Mheshimiwa Kigwangalla, Waziri wa Maliasili, wananchi wa Arusha tumechoka na mgogoro wa Loliondo. Kwa hiyo, miongoni mwa mambo ambayo tunakuomba yaishe sasa ni mgogoro wa Loliondo tumechoka nao. *(Makofi)*

Mhshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya nakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Amina Mollel. Kamati imemaliza muda wake kwa leo, Bunge linarejea.

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru kwa kazi nzito ya leo na namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie kesho tuje na mawazo mapya ya kuboresha mpango wetu badala ya kulaumu tu.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi/Kicheko)*

(Saa 1.45 Jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Ijumaa, Tarehe 10 Novemba, 2017 Tatu Asubuhi)